17ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 28 Juni, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 93

Ongezeko la Bei ya Umeme

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Kny: Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu) - Aliuliza:-

Inadaiwa kuwa katika kutafuta suluhu ya ongezeko la bei ya umeme Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi – Zanzibar iliiandikia barua Afisi yako juu ya ongezeko hilo, na Afisi yako iliwasiliana na Afisi ya Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kuomba Zanzibar ilipe bili ya umeme kama wanavyolipa wenzetu wa Tanzania Bara (kwa asilimia 21.7%). Afisi ya Waziri Mkuu ililikubali ombi hilo na kuitaka Wizara ya Nishati, Tanzania Bara kutekeleza suala hili kama tulivyoomba. Lakini inasikitisha kuona kwamba hadi leo bado agizo la Waziri Mkuu halijatekelezwa.

(a) Je, Mhe. Waziri, kwa sura na picha hii mnawaeleza nini Wananchi wa Zanzibar?

(b) Kwa kuwa suala hili Wizara zetu mbili – Afisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano na Afisi ya Waziri Kiongozi limeliingilia kati kwa njia ya mazungumzo na kulitolea maamuzi, lakini kwa kuwa maamuzi hayo hayakutekelezwa na taasisi husika. Huoni kwamba hizo ni kasoro kubwa ya kiutendaji na inaashiria kupinga au kukataa agizo la Serikali, jambo ambalo ni utomvu wa nidhamu?

(c) Zanzibar kuendelea kutozwa au kulipishwa asilimia 168% tofauti na Tanzania Bara kinyume na agizo la Waziri Mkuu, huoni kwamba hizo ni dosari na kasoro na kero kwa Muungano wetu?

(d) Wananchi wajenge hisia gani na wawe na matumaini na imani gani juu ya Muungano kwa tabia kama hiyo ya upande mmoja wa Muungano kuunyonya, na kuunyanyasa upande wa pili wa Muungano?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 93 lenye kifungu a,b, c na d kama hivi ifuatavyo:-

Kabla sijamjibu Mhe. Mjumbe swali lake, naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli afisi yangu iliwasiliana na Afisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuomba Zanzibar ilipe bili ya Umeme kama wanavyolipa wenzetu wa Tanzania Bara (kwa asilimia 21.7%) Afisi ya Waziri Mkuu ilikubali ombi hilo na kuitaka Wizara ya Nishati na Madini ya Tanzania Bara kutekeleza suala hili kama tulivyoomba.

Mhe. Spika, naomba kutoa jibu kwa Mhe. Mjumbe kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali bado ina imani kuwa uamuzi na maelekezo waliyopewa Wizara ya Nishati na Madini ya Tanzania Bara kuhusu utaratibu wa malipo ya umeme kwa upande wa Zanzibar utatekelezwa. Kwa hivyo, tunawaomba wananchi waendelee kuiamini serikali yao kwa juhudi zake za kutatua kero zinazowakabili, hasa katika masuala yanayogusa pande mbili za Muungano;

(b) Mhe. Spika, iwapo Taasisi husika itaacha kulishughulikia agizo hili ambalo limeshapata baraka za Rais wa Jamhuri ya Muungano, itakuwa sio jambo zuri na serikali haitakaa kimya kuona maamuzi yake hayatekelezwi;

(c) Mhe. Spika, serikali zetu mbili zimeshatoa maagizo kwa viongozi wa Mashirika ya Umeme ya pande zote za Muungano, wakutane kulipatia ufumbuzi suala hili, ili ongezeko la malipo ya umeme kwa Zanzibar liwe kwa asilimia 21.7% sawa na ilivyo kwa Tanzania Bara badala ya asilimia 1.68% kama *bill* inavyoletwa hivi sasa; na

(d) Mhe. Spika, pamoja na kasoro zinazojitokeza Muungano wetu bado ni imara, vikao vyetu vya kutatua kero bado vinaendelea na tutahakikisha hatua kwa hatua tunazipatia ufumbuzi kero zote kwa manufaa ya Wazanzibar na Watanzania wote kwa jumla.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, migogoro ya kibiashara ndio chanzo cha migogoro kutokana na Muungano wetu. Tukizingatia kwamba kila mtu analilia haki yake katika sehemu yake. Lakini bahati nzuri tuliyokuwanayo katika nchi yetu Tanzania Bara na Zanzibar tumeweka TRA moja kwa ajili ya kuondoa manung'uniko na hasa upande mmoja ikidai kwamba Zanzibar inakuwa inakuwa bei ndogo na Tanzania Bara bei kubwa. Kwa hivyo, kuwekwa chombo hiki ili kuleta umoja.

Swali langu liko hapa. Kwa kuwa Shirika la Umeme linanunua umeme Tanzania Bara yaani TANESCO na sisi tunategemea kwamba ni wateja wakubwa kuliko wengine wowot katika nchi hii.

(a) Ni kitu gani ambacho kimewasababisha kupandisha bei kiasi hicho?
(b) Je, huko si kurudisha nyuma maendeleo ya Zanzibar hasa kwenye sekta ya utalii na mambo mengineyo?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, mimi nakubaliana nasa na suala la Mhe. Mjumbe kwamba hiki kinachofanywa na TANESCO sasa hivi ni moja katika kudhohofisha hasa katika mambo yetu haya yanayohusu Muungano.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umeme ambao unatoka Tanzania Bara, miundombinu hii tuliifanya sisi wenyewe kwa gharama zetu SMZ kwa asilimia 100. Kwa hivyo, bado TANESCO hawana sababu ya kutupandishia *bill* bila ya sababu ambazo ni za msingi.

Wateja ambao pengine wangeweza kuzidishiwa *bill*, labda hata kama ile miundombinu wangekuwa wametuletea wao. Lakini miundombinu imewekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sisi kitu ambacho tunauziwa ni umeme, hatuuziwi miundombinu. Kwa hivyo, hatuna sababu kuwa Wazanzibari tuletewe *bill* kubwa. Ndio maana ile *bill* ambayo tulikubaliana ambayo wanalipa wenzetu, mpaka sasa hivi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia Shirika la Umeme Zanzibar, ndio *bill* ile ile ambayo inalipwa.

Kwa hivyo, bado kama nilivyosema tunaendelea na vikao vyetu na katika kikao chetu kilichopita cha kero za Muungano Bwawani, tuliliuliza hili suala na Mhe. Waziri wa Nishati na Madini alikiahidi kikao kwamba suala hili atalishughulikia na litapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi kuwa, kwa kuwa Waziri Kiongozi hana uwezo wa kikatiba katika mambo ya Muungano, tokea pale Rais wa Zanzibar alipoondolewa kuwa ni Makamu wa Rais. Je, huoni kwamba hili ni tatizo la kwamba Waziri Kiongozi hana nguvu za kikatiba kujadili mambo ya Muungano na ndio mambo haya yakakwama.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameunda chombo cha kushughulikia na kutatua kero za Muungano, kwa hivyo chombo kile ni chombo ambacho kina nguvu na ndio maana kuna baadhi ya kero nyingi ambazo zilizokuwa linayakabili masuala yetu ya Muungano, basi tumeanza kuyapatia ufumbuzi hatua kwa hatua.

Kwa hivyo, kama nilivyosema kuwa suala hili hata Waziri Mkuu tayari ameshatoa kauli yake, kwa sababu kama ingekuwa Waziri Kiongozi amewaandikia TANESCO, basi tungesema kweli katika mambo ambayo sio ya Zanzibar Waziri Kiongozi angekuwa hana nguvu. Lakini hata Waziri Mkuu vile vile kwa mambo yanayohusu Zanzibar na yeye anakuwa hana nguvu pia.

Kwa hivyo, suala hili kwa kuwa limekwenda katika vikao na Mhe. Waziri Mkuu ameshalitolea agizo kwa barua rasmi. Tatizo la TANESCO ni kwamba hawajaweza kutii amri wa Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali kule Tanzania Bara, kwa kweli huu sio utendaji mzuri kama watumishi wa serikali, kwa sababu yule ni kiongozi mkubwa ambaye amewekwa na Mhe. Rais kusimamia majukumu yote ya serikali. Kwa hivyo, bado naomba tena tuamini kuwa suala hili mimi naamini tutalipatia ufumbuzi.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi kupata kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Spika, ikiwa kama Rais ameshatoa tamko na yeye ndio kiongozi wetu tunayemfuata kwa kila kitu ambacho tumekubaliana naye. Vile vile nikiwa kama mwanakamati wa kamati hii, miadi alituwekea yeye mwenyewe waziri tukatoka na kumfuata Waziri Ngeleja, na tulipofika alitukimbia kabisa, hakutaka kuonana na sisi, halafu akatuwekea mtu ambaye hatoweza kuliamua hili suala na muamuzi ni yeye. Kwa sababu yeye *answerable* wa hili. Tulikataa kuonana naye na tukarudi.

Je, Mhe. Waziri ataniambia nani ambaye atatoa *suggestion* ya suala hili, wakati kero hii imetutosha na deni linaongezeka na yeye anasema bado tunaendelea na ufafanuzi. Ikiwa Rais hataki kutii amri ya Rais, ni nani mwengine ambaye atamtii.

Mhe. Spika: Hapo Mhe. Asha Moh'd Hilal umechanganya kidogo. Ikiwa nani?

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Ikiwa waziri muhusika, hataki kutii amri ya Rais na sisi wana kamati tumemfuata pia akatukimbia, inaonesha huyu hataki kutoa *suggestion* kuhusu hili. Je, Mhe. Waziri atatuambia nini kwa hili na kila siku deni linaongezeka na wananchi wanazidi kuatilika kwa hili, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Nafikiri ilikuwa ni amri ya Waziri Mkuu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwanza niwape pole sana wajumbe wetu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kwa namna walivyopata usumbufu wa kuweka miaka ya kumuona Mhe. Waziri wa Nishati na Madini wa Tanzania Bara, kwa bahati mbaya, mimi sitaki kusema amekimbia. Lakini kwa bahati mbaya alidharurika akamleta Naibu Waziri. Lakini kutokana na uzito wa suala lenyewe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati nzito ya Mawasiliano na Ujenzi, alikataa kuzungumza na Naibu Waziri na akataka kuonana na Mhe. Waziri mwenyewe. Kwa hivyo, kwa hilo nakupeni pole kwa usumbufu.

Lakini Mhe. Waziri mwenyewe muhusika kama nilivyosema katika kikao cha Juni, 2 kilichofanyika Bwawani cha kero za Muungano, yeye mwenyewe alikuwepo na suala hilo hata mimi nilimuuliza na akaagizwa na Mhe. Waziri Mkuu, "kwa nini lile agizo la Waziri Mkuu halikuweza kutekelezwa mpaka leo".

Mhe. Waziri yeye alivyosema pale katika kikao cha Bwawani, alisema yeye anavyoamini kwamba baada ya barua ya Waziri Mkuu agizo lile TANESCO wangelitekeleza, lakini kwa bahati mbaya mpaka siku ile katika kikao tukamthibitishia kuwa *bill* inayoletwa katika Shirika la Umeme ni ile ile *bill* ya asilimia 168. Kwa hivyo, ndio maana Mhe. Waziri kwa kuwa alikuwa hana uhakika, ndi akaahidi kwamba atakwenda kukutana na uongozi wa TANESCO ili kuweza kulipatia ufumbuzi suala hili na aliahidi atatupatia kwa maandishi.

Mhe. Spika, bado tunaendelea kulifuatilia suala hili kama nilivyosema, mimi naamini katika vikao vyetu tutalipatia ufumbuzi bila ya kuwapatia usumbufu wananchi wetu.

Nam. 11

Zanzibar Kuwa ZRB na TRA

Mhe. Said Ali Mbarouk: (Kny: Mhe. Nassor Ahmed Mazrui) - Aliuliza:-

Wakati Tanzania Bara kuna TRA tu ambayo inasimamia kodi za Forodha na ongezeko la thamani hapa Zanzibar, Kodi ya Ongezeko la thamani linashughulikiwa na TRA pamoja na ZRB.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa utaratibu huu wa kodi moja kukusanywa na taasisi mbili unafanya kazi ya kurejea (Duplication) na unaleta usumbufu kwa wafanyabiashara pamoja na Wawekezaji?

(b) Kwa nini shughuli hizi hazifanywi na taasisi moja tu?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Barza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, naomba ieleweke kwamba kodi za ndani zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yaani *Tanzania Revenue Authority*, kwa upande wa Zanzibar ni tofauti na zile kodi za ndani zinazokusanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), yaani *Zanzibar Revenue Board* kwani Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar, inakusanya kodi za ndani zile zinazojulikana kama ni kodi za Mapato yaani (*P.A.Y.E. na Cooperate tax*) ambazo ni kodi za Muungano na Bodi ya Mapato Zanzibar inakusanya kodi za ndani lakini ni zile zinazojulikana kama ni kodi ya Mlaji *(Consumption tax*) kwa upande wa Tanzania Bara kodi zote hizi za ndani iwe kodi ya Mlaji au kodi za Mapato zote hizi zinakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania; na

Mhe. Spika, Utaratibu huu wa ukusanyaji wa mapato kutoka maeneo husika, umewekwa kisheria na kwa wakati huo ilipotungwa sheria hio hapakuwepo usumbufu unaoelezwa.

b) Mhe. Spika, kwa sasa hivi, bado Sheria na Kanuni za ukusanyaji mapato Tanzania zinatuelekeza kwamba vyombo hivi vigawane namna hii nilivyotaja katika ukusanyaji wa mapato, mpaka hapo

tutakapo badili sheria hii ndio kodi hizi zitaweza kukusanywa na Taasisi moja kama inavyopendekezwa. Utafiti Mhe. Spika, kama tulivyoshauriwa hapo awali, unaendelea kufanywa kuangalia uwezo wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), kukusanya kodi ya Mapato ambayo kwa sasa inakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ili iihame kodi hiyo kuipeleka kukusanywa na ZRB. Utafiti huu utakapokamilika na (ZRB) kupewa jukumu hilo, kwa kiasi fulani ni imani yetu kwamba ule usumbufu ambao Mhe. Mjumbe ameulizia ambao upo kwa hivi sasa utawezakuondoka, ahsanate Mhe. Spika.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kodi ya *income tax* katika nchi zote inajulikana kama ni *inland revenue*. Pia hapa kwetu ni vile vile *Zanzibar Income Tax*, imo katika fungu la *inland revenue.* Masuala ya kodi za ndani kwa Zanzibar zinasimamiwa na ZRB.

(a) Sasa inakuwaje muda wote huo na kwa miaka yote hiyo kodi hii imeachiwa isimamiwe na TRA; na
(b) Pamoja na manung'uniko yote ya wananchi kwamba kusimamiwa na vyombo viwili vya taasisi za kodi kunaleta usumbufu mkubwa kwao na pia kunasababisha kutokuwa na imani na utowaji wa kodi. Je, hatuoni kuwa hii ni sababu tosha kwa serikali na kwa wizara yake kuona kwamba iharakishe kubadilisha sheria ili ZRB iwe ni chombo pekee cha ukusanyaji mapato hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kama nilivyosema hapo awali kwamba kodi hii ya *income tax* ni *inland revenue*. Huko nyuma ni kweli kabisa kwamba ilikuwa ikikusanywa na TRA na kuondoka hapa nchini kwetu.

Lakini kama Mhe. Spika, tunavyofahamu kuwa hiyo ilikuwa ni kero moja wapo kubwa ya Muungano ambayo Waheshimiwa Wajumbe mlikuwa mkituhimiza sana serikali na Wizara ya Fedha na Uchumi kuitetea kodi hii, hasa wafanyakazi wale kwamba wanafanyakazi Zanzibar basi kodi hii ibaki Zanzibar. Kwa hivyo, hili kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan kuwa ni moja ya mafanikio ya hayo mazungumzo yetu kati ya Mhe. Waziri Kiongozi na Mhe. Waziri Mkuu chini ya Mhe. Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kodi hiyo sasa tumefanikiwa itakusanywa Zanzibar na itabaki Zanzibar.

Kuhusu sheria Mhe. Spika, kwa kweli ni sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa tunafanya utafiti ili kukamilika na hili tutakwenda nalo sambamba, tutawaomba wenzetu kama tumeshafanikiwa huku basi na hii sheria nayo tuirekebishe.

Mhe. Spika: Ahsate sana. Mhe. Waziri jitayarishe na mambo ya kikatiba.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru sana na kweli kama ulivyosema, mimi nataka kunukuu katiba. Mhe. Spika, kwanza mimi napongeza juhudi za serikali za kukaa wakazungumza, wakafikia na wakakubaliana kwamba kodi hii sasa hivi itumike Zanzibar ni jambo zuri.

Mhe. Spika, lakini kwa kuwa makubaliano hayo sio makubaliano rasmi ni makubaliano ya kirafiki. Kwa sababu katiba bado inaitambua kodi hii kwamba ni kodi ya Muungano. Je, huoni kuwa kwa sababu wameshakubaliana kuwa kodi hii yote itumike Zanzibar, kwamba sasa wakati umefika hata katiba yetu kuibadilisha tukaitoa katika Muungano hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, hatua za mwanzo kwanza ni makubaliano. Tulikuwa tukihangaika siku zote tutafuta haya makubaliano. Sasa kimsingi makubaliano tumeafikiana na tumeyapata, sasa hatua inayofuata ndio hiyo sheria na watu wanaoji-*commit* kwa hilo sio watu wadogo.

Wakiwemo, Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mhe. Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na huku Mhe. Waziri Kiongozi wa Zanzibar ni watu wakubwa sana. Kwa hivyo ni kuelekeza tu utaratibu ufuate kisheria.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kuhusu hawa TRA. Je, hawa watu wanaotoa bidhaa kutoka nje wakaleta Zanzibar na wakalipa ushuru kwa *computerize*, wakisha wakalipishwa tena ushuru, na makubaliano yalifanyika na bado wanafanya hivyo hivyo. Je, ni lini watamaliza suala hili?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nafikiri Mhe. Asha Moh'd Hilal labda tulipokuwa tunalijibu hili swali ambalo niliwahi kuulizwa, basi alikuwa hayupo kidogo.

Mhe. Spika, nataka kusema kwamba katika moja ya makubaliano tulioafikiana na wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba

kuanzia sasa bidhaa yoyote inayoingia katika bandari yoyote au uwanja wa ndege wowote, yaani ile *port of entry* wazungu wanasema inahesabika imeshaingia Tanzania, kwa hivyo unawajibika kuchangia kodi moja tu. Sasa hiyo aliyozungumza Mhe. Asha Moh'd Hilal wazungu wanasema *is history* yaani yamepita hayo na huko tumeshafunga *chapter* hiyo.

Tunashukuru sana mazungumzo haya, kero hii moja kubwa sana ambayo ilikuwa inatukabili pamoja na wafanyabiashara wetu, sasa hiyo imeondoka, ahsante Mhe. Spika.

Nam. 41

Malipo ya Wafanyakazi Kupitia Benki na Kuwekewa Bima

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Hivi sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawalipa wafanyakazi wake wengi mishahara yao kupitia benki ili kupunguza usumbufu pamoja na kujikinga na wimbi la wizi wa mishahara. Vile vile wafanyakazi hao wamewekewa Bima hasa vikosi vya ulinzi na usalama.

(a) Je, Mhe. Waziri suala la wafanyakazi wetu kulipwa mshahara yao kupitia benki na kuwekewa Bima, serikali yetu imelipa uzito gani?

(b) Je, huoni kuwa utaratibu huu unapunguza matatizo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 41 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, suala la wafanya kazi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kulipwa mishahra yao kupitia Benki limepewa uzito mkubwa na utekelezaji wa hili kwa sasa umeshaanza. Kwa sasa hivi tayari baadhi ya taasisi za serikali zimeshaanza utaratibu kwa wafanyakazi wao kupokelea mishahara yao benki.

Mhe. Spika, wizara hizo ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, ni miongoni mwa taasisi zilizokwisha anza mchakato huu.

Mhe. Spika, serikali inaendelea kuwahamasisha wafanyakazi umuhimu wa kupokelea mishahara yao benki. Pamoja na utaratibu huu mabenki pia

yamekuwa yakitoa fursa ya kutoa mikopo kwa wafanyakazi, hivyo wengi wamekuwa wakizitumia huduma za benki zilizopo kuchukulia mishahara yao kupitia mabenki hayo.

Mhe. Spika, Wizara ya Fedha na Uchumi haina taarifa kuwa wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa Vikosi vya Ulinzi na Usalama kuwekewa BIMA. Kwa hivyo, wizara haijakuwa na mpango wa kulisimamia suala hili, ahsante.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo. Mhe. Waziri amekiri kwamba hivi sasa Tanzania Bara wala Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar haina utaratibu wa kuwawekea BIMA wafanyakazi.

Mhe. Spika, wafanyakazi wengi hivi sasa wanapata ajali makazini, wengine wanakuwa vilema na wengine wanakufa kabisa. Je, hawa wanapata msaada wowote wa serikali kama hawakuwekewa BIMA?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, taasisi mbali mbali za serikali hasa mfano upande wa vikosi wao wana utaratibu wao maalum ambao wale watu wanaopata ajali kazini kuna utaratibu wa kuwahudumia na kuwalipa. Kwanza kuwasaidia matibabu, halafu na hapo baadae katika maisha yao.

Kwa mfano, hata sisi hapa kwetu wale watu ambao wanaanguka kwenye mikarafuu, pia tunawasaidia kwa kupitia idara ile ya ustawi wa jamii, halafu tunafanya tathmini kisha tunawalipa.

Lakini Mhe. Spika, suala la BIMA wafanyakazi wenyewe nafikiri wanayo nafasi yao ya kukata BIMA ya maisha ambayo ina-*cover* kwenye ajali na matokeo mengine, nijibu hivyo tu Mhe. Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa hivi sasa wizara zinazochukua mishahara yao benki ni chache tu na kuna mpango wa wizara zote kuchukua mishahara yao benki. Hivi sasa ikifika siku ya kuchukua mishahara Chake Chake Benki ya Watu wa Zanzibar kunakuwa hapapitiki na watu wanapata usumbufu kwa mchana mzima, wanakuwa watu hawafanyi kazi zao nyengine.

Je, wizara yako ina mpango wa kuongeza mabenki ili kuwapunguzia watu usumbufu au watabakia kuchukua Benki hiyo hiyo ya Watu wa Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Subeit Khamis kwamba ni kweli taasisi ambazo zimeanza mkakati huu ni chache ukilinganisha na zile ambazo hazijafanya. Tumeandaa utaratibu serikalini hivi sasa ili tuone wafanyakazi wote wanachukua mishahara yao serikalini.

Lakini kabla utaratibu haujakamilika ni lazima tujitayarishe vizuri, ili kuepuka hili alilo

Mussa2
Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: (anaendelea) pale kuweka msongomano Chakechake na hata kwenye matawi yetu ya *PBZ*. Kwa hivyo, tunaandaa utaratibu kuona kwamba vipi uwezo wetu katika matawi yetu ya *PBZ* hata kutanua wigo.

Mhe. Spika, tuliwahi kuzungumza kwamba *PBZ* wanao mpango labda wa kufungua *mobile van*. Kwa mfano, wanatoka na *van* zao zile wanajua leo mshahara unakwenda Kusini Pemba na watu wote wanakuwa pamoja. Sasa wakati tunajiandaa na wao *PBZ* pia tunawawezesha kuhudumia hiyo shughuli baada ya kumudu na wao wawe tayari, yaani isiwe sisi tayari wao bado. Nakubaliana na Mhe. Mjumbe, lakini nadhani tujiandaa vizuri kwenye benki yetu na wala tusitokea benki nyengine kwa ajili ya kuipa faida.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu aliyojibu Mhe. Waziri ya kuwa na utaratibu wa kutafuta eneo jengine la kuweka Benki yetu ya Zanzibar kwenye eneo lenye nafasi ya kwa ajili ya kuondoa msongamano.

Je, katika kutafuta nafasi au jengo jengine ili kuondoa msongamano, ameangalia sehemu ya kuweka *VIP*, kwa ajili ya waheshimiwa na wananchi wengine wasibanane wakati wa kupata huduma za benki hizi?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Mjumbe pamoja na watu wetu wa benki. Kwa kweli watu wetu wa benki ukifika tu, yaani wakeshaona ni Mhe. Mjumbe kama vile Mhe. Ali

Denge Makame wanakupokea tena moja kwa moja wanakupeleka kwenye Chumba cha *VIP* na mwenye kukushughulikia ni Meneja mwenyewe wa tawi.

Mhe. Spika, hilo sio siri na kama hajafanyiwa huduma hiyo, basi mimi mwenyewe nitamchukua tukiondoka hapa kwa ajili ya kumu-*introduce*. Kwa hivyo, najua hivi sasa harakati tunazo nyingi Waheshimiwa Wajumbe, basi nitajitahidi na nitawapa *hot numbers* ya Maneja wa Matawi yale, yaani wakifika tu wapige najua kwa ajili ya kusaidiwa kwa muda mfupi tu na kwenda kufanya shughuli zao *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kuna maswali ya nyongeza mengine yanaulizwa bila ya mpango.

Nam. 74

Mbonyeo wa Gati ya Mkoani – Pemba

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Mawasiliano SMZ kwa zaidi ya miaka mitano, imeshindwa kurekebisha tatizo la mbonyeo wa Gati ya Mkoani.

Ufumbuzi wa tatizo hilo utapatikana lini?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria kikao cha Baraza kwa ajili ya kutekeleza majukumu tuliyopangiwa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 kama ifuatavyo:-

Wizara yangu haijashindwa kuifanyia matengenezo Gati ya Mkoani eneo lililodidimia. Lakini wizara yangu kupitia Shirika la Bandari katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita, imekuwa ikifuatilia kwa karibu hali ya mbonyeo katika Gati ya Mkoani kama ilivyoshauriwa na wataalamu mbali mbali wa ndani na wa nje ya nchi.

Uchunguzi uliofanywa kwa kipindi hicho chote umebaini kuwa hivi sasa kasi ya udidimiaji imepungua. Baada ya kuonekana mbonyeo huo kupungua,

ambapo mbonyeo sehemu ya katikati umefikia 17cm, baada ya kubaini kuwa udidimiaji huo umekwisha kabisa.

Wizara yangu sasa imeliruhusu rasmi shirika kuchukua hatua ya kulifanyia matengenezo eneo hilo. Mradi wa matengenezo ya Gati ya Mkoani sehemu iliyodidimia umo katika Bajeti ya Miradi ya Shirika la Bandari ya mwaka 2010, utekelezaji wa mradi huo unategemewa kuanza mwishoni mwa mwaka huu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Baadhi ya wataalamu na wananchi wa Zanzibar wanasema kwamba tatizo la mbonyeo wa Gati ya Mkoani ni kuwa mjenzi pamoja na SMZ walidhararu taarifa na tafiti za kimazingira, tatizo kama lile litaikumba Gati ya Malindi baada ya muda mfupi miaka ijayo.

(a) Je, serikali kwa utafiti huu wa wananchi na wataalamu inasemaje?

(b) Taratibu ya ujenzi ni kwamba mjenzi anapoharibu kazi hupaswa kulipia fidia au kupelekwa mahakamani, kwa Gati ya Mkoani nani mwenye kuwajibika, yaani mjenzi au serikali?

(c) Kama kuna mpango wa marekebisho na bajeti hii imezingatia Gati hii ya Mkoani, gharama hizo ni kiasi gani na nani atahusika SMZ au mfadhili?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza nataka kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba wizara yangu pamoja na Shirika la Bandari haijadharau ushauri wowote wa kimazingira ambao umetolewa.

Kuhusu nani atalipa fidia kutokana na ujenzi huo. Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika jibu mama kuwa wizara yangu tayari imeshatoa ruhusa kwa Shirika la Bandari, hivyo shirika tayari limeshajipanga kuona kwamba litafanya hiyo kazi kama nilivyoeleza kwenye maelezo ya awali *(Makofi)*.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri.

(a) Hivi ni mwezi gani uliofikiwa mwisho wa uchunguzi wa kuangalia bandari inadidimia kiasi gani. Sasa ikiwa mwezi huo ni wa mbali

kwa nini imekaa mpaka leo ndio serikali ikataka litatuliwe hilo tatizo?

(b) Kwa kuwa pale kulikuwa na utaratibu wa kuyatoa maji yake kwa kutoboa tundu kila yanapoingia. Lakini utaratibu ule uliachwa kwa muda mrefu na matokeo yake maji mengi sana yakatuwama pale bandari ambayo yanawakera sana wanaosafiri. Hivi wizara haioni kuwa imeshindwa kuyatoa yale maji?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi nilisema kwamba katika kipindi cha miaka mitano wizara yangu ilikuwa ikifanya utafiti pamoja na kushirikiana na tasisi nyengine, ili kuona hali hiyo iko vipi. Lakini mwezi wa mwisho ni hivi juzi, yaani mwezi wa Mei hali ile haiendelee tena.

Kuhusu suala la kutotoboa tundu pamoja na mambo mengine. Mhe. Spika, nafikiri masuala haya yote kama nilivyojibu kwenye swali la Mhe. Hija Hassan Hija ni kwamba tayari tumeshajipanga isipokuwa kilichobakia hivi sasa tunangojea wakati ufike kwa ajili ya kufanyakazi iliyokusudiwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, miaka miwili au mitatu iliyopita nilimuuliza Mhe. Waziri katika kikao kama hiki, kwamba wananchi wanalipa shilingi 500 kwa kila msafiri.

Je, Shirika la Bandari kwa sababu boti zinakuja kwa wakati maalum na sio wakati wote zipo, shirika limeshindwa hapa kupata *pump* kwa ajili ya kuyatoa yale maji?

Kwa hivyo, msimamo wa wizara ni nini katika kipindi hiki mpaka kufikia ujenzi, kwa sababu maji yaliopo ni mengi na magari yanaingia ndani na inakuwa ni tabu hata kwa wale wasafiri kuteremka kwenye yale magari na kuingia kwenye boti?

Mhe. Spika, hata kama watakwenda kwa miguu inabidi watambae kando kando ya bahari. Je, wizara ina mpango gani wa kuyatoa yale maji katika kipindi hiki mpaka hapo watakapoanza ujenzi wao?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza, Mhe.Rashid Seif alitaka kujua wananchi wanatoa shilingi 500/- fedha hizo haziendi kwenye Mfuko wa Bandari na zinakwenda serikalini.

Vile vile alisema kuna utaratibu gani wa kuweza kuyatoa yale maji. Mhe. Spika, suala hili tunalifanyia kazi.

Mhe. Spika, naomba arudie kidogo *point* yake ya mwisho.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, *point* ya mwisho kwa sababu amekiri yapo matayarisho ya ujenzi wa hiyo sehemu. Lakini katika kipindi hiki mpaka kufikia wakati wa ujenzi maji yaliopo ni mengi. Je, wizara pamoja na Shirika la Bandari ina utaratibu gani wa kuyatoa kila baada ya kipindi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, nilisema kwamba suala hilo tutalifanyia kazi. Lakini pia alisema ni kipindi gani, nilisema ni mwisho wa mwaka wa fedha wa Bandari, ni tofauti wa serikali, kwa sababu serikali tunaanzia Julai na wao wanaanza Januari, kwa hivyo mwisho wa mwaka hautakuwa sawa na huu wa serikali.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ili tupate wachangiaji wengi zaidi, basi tuende kwa utaratibu tuliokubaliana wa dakika 15.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi asubuhi ya leo, nikiwa mchangiaji wa mwanzo kutoa yangu machache katika wizara hii ambayo ni muhimu sana katika nchi yetu, inayoongozwa na mtu muhimu sana miongoni mwa mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar *(Makofi)*.

Mhe. Spika, naomba kabla sijaendelea nimtakie heri katika yale ambayo ameyakusudia *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atampa *(Makofi)*.

Baada ya hayo naomba niseme kwamba wizara hii ni muhimu sana katika mustakbali wa nchi yetu pamoja na watoto wetu. Katika ujio unaoitwa *East Africa Common Market*, masuala ya ajira na kazi yanahitajia umahiri wa wizara hii na namna serikali ambavyo imejiimarisha kuisaidia kwa ajili ya kutekeleza malengo yake.

Mhe. Spika, naomba kuishauri serikali kwamba ibadilishe sera, ili ione kwamba Zanzibar suala la kulipa umuhimu ni elimu, kwa lengo la kuweza kuuza katika nchi hizi za Afrika ya Mashariki na Kati. Kwa kweli tukiwekeza vizuri katika *quality education*, naamini na sisi tutakuwa na mchango mkubwa wa kuisaidia jamii yetu.

Kwa mfano, wenzetu wa Singapore tunaelezwa kwamba ilikuwa ni miongoni mwa nchi duni katika nchi zile za mashariki ya mbali. Lakini wakabadilisha sera na kuamua kuwekeza kwenye *quality education.* Hivyo imewasaidia sana na wala si kwa uchumi wa nchi yao tu na hata ku-*export* wataalamu katika nchi za jirani. Kwa hivyo, na sisi Zanzibar tunayo nafasi hiyo.

Mhe. Spika, tukiangalia tabia ya Wazanzibari, uaminifu wao tukilinganisha na majirani zetu. Serikali ikimsaidia Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa makusudi kabisa kuwekeza katika elimu na zaidi elimu ya kiwango cha juu, basi naanimi kwamba nchi zote hizi za karibu na sisi tunaweza kuwa na mchango mkubwa.

Kwa mfano, hivi sasa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali amejitahidi katika masuala ya elimu ya walimu. Kwa kweli tayari bara wanajaribu kututegemea sana katika ngazi hii. Sasa kama tungelifanya kwenye maeneo mengine, basi naamini tungepiga hatua kubwa.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali pamoja na mambo mengine bajeti ya Wizara ya Elimu haipaswi kuekewa *ceiling* ngumu, inatakiwa ile *ceiling* ambayo iko *flexible* kidogo, vyenginevyo kuweka *ceiling* ngumu katika Wizara ya Elimu bado tutakuwa na hali ngumu sana *(Makofi).*

Mhe. Spika, jambo jengine nimeona *organization chart* ya Mhe. Waziri na nimeipenda sana. Kwa kweli nimevutiwa na eneo moja ambalo ni muhimu kwamba Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (*Internal Audit*) kimewekwa chini ya uangalizi wa Katibu Mkuu na huu ndio utaratibu ambao ni muhimu sana.

Pamoja na hayo, huwezi kuchukua Kitengo cha Ukaguzi na kukiweka chini kwa watendaji wadogo wadogo kwa kweli hakitaweza kuishauri *management* ya wizara inavyopaswa. Utaratibu huu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nadhani unapaswa kuigwa na mawizara mengine *(Makofi).*

Eneo jengine ambalo nataka nishauri ni kuhusu uajiri wa walimu wenye ngazi ya *diploma*. Mhe. Spika, wapo walimu waliomaliza ngazi ya *diploma* ambao wamemaliza karibu mwaka na zaidi. Kwa hivyo, nashauri sana serikali imuwezeshe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kuwaajiri hawa.

Kwa mfano, kuna maeneo kama vile Micheweni wanahitajika sana, kwa sababu Skuli ya Micheweni inaukosefu wa walimu. Kama tukiwa na vijana wa *diploma* ambao wamemaliza na Mhe. Waziri hajapewa uwezo na serikali wa kuajiri ni tatizo kidogo.

Kwa hiyo, naiomba serikali kuna baadhi ya mambo yana umuhimu sana. Kwa maana hiyo, aongeze jitihada kuona kwamba hili ni tatizo ambalo linapaswa kufanyiwa utaratibu wa haraka sana, kwa sababu walimu wamemaliza pale Wilaya ya Micheweni na kwenye wilaya hiyo kuna tatizo la walimu. Kama Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali angesaidiwa kuwaajiri hawa basi ingesaidia sana.

Mhe. Spika, hapo hapo Micheweni naomba nizungumze suala ambalo juzi Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni alilizungumza wakati alipokuwa akizungumzia bajeti ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Kuhusu *transformer* ya Chuo cha Kiislamu Micheweni. Kwa kweli pale Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali amefanya utaratibu kwamba sasa kuna mafunzo ya diploma ambayo yanatolewa pale, *Form VI* na hata *Form IV*.

Transformer ile imeungua karibu miezi sita na wale watoto hawapati nafasi ya kujisomea usiku na wao wanafanya mitihani. Kwa hivyo, hili si la Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali moja kwa moja, lakini angemshauri Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi amkabe kuona kwamba ile *transformer* unafanywa utaratibu wa haraka. Vyenginevyo kesho kutwa watoto wanafanya mtihani, *performance* yao katika mtihani na hili isiwe sababu ya kuwaathiri katika mtihani.

Nadhani usiku vijana wanahitajika wasome, sasa kama umeme hakuna, lakini *Alhamdulillah* serikali imewezesha sasa Pemba upo umeme wa kudumu. Kwa hivyo, namuomba kwa yeyote yule mwenye kuweza kusaidia. Lakini waziri mwenyewe ajitahidi kumkaba Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, ili kuona kwamba ile *transformer* imewekwa haraka kwa ajili ya wale watahiniwa kesho kutwa waone wanapata nafasi ya kujisomea.

Mhe. Spika, eneo jengine kidogo nizungumzie kuhusu jimboni. Mwaka jana nilimuomba Mhe. Waziri kwamba madarasa yangu ya Kizimbani yanavuja. Ile skuli tuliirithi kutoka kwa *Missionaries* miaka mingi na skuli imekuwa mbovu kidogo na aliniambia kuwa atajitahidi najua kama mambo ni mengi.

Kwa hivyo, naomba kwa sababu kuna madarasa kama watano au sita yanavuja, yaani ile bati ya *asbestos* imeshaanza kuzeeka. Kwa maana hiyo, ningeomba kidogo akate pua aunge wajihi anisaidie kidogo.

Jambo jengine ambalo nataka kulifahamu na linalichanganya kwenye bajeti ya mwaka huu. Kwa kweli kuna suala la kurudia rudia kuhusu *component* ya wajasiriamali. Mara ya kwanza niliona kuna fungu kubwa kutoka Wizara ya Fedha ambalo limeekezwa kwa wajasiriamali, halafu nikaona kwenye Afisi ya Waziri Kiongozi kuna *component* nyengine ya fedha ambayo imepelekwa kwa

wajasiriamali na hapa kwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mfunzo ya Amali kwenye ukurasa wa 15 wa kitabu hiki kuna neno ambalo naomba kunukuu Mhe. Spika.

> Ukurasa wa 15 *paragraph* ya 39 kifungu cha (iv) kinasema hivi:-
>
> > "Jumla ya shilingi 946,000,000/- zimetumika kwa kuzikopesha Asasi tatu za Kifedha na Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa 23. Jumla ya wajasiriamali 2,875 wakiwemo wanawake 1,841 ambao wamefaidika na mikopo hiyo".

Mimi naanza kupata mashaka na mtazamo wa serikali wa jumla kuhusiana na suala la wajasiriamali, inaonekana serikali haina *formula* moja. Kwa hivyo, ninashauri kwamba masuala ya wajasiriamali yangekuwa *centralized* na isiwe hivi ilivyo, labda sijaifahamu vizuri, lakini naona inanipa matatizo.

Hivyo nataka nipate ufafanuzi kwa Mhe. Waziri wa Elimu au Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha anaweza kutoa ufafanuzi wa jumla kuhusiana na suala zima la wajasiriamali, linashughulikiwa vipi katika serikali, isijekuwa na kesho Waziri wa Kilimo akataja wajasiriamali, nadhani kuna haja ya kulipatia ufafanuzi kidogo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo naomba nimshauri Mhe. Waziri ni kuhusu wanafunzi wa kike na Masomo ya Sayansi. Kwa hivyo, nashauri jambo hili lipewe kipaumbele sana, kwa sababu watoto wengi siku hizi hawapendi kusoma sayansi.

Kwa mfano, ikitokea baada ya mtihani kuna watoto wa kike ambao wamefaulu masomo ya sayansi. Hivyo ninamshauri Mhe. Waziri awe na kitengo au mtu maalum wa kuangalia matokeo ya mwaka ule, yaani aangalie wanafuzi wakike wepi wanao uwezo wa kuendelezwa kusoma masomo ya sayansi. Basi hao wapewe kipaumbele badala ya wanafunzi wenyewe kuhangaika huku na kule kwa ajili ya kutafuta fursa ya kusoma sayansi.

Mhe. Spika, wakati mwengine watoto wenyewe huwa wanahitaji kusoma sayansi. Lakini wakaona sijui waanzie wapi, sasa ile waanzie wapi ni tatizo kidogo. Kwa hivyo, ninashauri sana Mhe. Waziri aone kwamba kuna umuhimu wa kila baada ya mtihani kuna jambo ambalo wanalifanya.

Vile vile naomba kidogo nizungumzie kuhusu Chuo Kikuu (*SUZA)* juu ya suala la maabara. Mhe. Spika, sisi Kamati yetu ya *PAC* tumekuwa tukitembea sana katika mawizara na kwa kweli tumeridhika na udhibiti wa fedha ndani ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa kweli utaratibu wao ni mzuri sana

na sijui kwa sababu Katibu Mkuu ni mwanamke kama ni *Accounting Officer* na Mhasibu pia ni mwanamke.

Lakini kumekuwa na utaratibu mzuri wa udhibiti wa fedha wa ndani, yaani *Internal Accounting System* ya fedha imekuwa nzuri na wamejipanga vizuri na Kitengo cha *Internal Audit* wanafanyakazi vizuri kwa kushirikiana, na hili nataka niwapongeze sana.
Mhe. Spika, tumekuwa na tatizo la kilio cha Maabara ya *SUZA*. Suala hili tungeomba Mhe. Waziri alipe kipaumbele na zaidi mimi binafsi ningependa kujua katika bajeti hii ambayo tunayoijadili Mhe. Waziri hili amejaribu kulishughulikia vipi. Kwa kuwa sipendi mwakani tukijaaliwa mwaka liwe ni jambo lenye kijirudia. Kwa maana hiyo, naomba kwamba kwenye bajeti ya mwaka huu nione Mhe. Waziri katika hili amejipanga kibajeti kulishughulikia hili.

Suala jengine Mhe. Spika ambalo nataka nizungumze labda nipongeze utaratibu ambao Mhe. Waziri ameupanga baada ya kumshauri mwaka juzi au jana wa kufanya bajeti *allocation* kwa idara zake za Unguja na Pemba. Kwa kweli utaratibu huu zamani haukuwepo, lakini sasa naona ameuanzisha na hili ni jambo zuri.

Lakini katika jambo hili nina masikitiko kidogo, kwa sababu najua Mhe. Waziri mwaka huu amekuwa na shughuli nyingi sana na wale wanaomsaidia nadhani katika hili hawakumsaidia vizuri.

Kwanza kwenye *sub-votes* zote za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kifungu cha mishahara kiko zero, yaani hakuna kitu, nilishituka ninaona sijui Mhe. Waziri mara hii hataki kutoa mishahara au vipi tukiangalia kwenye kitabu kikubwa.

Kwa kweli vifungu vyote vya *sub-votes* ambavyo viko kwenye *specific department* sasa vifungu vya mishahara viko zero. Hivi wafanyakazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali mara hii wamekusudia kujitolea au vipi, kwa hivyo katika hili naomba ufafanuzi, ili kujua tatizo.

Mhe. Spika, nimeona kwenye Idara ya Utumishi, lakini nataka kufahamu zimehamishiwa kule au kuna utaratibu gani. Lakini utaratibu wetu wa kawaida kila *sub-votes* inachukua malipo ya mishahara na marupurupu mengine, sasa mara hii ziko zero zero.

Vile vile kuna idara nyengine zina mafungu mazuri katika idara za Pemba, kwenye ile *proportional budget allocation* baina ya Kisiwa cha Unguja na Pemba. K

wa kweli zimenifurahisha sana. Kwa mfano, Idara ya Mipango inayo asilimia nzuri, Idara ya Utumishi, Idara ya Elimu, Idara ya Elimu ya Watu Wazima, Idara ya Mafunzo ya Ualimu.

Lakini nimeshtushwa na baadhi ya idara ambazo nitazitaja na pengine Mhe. Waziri anaweza kunipa maelezo. Kwanza ni Idara ya Elimu ya Juu Unguja kuna 7.8 bilioni na Idara ya Elimu ya Juu Pemba ni 4.2 milioni, yaani 0.05 *percentage* na hii ni *very low allocation* na sijui ni kwa sababu gani.

Kwa maana hiyo, idara inahitaji kuimarisha Taasisi ya Elimu ya Juu Pemba, lakini Mhe. Waziri anaweza kuniambia vyengine. Mhe. Spika, 7.8 bilioni kwa Idara ya Elimu ya Juu kwa Unguja na 4.2 milioni kwa Pemba, kwa kweli ukifanya mahesabu ni sawa na 0.05 *percentage*.

Idara nyengine ambayo inafuatia kwa *share* ndogo ni Idara ya Nyaraka Unguja kuna 106.8 milioni na Pemba kuna 8.6 milioni. Kwa hivyo, nimeshtuka kama asilimia 8 na Pemba kuna mambo mengi ya nyaraka ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi. Lakini kwa *share* hii ndogo afisi ambaye yupo kule atakuwa hana kazi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, eneo jengine ni kuhusu Idara ya Mitaala kuna 1.07 bilioni kwa Unguja, lakini Pemba kuna 145 milioni na hii ni 13.5 ambapo bajeti haitoshi. Mwisho ni Idara ya Ukaguzi Unguja kuna 43 milioni na Pemba kuna 12 milioni tukitegemea kwamba shughuli za ukaguzi zinahitaji kufanywa.

Sasa idara hizi nne naomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atakapokuja kufanya majumuisho anipe ufafanuzi kidogo kuhusiana na masuala haya. Hata hivyo, kwenye Idara ya Elimu ya Sekondari kuna 120 milioni kwa Unguja, lakini Pemba 15 milioni nayo pia ni asilimia 13.

Mhe. Spika, kwa ujumla utendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambacho Mhe. Waziri amekuwa kwa kweli ni ya kujivunia sana, kwa sababu tumepata mafanikio makubwa na kila eneo ambalo nchi yetu ipo, basi kuna *effect* za wizara ya elimu. Hata Uvinje ambako Mhe. Waziri juzi alifanya ziara na kupokewa vizuri sana na wananchi wa Uvinje pamoja na kumuombea dua sana na kule

ukiombewa dua na wananchi wa kule anajua Mhe. Hijja Hassan Hija na Mhe. Ame Mati Wadi mambo yake yanakuwa sio mabaya, kwa hivyo nampongeza na namshukuru kwa jitihada zake kubwa ambazo amezifanya, ni kweli hazijakamilika vizuri lakini amejitahidi sana.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando kwa jitihada ambayo Mhe. Waziri amefanya naomba niunge mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwanza niwashukuru na kuwapongeza sana Waziri pamoja na watendaji wa Wizara hii kwa juhudi zao kubwa wanazochukua.

Mhe. Spika, nikianza na kifungu cha kumi na tisa ukurasa wa sita nawapongeza kwa dhati Waziri na walimu katika juhudi zao kubwa wanazozichukua kunako mwaka 2000 kwa kufaulisha wanafunzi 2,806 hadi kufikia mwaka 2009 kufikia wanafunzi 8,725 kwa kiwango hiki tuzidishe mikakati. Nawapongeza sana sijui walichukua bidii gani hadi kufikia wanafunzi 8,725 kwa kipindi cha mwaka 2009, kwa hivyo kama walifanya mikakati maalumu wanayoitambua wenyewe ningewaomba hapa wazidishe zaidi ili tupate kufautu kuwafanikisha wanafanzi wetu zaidi.

Vile vile nawapongeza wanafunzi waliopata daraja la kwanza *Division one* kutoka kumi na nane Mwaka 2000 hadi kufikia arubaini mwaka 2009 hapa nawapongeza sana, kweli kama tutakusudia tunaweza leo hii vijana wetu kufikia *Division one* kwa kufika arubaini ni kiwango kizuri na kinaridhisha, kwa hivyo na hapa ni pahali pa kuangaliwa zaidi kwa hivyo hata kufika kidatu cha sita wakafaulu kama hivi inaleta matumaini hata kwa serikali, itakuwa imeshakuwa na watoto wenye ufahamu mzuri wa kutekeleza mambo yao na mambo ya serikali.

Kwa hivyo ningeiomba sana Wizara ikajitahidi sana na kuangalia watoto waliofikia kiwango kama hiki kuwasaidia pale palipokuwa panahitajika kupatiwa mkopo wa kuendeleza elimu yao wakasaidiwa zaidi, kama inavyoeleweka baadhi ya wananchi wetu hapa Unguja na Pemba wengi huwa wanashindwa kuendeleza watoto kulingana na kiwango cha uwezo wa fedha. Kwa hivyo kama kuna misaada ya mikopo wangeangaliwa zaidi vijana wetu hawa ili wakapata kujiendeleza na masomo ya serikali.

Mhe. Spika, nije katika suala la meza za skuli baadhi ya maskuli yetu sasa hivi yamekuwa na upungufu wa meza juu ya jitihada kubwa anazojitahidi Waziri kuingiza meza katika maskuli yetu kila siku lakini kumekuwa na uharibifu mkubwa unaofanyika katika meza hizi, kwa makusudi baadhi ya wanafunzi wanashirikiana na baadhi ya wachongaji ili kuzivunja meza zile na kuzifanyia mahiji yao mengine wanayohitaji, kwa hivyo suala hili la meza kila siku ukipeleka skulizitakuwa zinavunjwa.

Kwa hivyo mimi ningeiomba Wizara ikachunguza ubunifu mwengine kama inawezekana kutengeneza mesa za aina nyengine kama *plastic* kavu au mabati angalau kuondosha huu upungufu unaotokea sana kuvunjwa meza kiholela, ili kama kuna uwezekano wa kufanya mbinu kama hizo ikafanyika hivyo. Kwa sababu kuweko kwa meza skuli inasaidia sana wanafunzi kupata uzoefu wa kuzitumia meza zile ili watakapopata kuajiriwa wakawa na uzoefu wa kukaa kwenye meza, vyenginevyo ukosefu wa meza ikiwa kila leo wanafunzi wanakaa chini na kupinda miguu yao nafikri tutakujakuwa tunapata makarani waliokuwa wameshapata ulemavu wa miguu yao kufanya matege.Mhe. Spika, ningeomba suala hili la meza likachunguzwa sana baada ya kukaa miaka kumi au miaka minane mwanafunzi chini bila ya kutumia meza, baadae anaweza kupata ulemavu.

Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa sitini na moja kifungu cha mia moja na tisini na tatu kitengo cha ushauri nasaha, nampongeza Mhe. Waziri kwa kutoa mafunzo ya ushauri nasaha kijinsi na ukimwi kwa walimu 150, hapa ni vyema kuanzisha kitengo hicho cha ushauri nasaha kwa sababu kama inavyoeleweka baadhi ya vijana wetu wengi wanafunzi sasa hivi wamekuwa waangaliaji sana wa vyombo vya habari, TV na mitandao mbali mbali kwa hivyo wanaona mambo mbali mbali. Pindipo wakitolewa waalim hawa kutoa nasaha katika maskuli yetu kidogo nafikiri janga hili la ukimwi litapungua na tutajiepusha na matatizo mbali mbali ya wanafunzi wetu.

Kwa hivyo ningeomba Mhe. Waziri hapa akapaangalia sana na kupatilia nguvu ili hao wanaopewa mafunzo haya wakayatoa kwa dhati kwa wanafunzi wetu ili kujiepusha na masuala kama haya.

Nije ukurasa wa 64 kifungu 202 kitengo cha ununuzi na ugavi. Mhe. Spika, naomba kitengo hiki kiniangalie katika ujenzi wake wa skuli zeke kumi na tano za Sekondari za vijijini Unguja na Pemba kwa upande wa banda langu la skuli ya msingi ya Kilimahewa kwa kuwe limeshakuwa na hali mbaya lile moja ambalo limeelekea *East* na *West* banda hili limekuwa hali mbaya sana halifai kusoma tena wanafunzi limekuwa na kuta mbovu ndani ambazo zinatishia maisha kwa kuinama na wakati ardhi yake ya kichanga, kwa hivyo hata wale watoto kuwaambia wakae kwa muda wa miezi mitatu linatisha. Ningeomba wataalam wa ardhi wakenda kuliangalia na wakalitizama kama kuna ukarabati wowote wa kufanyiwa likafanyiwa ukarabati au kuzuiliwa kuta zile zisije kuporomoka na kuathiri wanafunzi wanaosoma katika banda lile.

Kwa hivyo katika mipango yake ya ujenzi wa skuli hizi kumi na tano na mimi akaniangalia katika banda lake hili kwa kunusuru ajali kwa wanafunzi wanaosoma pale, ingawa wazazi wanajitahidi kuchangia michango mbali mbali lakini kama inavyoeleweka baadhi ya wananchi zetu hali zao ngumu za

kimaisha, kwa hivyo suala la kukarabati banda like kwa wao linakuwa gumu. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri akaniangalia hapo katika kukarabati banda lile kabla ya kutokea ajali.

Mhe. Spika, ukurasa wa 64 kifungu 203 katika ujenzi wa skuli mpya tatu za ghorofa za Sekondari katika Mkoa wa Mjini Magharibi nafikiria ni mmoja wapo niliyeahidiwa na Waziri tokea Januari, 2007 ambayo ahadi yake haijatekelezeka, kwa hivyo kidogo naomba kunukuu maagizo ya wanafunzi wananiuliza huyu ndiye aliyechukua fomu ya Urais, ndio yule yule aliyahidi kutujengea gorofa ndani ya maeneo yetu ya Skuli za Kilimahewa ndani ya Jimbo la Amani, kama bado ujenzi basi atupigie angalau *grader* na kusafisha eneo hilo kabla ya Julai, 20 mwaka huu.

Nikawaambia kwa ninavyomtambua Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa suala kama hilo naamini wazi anaweza kulifanya kabla ya Julai, 7 mwaka huu, kwa hivyo wanafunzi hawa wanasema pamoja na wazazi kwa suala hilo la kuchukua fomu wao hawana wasi wasi Mheshimiwa jitayarishe tu utapeta kwa agizo lao.

Mhe. Spika, nikimaliza hapo nije ukurasa wa 60 kifungu 188 kesi za ujauzito na ndoa kwa wanafunzi hili sio zuri waziri, wazazi na walimu walipigie kelele sana hususan wanafunzi wa msingi hadi *Form VI* hapa serikali inakuwa imeshategemea kuwa na wanafunzi wazuri tu ambao wataleta matumaini kwenye serikali hii, lakini kama mwanafunzi ameshakuwa na kitendo hicho cha kuwa ujauzito au mwanamke kuozeshwa mwanamme bado mapema au umri wake mdogo hapa inakuwa inaleta picha mbaya. Kwa wale wanafunzi ambao hawana matatizo haya watachukua kumbu kumbu za wenzao wanaofanya hivyo, kwa hivyo ningeiomba Wizara ikalipigilia kelele suala hili ili lisifanyike na liondoke kabisa kwa mwanafunzi anaposoma kuanzia *Form IV* hadi *Form VI* na madarasa ya kumi waupukane na masuala kama haya.

Mhe. Spika, kama inavoeleweka kuwa elimu ni kitu muhimu sana katika dunia hii kwa hivyo leo kwa kuwa tumeshawategemea wanafunzi hawa kwa kuja kuendesha nchi ukishapotosha maadili yao mapema hii italeta sura si nzuri kwa wanafunzi wetu, kwa hivyo ningemuomba hili Mhe. Waziri alipigie kelele sana pamoja na walimu wenzake ili liepukane na lisifanyike.

Mhe. Waziri ningemuomba ajitahidi sana kutilia mkakati zaidi katika wanafunzi wetu wa vyuo vikuu kwa kuwa sasa hivi tumekuwa na utaratibu mzuri, kwa kuanza na chuo kikuu cha kwanza mpaka sasa hivi tumeshakuwa na vitatu kwa hivyo tumeshakuwa na matumaini mazuri kwa wanafunzi wetu nao kupata kusoma vyuo vikuu hapa hapa nchini, na hata kupata wananchi kutoka nchi mbali mbali kwa kuja kujiunga vyuo vyetu hivi. Kwa hivyo

ningemuomba akaongeza wataalam zaidi kutokana na tuliokuwa nao pia si vyema kupata wataala mkutoka nchi mbali mbali ili kuja kusaidia zaidi kutia nguvu katika usomeshaji wa vyuo vikuu hivi.

Mhe. Spika, mimi Wizara hii naipongeza kwa juhudi zake kubwa inazochukua kwa kila mtu ambae mwenye macho anaona juhudi anazozichukua Mhe. Waziri, juu ya kuwa kila mara anakuweko nje kutafuta misaada mbali mbali ya kufanikisha masuala ya elimu, kwa hivyo tunampongeza kwa juhudi yake kubwa anayofanya ya kutafuta wafadhili kupata kutusaidia maskuli yetu mbali mbali pamoja na wanafunzi kwa hili nampongeza sana. Vile vile nawaomba walimu wanaosomesha skuli mbali mbali wawe wastahamilifu katika maslahi yao yote, kwa ninavyomjua Mhe. Waziri atawasaidia na atawapatia kwa wakati ili wafanikishe kuendeleza masomo yetu kwa wanafunzi wetu.

Mhe. Spika, kwa wizara hii sitokuwa na mengi sana ya kueleza kwa kuwa kazi zake zinaeleweka na zinaonekana juhudi zake Mhe. Waziri, mimi pamoja na wananchi wangu wa jimbo la Amani naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe, Waheshimiwa wangu mara hii wamekuwa na dua na utaratibu wa maombi ambayo nashindwa hata kufanya *assessment* vizuri, Mhe. Haroun Ali Suleiman yuko pamoja na wajumbe kwamba apate, Mhe. Waziri Kiongozi yupo pamoja na wajumbe kwamba apate, Mhe. Ali Juma Shamhuna yuko pamoja na wajumbe hawa ili apate. Yuko mmoja alisema anaomba wote wapate sasa nashindwa kufanya *assessment* yupi aliyekusudiwa apate, lakini hiyo kazi tuwaachie wananchi wenyewe.

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tuliofika hapa tukiwa ni wenye afya njema na kuja kujadili mambo yetu katika nchi yetu, lakini pili nikushukuru wewe na mimi kuniona kutoa mawazo yangu na dua zangu na *ishaalla* Mwenyezi Mungu atujaalie ziwe *Kabul* kwa sababu damu yangu iko katika asili ya masharif, basi yule ambae kuwa nitamuelekeza dua hii *ishaalla* Mwenyezi Mungu amfaulishe mambo yake penye uzito pafanye wepesi na ishaala yale anayoyataka ampe.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Wangu kivuli kwa sababu hotuba ameimaliza na kama sio lazima na mimi kutoa mawazo yangu basi ningesema inatosha nikaunga mkono hoja, lakini kwa sababu ni wajibu kwa kila mmoja kutoa mawazo yake kwa yale ambayo ameyaona basi ni vyema na mimi kutoa mawazo haya.

Lakini la nne na la mwisho ni kwa sababu tunamaliza baraza hili nashukuru Mhe.Spika, umetuendesha vizuri Mungu akujaalie akupe umri mkubwa zaidi, Mungu akupe ya kheri na akupe mafanikio kwa yale ambayo tunayahitaji, lakini sitomsahau kiongozi wangu wa upinzani kwa utaratibu ambao ameuchukua kutulea wana wao na kutuongoza vizuri Mungu ishaala afanye wepesi kila penye uzito, mungu awape mahitaji mema na *ishaallah* ikifika siku basi uende peponi amin. Mhe. Spika, mimi hivi sasa bado sijataka nife kwa sababu nilikuwa mgonjwa nikenda hospitali labda ufike wakati.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye bajeti na bahati nzuri kabla sijamaliza muda ambao utanipa na kama utaniongeza basi nitakuja kutaja wengine, lakini nianze na Chuo cha Walimu Mchangamdogo, chuo hiki mwaka 2008 Mhe. Waziri alikizungumza, mwaka 2009 na leo tuko mwaka 2010, ni imani yangu kwa kuwa anataka urais na anataka dua zetu na *ishaallah* Mungu amjaalie hivyo basi atachukua juhudi kwa kasi kabisa muda huu mchache uliobakia ili kufanikisha malengo yake, Mungu amng'arishe kama tulivyosema mwaka 2009. Labda umtie podari kidogo tu ya kifua isionekane lakini weupe wake *ishaallah* Mwenyezi Mungu amjaalie ung'are zaidi.

Sasa sijui chuo hiki tumefikia hatua gani? Sababu muda ndio unamaliza na kila ninapokwenda walimu wananiuliza mbona kile chuo hatujakiona pirika zake, lakini mimi nina imani kama Waziri bado yupo katika utafiti wa utendaji wake. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri, jinsi ya majibu atakayokuja kunileta Mhe. Waziri katika chuo hiki basi na zile hatua za utendaji zianze kuonekana, wala sio kitu cha ajabu na aibu hata mimi Mwakilishi kunambia lete gari kumi za mawe ili kile chuo kiende haraka basi niko tayari kufanya kazi hiyo, lakini mradi na zile nguvu zake *inshaallah* Mwenyezi Mungu anijaalie nifanikiwe nifanikiwe katika matatizo hayo.

Nikiondoka hapa nije katika ukurasa wa 60 kitengo cha kesi wa ujauzito na ndoa za wanafunzi kwa kweli haya yamekuwa malalamiko sana kwa wazazi na kila mtu ana malengo yake katika kufanikisha lengo la kumlea mtoto, Mhe. Waziri hapa karipoti kwamba ripoti zilizoripotiwa mpaka sasa hivi ni 37 bahati nzuri katika kesi 7 zilikuwa ni za wanafunzi kwa wanafunzi. Lakini pia kaendelea kasema kesi za ujauzito ni kesi 16 kati ya hizo, 3 ni wanafunzi kwa wanafunzi, kuna za ndoa mbali na kuna za ujauzito mbali, za ndoa wanafunzi 7 ndio walioowana kwa kupendana. Lakini za ujauzito ni kesi 16 tatu ni wanafunzi kwa wanafunzi lakini kumi na tatu jee nataka ufafanuzi waliohusika ni nani katika ujauzito huu.

Kumi na tatu hazijajulikana nani ambae kuwa alichochea mambo haya au kama walikuwa ni watu waliokwenda chooni halafu wakaona miujiza vile vile Waziri anaweza kutwambia, hapo nataka ufafanuzi nielewe tatizo hili lilitokea je?

Lakini nikiondoka hapo Mhe. Spika, niende kesi za ardhi katika maskuli hili limekuwa ni tatizo kubwa na sio maskuli tu lakini ardhi imekuwa na matatizo katika sehemu zote za nchi yetu kutokana na ufinyu wake wa ardhi, kutokana na utaratibu ambao kuwa bado tunautumia. Je, ni kesi ngapi za ardhi katika maeneo yetu ambazo tumezipata, ngapi zimepata ufumbuzi na ngapi hazijapata ufumbuzi. Halafu ni maskuli mangapi ambayo kuwa yana hatimiliki ya ardhi na ambayo kuwa maeneo yake yamehifadhiwa na maskuli mangapi ambayo kuwa hayajapata haki miliki za ardhi na maeneo yake hayajahifadhiwa.

Mhe. Spika, cha ajabu skuli ni eneo ambalokuwa liko huru, lakini utakwenda kuikuta nyumba ipo chini ya skuli, kesho kutwa skuli ikibomoka tarati anahifadhi na lile eneo anasema lake, matatizo haya yanatupelekea sasa kukosa amani kwa watoto wanaosoma na ndio zile kesi za ujauzito zitatokea, kwa sababu haiwi nyumba yako iko chini ya skuli mtoto anakunywa maji mwako halafu ukamtizama tu jamani kuna kazi , na ndio haya matatizo yakawa yanatokea kila wakati. Maskuli hayana hifadhi na yamekosa yale maeneo yake kupata utaratibu ulio bora.

Sasa nafikiri Mhe. Waziri akija atanambia ni maskuli mangapi yamepata hatimiliki na mangapi ambayo yameshahifadhiwa ili kulinda mazingira ya skuli yashiharibike, halafu katika hili bajeti ya mwaka 2009 tulitoa ushauri wetu kwa kuwa maeneo ni madogo basi tungeanzisha ghorofa moja moja au mbili ili kukidhi maeneo yetu kupata kusogea tena mbele kwa mazingira mengineyo. Wenzangu kamati ya PAC wanasema walivyorudi safari zao waliyakuta majengo mengi mpaka wale wanyonge wa Mungu kama utaratibu wa Mhe. Abeid Karume wa mwanzo alivyofanya kujenga majengo ya ghorofa, ili kuondoa rasimu ya ardhi kutumika sana. Sasa na sisi katika maskuli yetu tungeanza na utaratibu huu japokuwa nguvu yetu ni ndogo, lakini utaratibu wa kujenga mejengo maeneo haya.

Mhe. Spika, mimi nataka nisipoteze muda wako niende katika mambo ya hifadhi ya nyaraka na makumbusho tulisema ni muhimu sana na haya ndio makumbusho yetu ya vizazi vinavyokuja baadae kupata kujua kilichotendeka na ambacho kuwa watakitenda wao, kama hakuna hayo basi ni kazi kubwa kwa sababu sasa hivi dunia imekua mambo mengi tunasema ni ya Kompyuta lakini hii ni mashine na mfano ulitokea karibuni miezi miwili hatuna umeme kompyuta zilikuwa hazifanyi kazi, lakini kama kuna kumbu kumbu za karatasi zilizoandikwa zikahifadhiwa vizuri basi watu watatumia vigezo vile na baadae matatizo yaliyokuwepo yataondoka kwa kupata utaratibu uliokuwepo.

Kwa hivyo ningeomba majengo haya yanayohifadhiwa nyaraka sio kukarabatiwa lakini kujengwa upya na kutengenezwa vizuri ili kumbu kumbu zetu zisipotee kwa vizazi vyetu vijavyo vikapata kujua, lakini kwa vyenginevyo

majengo haya yanayoondoshwa nyaraka kwa nilivyokwenda kuyaona mimi mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii hayaridhishi. Kwa sababu Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ana kazi kubwa katika Wizara yake kila unapogusa ndipo, kila unapopaona aa! ukweli ni jambo la kuangaliwa Wizara hii hata bajeti ya dharura basi kuingiziwa si makosa. Lakini vyenginevyo atakuja kushindwa kufanya kazi zake na hatima yake kumbu kumbu zote tutakuwa hatunazo.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende katika ujenzi wa vyuo vya *Qur-ani*, wananchi wanajitahidi na ni vyema serikali kwa sababu hili wameliona muda mrefu wanalipigia kelele kulifuatilia na kulisadia, naomba Mhe. Waziri na kwa sababu anaelekea katika nyota nyengine anaondoka nyota ya tatu anaingia nyota ya kumi tukijaaliwa basi ajitahidi kipindi hiki vyuo vya *Qur-ani* viangaliwe san asana, tena kuwe na mfuko maalum. Sio kwamba kila jimbo aa lakini angalu kwa kila Wilaya tujue ni vyuo vingapi ambavyo viko katika bajeti na vitashughulikiwa.

Kwa sababu adhma ya serikali inasema anzeni wananchi serikali itakuja kuongeza nguvu basi nataka nimwambie Mhe. Waziri jimboni kwangu tayari wananchi wameshaanza vyuo vya kisasa vyengine vya ghorofa moja na vyengine vya kawaida, lakini hawajamaliza shughuli zao ningemuomba Mhe. Waziri kupitia kwako angalau akishamaliza bajeti yake aniambie Mhe. Omar Ali Jadi ni vyuo vipi vilivyojengwa kwa matofali vya ghorofa na vile vya kawaida ni vipi angalau serikali ikaone ili ijitutumue kuwasaidia. Mimi niko tayari siku hiyo nafikiri nitamlisha uwele na pweza ili kuja kuona mazingira ya watu wa jimbo langu kama Kijiji changu cha Kojani kilivyo kuwasaidia vyuo vile vya Qurani ili na wao kujiona katika nchi yao kama kweli wana manufaa.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naona unaniangalia sana sasa kwa kumalizia niende elimu ya watu wazima serikali imetangaza katika dira yake ya maendeleo ya 2020 tunapofikia mwaka 2020 angalau watu wote wawe wanajua kusoma na kuandika, lakini utaratibu huu katika miaka ya nyuma nimeuona vijijini unakwenda lakini sasa hivi haupo tena, sasa ni vyema Mhe. Spika, Mhe. Waziri akaja akanambia au akalieleza Baraza lako ni utaratibu gani uliopelekea mafunzo yale ya wazee katika vijiji yamekufa, sababu hayana fedha au walimu hakuna au ni utaratibu gani uliopelekea kumalizika hivi.

Watu wengi wamejielimisha na wamefahamu sasa kwa sababu mambo yetu ya sasa tunakwenda na ulimwengu wetu wa kileo ni vyema suala hili la elimu ya watu wazima kuchukuliwa mkazo kwa nguvu zote, ili tunapofikia hatua hiyo basi wananchi wote wawe wameshafahamu kusoma na kuandika kwa nchi hii.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kwanza niseme ahsante sana kwa kunipa muda wako na ukakubali kunisikiliza kwa makini na wajumbe wako wakakubali kunisikiliza na wamenifahamu. Kwa hivyo ningemuombea Mhe. Haroun Ali Suleiman yale niliyomueleza ayafanyie kazi na asiwe na wasi wasi walioomba ni wengi. Lakini kwa sababu najali bajeti yake Ishallah Mwenyezi Mungu amfanyie wepesi wajumbe wote wa Neki akifika kule wamuone Mhe. Haroun anafaa kuiyongoza Zanzibar.

Mhe. Spika, ahsante sana. Samahani nimesahau naunga mkono hoja.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru na wewe nakuombe lile ambalo unalitaka lenye kheri na wewe.

Pia namuombea duwa Mhe. Waziri wa Elimu apate lile lanalolitaka lenye kheri na yeye. Na mimi mwenyewe binafsi najiombea dua nipate ninalolitaka lenye kheri na mimi.

Kwanza sina budi kuipongeza Wizara ya Elimu nzima akianzia Waziri, watendaji wake pamoja na walimu wote.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri hii miuhtasari yetu tunavyoitengeneza nakuomba au nakushauri tuifanyie na vitabu, tuviandike na *reference* yake kabisa kama Kadege tuandike 1990 na kuendelea ili kujulikane hasa kama hichi kitabu cha Kiingereza ndio ambacho kinataka kutumika. Baadhi yao ikiandikwa tu Kadege iko ya mwaka 1990, 1992, 1994 wabatumia yeyote inakuwa hakuna mpangilio. Lakini tukiweka pale kwa makusudi mazima kwamba hii inaendana na hii nafikiri tutaondoa suala hili.

Ukurasa wa 11 Miradi ya Shule. Mhe. Waziri miradi ya shule mingi imetekelezeka, umeifanya vizuri kwa ufanisi na unahitaji kupongezwa kwa hilo. Lakini nakuomba na ile skuli yangu ya Magogoni hiyo kasma uliyopata juzi kanifunikie bati pale. Maana nakujua Mhe. Waziri ukikumbushwa mara moja unafanya.

Ukurasa wa 19 mradi wa upanuzi na uendeshaji wa maktaba. Kwa kweli tumepata maktaba yetu nzuri na tumeifungua hivi karibunia. Lakini nakushauri Mhe. Waziri kwa makusudi kama tunavyopita tukaomba haya mengine na hii tuiyombee maktaba yetu iwe na kumbukumbu za kutosha, zinazokwenda na wakati sio magazeti tu halafu tuitangaze kwenye vyombo vya habari kama radio na television kwa vizuri ili wateja wapate kutumia vizuri na watu watuelewe kama tuna maktaba.

Mhe. Spika, nije suala la Michezo. Mhe. Waziri wewe ni mwalimu na mimi ni mwalimu. tunajua kama IQ ya mtoto inakuwa na anakuwa na upeo zaidi wa kufahamu kama atacheza na michezo. Baadhi ya maskuli mengi mjini hayana viwanja vya michezo. Sijui hapa tutafanya vipi ili hawa nao wacheze kama wengine. Nakuomba hili hapa tulifanyie kidogo ufafanuzi kuwaelewesha walimu kama tupange siku maalum ili na watoto wale waende kwenye viwanja wacheze ili na wao IQ zao ziwe *active* kama wale wengine ambao wana viwanja vya michezo.

Mhe. Spika, ukurasa wa 22 mradi wa kumbukumbu za kale na historia, hifadhi za mambo ya kale (makumbusho) namuomba Mhe. Waziri haya makumbusho kwenye kitabu hiki sana imetajwa majengo, lakini kumbukumbu za kale sio majengo tu. Hawa watoto wanakwenda mashamba kuna mapango wanaingia kwa kweli vile wanavyoingia kule inakuwa ni hali mbaya wanaweza kusukumana na wakaumizana. Na yale pia yanatakiwa kuwafanyiwa marekebisho angalau ngazi za kuingikua mle ili wasisukumane. Zile pia ni historia na wanakwenda kwa wingi na wanavutika na yale mambo yaliyokuwepo kule chini ya mapango. Kwa hivyo pale tungefanya utaratibu labda wa ngazi tukawajengea ili wakaweza kufika chini ili wakaweza kuendelea na misafara yao vizuri na kuweza kusoma vizuri.

Kuhusiana na majengo namuomba Mhe. Waziri ayafanyie ukarabati isijekuwa *confusion* na hawa Mji Mkongwe. Kwa sababu Mji Mkongwe mkali sana kwa majengo yake. Hapo utakapofanya marekebisho yabakie kwenye uhalisi wake ule ule, lakini marekebisho yafanywe kama kugonjwa na rangi.

Ikurasa wa 26 na 27, maambukizo ya virusi vya Ukimwi hili ni tatizo gumu sana kwa wanafunzi, tujaribu kuwaelimisha na sio walimu tu hata nyumbani tujitahidi kwa sababu mzazi na yeye awe na muda wa kukaa na mtoto wake amfahamishe, kumwachia mwalimu tu haitoshi. Kwa sababu wimbi kubwa la hawa wanaohujumu wanakimbilia kwa wanafunzi kwasababu hawa wanakuwa hawana hasara, akimuona mtu ana gari akimpakia siku moja au siku mbili anampa na shilingi elfu tano au elfu mbili anampa, tayari anamuachia Ukimwi, analeta janga kwa jamii. Mwanafunzi yule anapotezewa haki zake zote na mambo yake yote yanaharibika. Wazazi tujitahidi kwa makusudi mazima ya kuelimisha hao watoto wetu kuhusu mambo ya Ukimwi. Siku hizi watoto wengi wamekuwa wana tamaa sana kuliko zamani.

Ukurasa wa 30 madrasa na vyuo. Mhe. Waziri kwa kweli tulipe upeo hili suala. Hawa walimu wanaosomesha vyuo vya Qur-ani kwa kweli vingi ni masikini mno. Nafikiri tungelilishuhulikia hili kwa kina wewe pamoja na sisi kwa sababu hii sio kazi yako peke yako hii ni sadakatu jariya, kila mtu akifanya Mwenyezii Mungu atamlipa huko mbele tunakokwenda. Lakini Mhe. Waziri

kama unavyopandisha soksi kuezeka maskuli, kufanya mambo mengine, hetu litupie jicho na hili, Mungu atakupa fungu lako na Mwenyezi Mungu atakurejesha tena na atakupa unachokitaka. Humu ndio ambamo kwenye hizo baraka zenyewe. Kwa hivyo hili nafikiri tulitizame kwa kina, uliingize kwa makusudi hata kama halimo kwenye bajeti lakini ufanye hivyo hivyo. Hiyo miradi ambayo unaiyomba huko na hapa utupie tupie.

Idara ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia ukurasa wa 36. Mhe. Waziri nakwambia tena nakukumbusha. Shule zetu za sekondari zina vitabu vingi vya sayansi, hesabu na vyenginevyo. Tatizo sugu *dictionary* huwezi kusoma kama huna *dictionary*, huwezi kutafuta *formula* wala huifahamu vizuri kama huna *dictionary*, asili ya neno, mzizi wa neno halafu huwezi kutia kwenye *structure* neno lolote kama huna *dictionary.*

Narudia tena kusema lolote huwezikufanya kama huna *dictionary* hebu tujitahidi mara hii tufanye kama mradi wa mpito huu, hao walimu wa Sekondari na wao na wanafunzi pia wawe na *dictionary* mtu anafika kumaliza hajui *how to use dictionary* hajui chochote kuhusu *dictionary*, hatujui chochote kuhusu *dictionary* ukimuuliza *dictionary* anakuuliza nini. Hubu tufanye, tujitahidi mimi najua ukikumbushwa sana unafanya, kwa hivyo na hili tulitupie macho.

Nakuje kwenye *scheme of serves*, nakupongeza na nakushukuru, tumepiga kelele kwa kusema kuweza kuwaombea maana yake hawa ni walimu wenzangu na malalamiko mengi naletewa. Umejitahidi nakushukuru, Lakini kuna wengine hazijakaa vizuri, kwa hivyo zile zilizokuwa hazijakaa vizuri hizi zao kama ulivyonielekeza tuwaombe kwa utaratibu maalum sio wote. Mhe. Waziri kwa imani kabisa wamenambia hili niliseme kwa wale ambao kidogo wana matatizo waorodheshwe majina yao waende pale kwa utaratibu uliokuwa mzuri wakafanyiwe marekebisho yao.

Na hii *teaching allowance* wanavyotaka walimu isichanganywe changanywe wanataka kama zamani iwe peke yake kama iliyokuwa mwanzo. Nafikiri tukiichukua hii tukiiweka kama mwanzo huu mgogoro na hili zogo litakwisha. Hapa nafikiri ndio tutakuwa tumeondosha huu mgogoro au hili tatizo lililokuwepo.

Mhe. Spika, ukurasa wa 23 Elimu Mjumuisho. Kwa kwei tumeletwa hii elimu mjumuisho ni elimu nzuri kwa sababu haijibagui watu wote wanachanganywa kwa pamoja, wanasoma kwa pamoja haijali mtu mlemavu, haijali taahira au mwengine yeyote. Mhe. Waziri hii elimu hao walimu wanataka mafunzo ya hali ya juu kwa sababu wengine waliopelekwa kule ni hawa walimu waliokuwa wanasomesha watu wa kawaida, sasa huu mchanganyiko sio wa watu wa

kawaida. Hii nafikiri tufanye semina za makusudi lazima tuwachukue na hawa kuwafunza kama wale wa mwanzo waliokuwa wanasomesha wale ambao waliokuwa wametengwa sehemu tofauti, sasa hivi labda tuwape elimu na hawa ili waweze kuwaendeleza wote kwa pamoja. Nafikiri Mhe. Waziri hili utalichukua utalifanyia kazi.

Mhe. Spika, la mwisho kuhusu Elimu ya Juu. Elimu hii utaratibu wa mikopo ni mzuri lakini tunakuwa na watu wengi ambao wanahitaji mikopo, sasa wengine wanakuwa wanapata wengine wanakuwa wanakosa mikopo na wanakuwa na sifa za kusoma inabidi wabakie wasubiri. Labda tungeengeza hii idadi yah ii mikopo ili wote wale wanaohitaji wenye sifa au waliopasi vizuri kwa wakati ule wakapata kusoma kwa muda ule kwa sababu ukikaa wakati tayari unayo hamu ya kusoma ukiaa unapoteza muda wa mwaka mzima unasubiri mpaka mwakani kupata mkopo. Nafikiri tungelitizama tena na hili ili tukaongeza zaidi mikopo ili wote wanaotaka kusoma wakapata mikopo na wakasoma vizuri.

Ahsante sana Mhe. Spika, mimi hii ni *field* yangu nimeichangia point nyingi lakini *short and clear* nafikiri watu wamenielewa. Kwa mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni naiyunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Namuombea Mhe. Waziri Mungu amjaalie apate anakitaka kwa salama ili atuongeze kama anavyotuongoza katika Wizara. Ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii kwa kuchangia kwa ufupi sana kuhusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza nianze kwa kutoa shukurani kwa Mhe. Waziri kwa namna tulivyoshirikiana katika kipindi chote kwa kunisaidia kukuza sekta hii ya elimu katika jimbo langu. Tumeanza na Mhe. Waziri skuli zote nilizokuwa nazo kule ni sita na ilikuwa inamalizia darasa la kumi tu basi, lakini hivi sasa tunazo skuli saba na katika hizo tano ni mpaka darasa la kumi na mbili (12). Ni maendeleo kwa jimbo langu na najifaharisha nayo na yote haya yasingekuwa isipokuwa ni mashirikiano mazuri baina yangu na Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, pia nashukuru kwa kunisaidia kupata misaada mbali mbali ya kuendeleza majengo yangu katika skuli, kiasi ambacho hivi sasa tuna majengo mengi kwa juhudi yake yanasubiri kutiwa bati tu.

Kwa upande wa dini ametusaidia pamoja na wanzangu kupata misahafu mengi na tumeyaeneza katika vyuo chungumzima.

Shukurani ya mwisho kwa Mhe. Waziri ni namna alivyoleta dibaji yake na kuhubiri serikali ya ummoja wa kitaifa na kuiyombea dua kwa wananchi wote kuwa watumie demokrasia yao ili waone kuwa baada ya uchaguzi mkuu

tunakuwa na serikali hiyo ya ummoja wa kitaifa ikimaanisha kuwa watumie kura zao kutia kule ambako ni **Ndio** na hili ndio lengo langu.

Mhe. Spika, kitabu kimeandikika na nilikuwa naangalia malengo ya mwaka 2010/2011 nimeona yamekamilika. Sikupenda kuchangia sana kuhusu kitabu lakini badala yake ni kutoa ushauri na Ishallah kama hali itawezekana Mwenyezi Mungu atujaalie hapa tulipo fika katika sekta hii ya elimu amayo ni sekta muhimu kuliko sekta zote kwa sababu ni sekta tegemezi kwa maendeleo ya jamii na nchi kwa jumla kuzungumza haya yafuatayo.

Mhe. Spika, tunajua kuwa ili tupate elimu tunahitaji wanafunzi, sehemu za kufundishia zilizo na hadhi ya kufundishia vifaa na mazingira mazuri ya kazi. Tunajua kwa sababu idadi ya wananchi inaongezeka hapa Zanzibar na kwa hivyo mahitaji ya elimu yanaongezeka. Na hivi sasa tuna skuli nyingi sana katika kila Majimbo kuanzia Unguja na Pemba inachua wanafunzi kuanzia ngazi za chini na kuelekea juu. Ili tuweze kumudu hayo mazingira tumeongeza vyuo na kadhalika.

Mhe. Spika, unapomchukua mwanafunzi kuanza kumfundisha na ili afaidike na yale masomo kwa namna lengo lilivyokusudiwa kuna mambo mengi sana ya kuyatekeleza,

1) Wanafunzi wanahitaji kuwa na walimu wenye ujuzi
2) Aweze kukaa pazuri
3) Awe na cha kuandikia
4) Aweze kupata vitu vya kuweza kumsaidia kujua kinachosomeshwa
5) Kwa wale wanaosoma sayansi kunatakiwa kuwe na maabara na ndani yake kuwepo na vifaa vinavyohitajika kwa daraja ile ya masomo
6) Kuwe na ukaguzi wa kina kuona shughuli za ufundishaji zinaendelea vipi

Mhe. Spika, nashukuru tumejenga majengo mengi sana. lakini Mhe. Waziri anakwenda kutokana na bajeti yake anayopitishiwa. Kwa sababu ya mahitaji ya elimu huwa haitoshelezi hata kidogo ndio tukaona hivi sasa kuna baadhi ya mashule hakuna vikalio wala hakuna meza. Kuna shule nyingi tu zenye elimu ya sekondani kuanzia darasa la tisa mpaka la kumi na mbili na kuendelea hakuna maabara na wala hakuna vifaa vya maabara na nyingi ambavyo vipo si kamilifu, lakini hata wale tunaowaita *lab-assistance*, hamna.

Mimi ushauri wangu kwa Mhe. Waziri ni kuwa pamoja na fedha haimtoshi aliyopitishiwa lakini kwa sababu yeye mwenyewe ni mwalimu na ndio tukaiyona Wizara ya Elimu imekuwa hivi, namuomba atafute kila inavyowezekana kwa vile ni mwepesi wa kuomba misaada hufanikiwa

kutokana na uhodari wake ili tuone kuwa hii hali ya kuwapatia wanafunzi wetu vikali katika skuli zetu inapungua kwa kazi kubwa sana. Hatuwezi kuikamilisha kwa mara moja lakini angalau kasi iwe inapungua kwa kasi kubwa sana. Ishallah huko tunakokwenda iwe kila mwanafunzi awe kwenye kiti na meza zilizokuwa nzuri na kufanya kazi zake inavyohitajika.

Mhe. Spika, pia kuna majengo mengi sana kwa makusudi serikali kupitia Wizara iliwaomba wananchi wawasaidie kujenga haya majengo kwa kuondoa shida ya wanafunzi wetu. Lakini bado mpaka leo majengo yale, nguvu za serikali kutokana na ahadi yake kuwa yanapofikia linta yataezekwa lakini haijawezekana kwa sababu ya kuwa si kuwa hataki yaezekwe lakini kutokana na uwezo wa bajeti yake inavyomruhusu.

Kwa sababu tulihimiza kufanya hivi tulijua kuna wanafunzi wataongezeka na wanafunzi hawa watakuwa na mahitaji ya majengo haya. Namuomba Mhe. Waziri hili aone kwa kubakia majengo yale bila ya kuezekwa ni kubakisha tatizo lile ambalo lilikuwa Wizara kwa makusudi na kwa nia safi ilikuwa iliondoe. Kwa hivyo katika misaada yake pamoja na kuwa mara nyingi yeye anaangalia mbele twende wapi ili tuwe na watu. ambao ni *comparative* katakana dulia hoi. Lakini *back ground* nayo ina umuhimu wake aangalie namna gani kuondoa matatizo huku chini. Ujimjenga mtoto chini ndivyo atakavyokuwa mtoto bora huko tunakokwenda.

Mhe. Spika, kwa sababu maskuli yanaongezeka, wanafunzi wameongezeka na vyuo vimeongezeka na wengi sana alhamdulillah wanapasi wanaingia katika skuli kadhaa. Lakini wengine kwa mazingira hubakia kama ni wanafunzi waliobakia katika dahalia.

Hapo zamani Mhe. Spika, mwanafunzi akishakufaulu katika masomo yake anakwenda katika dahalia basi kule ilikuwa akipokea kama ni mwanafunzi mwenye mahitaji makuba sana. Alikuwa hapeleki chochote kule isipokuwa nguo zake mwenyewe, lakini vyengine vyote alikuwa anahudumikiwa na serikali tokea malazi, mpaka chakula. Kwa hivyo mwanafunzi alikuwa ana utulivu mzuri wa kushuhulikia masomo yake. Hivi sasa wanafunzi wanasoma na wanapasi na wakipasi namshukuru Mhe. Waziri anawatangazia vyuo kadhaa kutokana na namna alivyopasi au alivyofanikiwa katika mitihani. Kwa bahati mbaya sana wale wanafunzi inabidi wajitegemee wenyewe katika chakula japo kuwa mchango wanaotoa si mkubwa hata hivyo. Lakini kupata mchango wa kuweza kukufanya kuweza kuishi katika mahali mbali na nyumbani nakushuhulikia hili somo ni kazi ngumu sana na ni mzigo mzito sana kwa wazee.

Hivyo basi ili lengo lifikiwe na wanafunzi wapate utulivu wa kuweza kuyamudu masomo yao, ningemuomba Mhe. Waziri arudishe ile hali tuliyokuwa nayo zamani tuliyokuwa nayo zamani iliyotufanya sisi tukaweza kusoma na kuweza kufanikiwa kwa kupata utulivu katika dahalia, ni vyema hawa wanafunzi wasaidiwe kwa chakula. Tunao wanafunzi 1993 Dahalia hivi sasa sijui ni kwa namna gani Mhe. Waziri, lakini zile shida tunazijua sisi. wengine tunao hapa na sisi ndio wawakilishi wao na tunajua namna wanavyohangaika.

Japo kuwa sio Wizara yake lakini hata Chuo cha Afya Mbweni kuna watu kama hawa. Kwa bahati mbaya sijaangalia vizuri lakini naona wanawake ni wengi sana. Kwa hivyo angalia mtoto mwanamke kwenda mwahala na akawa anajitegemea mwenyewe kwa chakula wakati huku nyumbani anakotoka hali ni ngumu sana. Haya mambo mengine yote ambayo kuwa tunayapiga vita ndio pengine ni moja katika sababu yanayosababisha yatokee. Kwa hivyo tuwatulize watoto wetu ili wapate kula, ili waweze kusoma vizuri. Njia za kufanya ni utaalam ataweza kufanya na kuweza kujua wapi pa kupunguza palipokuwa si muhimu sana lakini angalau hawa watoto wasaidiwe kwa chakula.

Mhe. Spika, chengine huu ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia, watoto wetu wanahangaika. Pale zamani ilikuwa angalau watu wanafanya mitihani hii ya masomo ya sayansi kwa kujibu kwenye karatasi tu lakini hivi sasa mtindo umebadilika wanafanya *practical* kama tulivyokuwa tukifanya sisi. Mashule yetu kwa bahati mbaya kuna upungufu mkubwa wa hivi vifaa vya maabara, ni ghali na sisi weheshimiwa wawakilishi hufikwa na shida kubwa inapofika wakati wa mitihani wa kuchangia ili angalau watoto wetu kwa mambo mengine madogo madogo waweze kuyamudu kwa kujifanyia mazoezi kabla ya siku zao za mtihani.

Mimi nashukuru Mhe. Waziri kwa kuhimiza kuwa popote panapojengwa jengo jipya pawe na chumba cha maabara. Tumeshafanya hivyo na tunamuomba kwa zile skuli ambazo hazijapata vifaa hivi vya kufundishia mambo ya sayansi visaidiwe angalau kwa ile hatua ya level ya elimu yao ili waweze kuyamudu yale mazingira vyenginevyo utaona ndio sababu ya watoto wetu wengi wanafeli kwa sababu hawaoni yale mambo yanavyotakiwa yafanywe kwa kuyafanya kwa vitendo.

Mhe. Spika, sisi tuliposoma mfano tulikuwa tukisomea uwalimu hapa Nkuruma, tulikuwa tuna mwalimu wetu akitusomesha *Chemisry*, mwalimu Njeketu, lakini siku moja tu alikuwa akiingia *laboratory* wiki nzima tunakwenda wenyewe hatuhitaji tena mwalimu kwa sababu kila kitu kilikuwa kipo. Juzi tulipokwenda kuangalia kule ikiwa sasa ni Chuo Kikuu tulishangaa kuona kuwa wanafunzi inabidi *practical* zao nyengine wakafanyie Dar-es-

Salaam kwa gharama kubwa sana. Kwa hivyo ili tuendelee katika hilo lengo linalohitaji sayansi na teknolojia tuone kuwa vifaa hivi vya maabara ni muhimu sana na Mhe. Waziri ajitahidi ili ile hali ipungue *at list* kama haikuwezekana kwa wote liwekwe katika *centers* maalum ili wanafunzi waweze kufika kwa urahisi na kuweza kufanya *practical* zao.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningeliomba kwa Mhe. Waziri kuwa katika Jimbo langu kuna Kisiwa kimoja kinaitwa Kokota na kile ndio kisiwa kilichokuwa na watu wengi sana miongoni mwa katika visiwa vilivyokuwemo katika jimbo langu. Wananchi wa Kokota wapo katika hali ngumu sana kule hakuna skuli, hakuna kituo cha Afya na wako mbali sana na hii nchi kavu ni kisiwa kilichojitenga mbali mpaka upite Fundo na kadhalika ndio ufike Kokota. Kwa kuondoa shida ya wananchi tumejitahidi. Nashukuru Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi waliwahi kwenda, tumejitahidi na kule tumejenga banda la skuli. Natumai kama sikosei limeshafika linta.

Kwa hivyo kwa makusudi namuomba Mhe. Waziri atembelee Kokota alione hilo jengo na vile vile kumuomba msaada wake kutusaidia tumalize kwa pale tulipofika ili wale watoto waweze kuanza kusoma kama walivyowenziwao. Mimi sijisikii vizuri nikiona shehe Said yeye katika Visiwa vyake kile kimoja kina skuli kingine kina hospitali lakini mimi nikawa nina majengo matupu na siku ya safari hiyo ningelimuomba anialike ili nimtafutie watu wa kumuombea duwa.

Mhe. Spika, katika skuli tunakuwa tuna masomo mengi tunasomesha na skuli zetu ni nyingi sana, tunakuwa na matatizo hasa ya walimu wa sayansi. Kwa hivyo kuna kitu tunaita *pert time teachers* yaani mwalimu anakuwa anasomesha shule hii, siku nyengine anakwenda shule ile, yaani anakuwa hana utulivu wa kituo kimoja kutokana na uhaba.

Ombi langu ni kamba hawa *pert time teachers* wengine wanakwenda masafa makubwa sana. Na kwa sababu skuli nyengine ingeliwezekana kupata walimu kama ingelikuwa walimu wale wana pahali pa kuishi. Ushauri wangu kwa Mhe. Waziri ni kuwa tuanze mkakati maalum wa kujenga nyumba za walimu kwa zile skuli ambazo ni zenye mazingira magumu na kule ambapo kuna masomo ya juu yanataka kufundishwa.

Kama haikuwezekana si vibaya wizara ikajipanga katika utaratibu wa kushirikiana na masheha ili mwalimu yule apatiwe nyumba akodi na wizara ihudumikie kama ilivyokuwa hapo zamani.

Mwisho kwa sababu ya wakati ni kwamba Mhe. Waziri nashukuru kuona kwamba vyuo vya *Qur-an* unavishuhulikia pia na skuli zetu. Watoto

wanaosoma chuoni na watoto wanaosoma skuli ndio wale wale. Mhe. Spika, watoto ni binadamu kwa hiyo binadamu yeyote anataka mapumziko ili aweze kuvuta fikra mpya za kuendelea na shughuli nyengine. Mhe. Spika, hata sisi Mwenyezi Mungu katujaalia kuwa ni lazima tupate usingizi wa kutosha kiwiliwili kiweze kupumzike tukiamka siku ya pili tuweze kufanya mengine katika hali ya utulivu.

Mhe. Spika, matatizo yanayojitokeza kwa uzoefu ni kuwa mwalimu anayesomesha chuo cha kur-ani anataka mtoto wake aendelee na afanikiwe, lakini na mwalimu anayesomesha skuli yuko katika hali hiyo hiyo. Kwa hivyo, mtoto anakuwa hana utulivu na hapumziki hata kidogo.

Mhe. Spika, wakati mwengine inapofika hiki kipindi cha wanafunzi kufanya mitihani, watoto wengi huwa wanakwenda katika *tuition* kuanzia darasa la saba na kuendelea. Lakini na walimu wa chuoni huwa hawawakubalii mpaka mimi ulinifika mtihani mmoja. Mhe. Spika, naomba dakika mbili zaidi kulieleza hili, nilikuwa na mtoto wangu anasoma darasa la saba akaona aende *tuition* kule mjini kwa sababu kuwa kule watoto wanapasi sana, lakini na huku anahitajika chuoni. Nilipokwenda nikaikutia kesi hii mtoto anataka kusoma na mwalimu wa chuoni anamwambia huondoki kuna tafsiri kur-ani hapa. Mhe. Spika, mimi nikanyamaza kimya nikatoa uhuru maana yote ni mambo muhimu, yule mtoto akenda akasoma na akapasi darasa la saba.

Mhe. Spika, bahati mbaya huku chuoni ikabidi afukuzwe hakutii amri ya mwalimu wa chuo. Kwa hivyo, ninaiomba wizara kwa vile hizi taasisi zote zimo katika mamlaka yake aweke utaratibu ili shughuli katika chuo cha kur-ani na kwenye skuli zifanyike vizuri kwa maslahi yule mtoto.

Mhe. Spika, nilikuwa nina mengi sana yakuzungumza lakini kwa sababu naona robo saa imemalizika na dakika moja juu, naomba kumaliza hapo. Ahsante sana.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kutufikisha katika hali ya uzima na tukaweza kuchangia bajeti hii. Pili nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Makamishna, Wakurugenzi, Walimu Wakuu na wote ambao walishiriki katika kuiandaa bajeti hii.

Mhe. Spika, mimi kusema kweli nilikuwa sina nia ya kuichangia hii bajeti nimepewa maombi na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini ndio imenipa nafasi nisimame ili niyaombe. Maombi haya tumeshayaomba kwa maandishi,

kwa maelezo lakini kwa umuhimu wake nimeona na hapa nisimame huenda waziri na wahusika wakanionea jicho la huruma.

Mhe. Spika, katika jimbo langu la Mfenesini nilipoingia mwaka 1995 tulishauriana na wananchi wangu kwamba sisi tuwekeze kwenye elimu zaidi na mengine ndio yafuatie. Kwa nia nzuri hiyo Mwenyezi Mungu ametujaalia kweli tumewekeza kwenye elimu. Kwa nini? Kwa sababu mwaka 1995 Jimbo la Mfenesini lilikuwa na skuli moja tu ya Mfenesini na bahati ilikuwa jimbo limeanzia Kiwanda cha Viatu hapa tukawa na Skuli ya pili ya Bububu, baada ya kukatwa jimbo yakatoka matatu mimi nikabaki na jimbo langu mpaka wangu uko meli nane kwenye kituo cha mafuta. Eneo hilo lote sasa hivi shehia sita tumeshajenga skuli kuanzia Mfenesini wenyewe tuliyoikuta mwanzo skuli mama, lakini tumejenga Mwakaje na Mwakaje bahati nzuri Shehia moja tumejenga skuli mbili, moja iko Mwachealale, tumejenga Mbuzini, tumejenga Chuini, tumejenga Kama na sasa tunamalizia Meli nane shehia ya mwisho.

Mhe. Spika, tunashukuru kwamba mote humu jitihada za serikali kupitia Wizara ya Elimu wametusaidia tukishafika hatua ambazo wenyewe wanataka wanatumalizia. Mhe. Spika, siri iliyokuwepo katika ujenzi wa skuli hizi unapoanzisha skuli usisite kila mwaka muendelee kwa sababu kama utajenga banda moja halafu ukisita itabidi wanafunzi uwahangaishe, wakishakuja hapo itabidi uwatowe uwapeleke skuli ya jirani. Hiyo ndio hatari sasa hivi iliyokuwepo katika jimbo langu.

Kwa mfano, Skuli ya Mwachealale watoto walikuwa wanakwenda kusoma Skuli ya Kitope na nusu walikuwa wanasoma Mfenesini, lakini baada ya kujenga pale sasa hivi wote wamesehelea kijijini kwao. Banda la mwanzo tulilojenga limejaa na sasa hivi tumejenga la pili lakini bado halijakamilika liko ngazi ya kuezekwa. Kwa hivyo, tunaishauri wizara kabla watoto hatujawagawa tena kama mwanzo kuwapeleka Kitope na kuwaleta Mfenesini watusaidie ili tuweze kuliezeka lile banda.

Mhe. Spika, tatizo kama hilo pia liko Mbuzini, Mbuzini walikuwa wanasoma Skuli ya Bububu ama waende Chuini na wao tumejitahidi tumejenga na tumemaliza sasa kuna banda jengine ambalo wale vijana waweze kuingia mle lakini bado hatujapata msaada wa wizara. Kwa hivyo, tunaomba na pale tupunguze usumbufu ili wanafunzi wasehelee pale pale Mbuzini.

Mhe. Spika, jambo la tatu ni kwamba Skuli ya Kama *TASAFF* mwaka jana tulikuwa na nyumba ya Mwalimu Mkuu tukaitia saruji vyumba viwili na *black board* wamesoma watoto vyumba viwili mle na mwaka huu tumeshatia cha tatu ukumbi lakini bado vijana wamekuwa wengi. Mhe. Spika, pia tayari

tumeshajenga banda la vyumba vinne na tumemaliza kila kitu tunaomba wizara kwa skuli zangu hizo tatu wakatupa kipaumbele.

Mhe. Spika, jambo la mwisho ni kuhusu Meli nane sasa hivi ni mjini sawa sawa na ilivyo Kihinani, Bububu wenyewe, ilivyo Kijichi huko kote sasa hivi ni mji. Kwa hivyo, tunaomba na Meli nane nako tusaidiwe ili kupunguze watoto kuhangaika kuja Bububu ama kwenda Kijichi ama kuja Chuini. Naomba hilo Mhe. Waziri ulitizame kwa jicho la huruma ili tuweze kupunguza matatizo ambayo wanayapata wananchi wetu.

Mhe. Spika, jengine mimi jimbo langu limefika mpaka Kijichi upande mmoja, hivi karibuni tunaipongeza serikali, wizara pamoja na wenzetu wa nchi ya China kusaidia kujenga skuli na tayari imeshafunguliwa. Jana nimepita katika eneo lile nikapata salamu za wananchi kuniona wakanita wakaniambia mheshimiwa tunashukuru kwa jitihada mlizofanya lakini kidogo mipango iliyopangwa hatukupendezewa nayo, hivyo tunaomba tukupe ushari wetu ukaupeleke. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri nimepewa ushauri na watu wa Kijichi katika skuli mpya iliyofunguliwa juzi kama wameelewa vibaya basi utatoa maelezo ili wafahamu vizuri.

Mhe. Spika, wameniambia kwamba pale pana watoto wengi sana wanasoma Bububu wa darasa la kwanza na kuendelea. Lakini skuli iliyofunguliwa wanasema kwamba watachukua watoto kuanzia darasa la tano kwenda mbele. Mhe. Spika, nia ya wazee walitaka wale watoto wadogo chumba cha kwanza mpaka la nne wasisumbuke kwenda Bububu kutokana na hali njia ilivyo na magari yalivyokuwa mengi, walidhania watasehelea pale. Mhe. Spika, kumbe pale watabakia watoto kubwa na wale wadogo wasumbuke waende kule kule Bububu.

Kwa hivyo, wanaomba kama uwezekano upo basi pale paanze na darasa la kwanza, la pili, la tatu na la nne ili watoto wadogo wasipate matatizo ya kutoka pale kwenda mpaka Bububu. Kama walielewa vibaya wizara itazungumza ili wananchi wale wafahamu huku wengine nasikia wanasema pale itakuwa skuli ya watoto wenye vipawa maalum. Haya yote hayo yana matatizo wananchi wa pale hawajajua ukweli uko wapi, namuomba Mhe. Waziri ukipata nafasi ya kuja kufanya majumuisho uwatoe wasi wasi wananchi wa Kijichi juu ya skuli mpya iliyofunguliwa.

Mhe. Spika, nikiendelea kuzungumza juu ya suala la walimu na mimi nilipitia ualimu miaka miwili mitatu, nilikwenda chuoni na baadae nikarudi nikasomesha Skuli ya Mfenesini lakini siasa ikanizonga ndio mpaka leo nimesehelea kwenye siasa. Mhe. Spika, ni kwamba bado walimu wenzangu wanapata shida kubwa na uzuri sisi kama tumepita kwenye kazi hizi lazima

tukereketwe tuwasemee wenzetu, wao wanasema lakini na sisi sauti zetu zinafika mbali zaidi. Jambo kubwa sasa hivi linalowasumbua walimu ni kwamba bado usafiri wa kutoka mjini kwenda mashamba kusomesha unawasumbua. Mhe. Spika, kila siku zikicha mafuta yanazidi bei lakini nauli iko pale pale wanayolipwa.

Kwa hivyo, ningeliomba Mhe. Waziri hii mara ya pili kulizungumzia hili tukasema angalau skuli za karibu zitafutiwe gari, zamani ilikuwepo hivyo walimu walikuwa wanapelekwa walimu kuanzia Mahonda, Bumbwini, Fujoni wanakuja mjini hapa wanarudi majumbani mwao vizuri kabisa. Mhe. Spika, mwalimu anatakiwa darasani ukenda upendeze na watoto wapate mfano wa kwako, lakini unaondoka nyumbani umependeza unapanda gari la saruji unafika kule umechafuka. Kwa hivyo, naiomba wizara ingeliangalia utaratibu wa kuwaongezea mshahara ama kuwaongezea hizi nauli za usafiri ili mwalimu akapata kwenda safi akarudi safi. Hili nadhani likiondoshwa walimu watakwenda kwa furaha kusomesha na watafika katika hali nzuri kabisa.

Mhe. Spika, nikimalizia sehemu ya walimu nije kwenye marekebisho katika Wizara ya Elimu. Mhe. Spika, tunashukuru nyongeza zimefanywa lakini bado baadhi ya walimu nyongeza hizi hawajazipata na hivi sasa unakaribia mwezi wa tatu wameshajaza fomu lakini wanaambia hali kidogo ngumu. Mhe. Spika, hali ngumu wakati wenzao hali laini wanapata kidogo wanapata kusononeka, namuomba Mhe. Waziri hawa wenzetu ambao bado neema hiyo hawajaipata na tayari wameshajaza fomu basi watume wahusika na wao wachacharike ili na wao wapate fedha zao.

Mhe. Spika, fedha hizo pamoja na kuwa tayari miezi mitatu wenzao wameshatangulia mbele ningelipendekeza kwamba na haya marupurupu yao ya huko nyuma basi wangelifanyiwa wakaunganishiwa pamoja ili na wao wakenda sambamba na wenzao. Mhe. Spika, nadhani upande wa ujenzi wa skuli wa mabanda pamoja na upande wa walimu niishie hapo sasa nije katika ukurasa mwengine unaozungumzia makumbusho.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 17 nashukuru kwamba hivi sasa wizara inasimamia uzuri sehemu zote ambazo za historia na zinafanyiwa ukarabati kwa lengo la kuwa vijana wetu watakaokuja baadae waweze kujua kwamba Mwinyi mkuu alikuwa na nyumba ngapi, anakaa wapi hii inasaidia sana.

Ninachoomba mimi kwamba hapa Chuini kwenye Hoteli ya Mawimbini ubavuni kwake na sisi tunalo gofu moja sijalifuatilia alikaa nani hapo lakini pana gofu ambalo juu walifanya kama ghala ya kuwekea watumwa na chini ndio alikuwa anakaa mwenyewe huyu ambaye alikuwa anatumia gofu hilo. Pia pana kama rasi imeingia kajenga msikiti upande wa pili amefanya daraja

anatoka kwenye nyumba yake anakwenda kwenye msikiti bahati nzuri kwenye msikiti kule wamejenga hoteli kuna kampuni fulani inaitwa Sitaki Matata. Mhe. Spika, hili gofu safari hii zimeombewa pesa katika Mradi wa TASAF nasikia zimepatikana wanalisafisha wananchi ili waweze na wao kuweka mradi waje wageni wakague waweze kupata chochote.

Mhe. Spika, katika kitabu sikubahatika kuliona hilo kuandikwa. Kwa hivyo, mimi nashauri Mhe. Waziri ukikaa na watendaji wako basi mjue kwamba na Chuini pana gofu la historia na hivi sasa tayari linafanyiwa kazi ili muweze kulitia kwenye kumbukumbu lijulikane na tuweze kujua historia yake alikuwa anakaa nani na kwa madhumuni gani. Naomba hilo nisaidiwe kama lipo basi Mhe. Waziri akija hapa ataniambia kama tunalo na alikuwa anakaa mtu fulani kwa madhumuni fulani.

Mhe. Spika, kwa kujali muda wako nimalizie katika uchangiaji wa mwisho nije kwenye ukurasa wa 57 juu ya suala zima la kitengo cha elimu mjumuisho. Mhe. Spika, elimu mjumuisho kwamba wengi tumefurahika nayo kwa sababu siku za nyuma ilikuwa watoto hawa wenye taahira, wenye matatizo mbali mbali ya ulemavu walikuwa wanafichwa na wazee wao na wanakosa haki ya elimu. Lakini kwa kuhamasishwa hivi sasa watoto wale wanatolewa na wanapata haki zao za elimu. Mhe. Spika, bado mimi nilikuwa nina wasi wasi juu suala zima la kuchanganya hawa watoto ambao wenye taahira pamoja na watoto wa kawaida. Kweli hivi sasa dunia haitaki watu wabaguliwe lakini nahisi bado utaalamu tunaoutumia katika kusomesha bado watoto hawa ufahamu wao itakuwa ni mdogo.

Mhe. Spika, wenzetu Tanzania Bara wanao watoto kama hawa na wamefungua skuli za *primary* mpaka sekondari wanasoma mbali mbali. Primary iko Malapa na wakipasi hapo wanakwenda Mikoa mbali mbali moja Tabora wanaendelea na sekondari. Kwa hivyo, na mimi ningeshauri pamoja na kwamba tumeanza katika hatua hii lakini sio vibaya tukajenga majengo maalum pengine kwa kila Mkoa ili tukasomesha vijana kuanzia *primary* pamoja na sekondari ili na wao wende kwa wakati na waweze kusoma kwa nafasi. Hii mimi nashauri kwamba itatusaidia katika ufahamu wale watoto wenyewe pamoja na walimu kwa sababu ninavyofahamu mimi kama ni elimu mjumuisho basi aweke mwalimu anayesomesha taahira na aweko mwalimu anayesomesha wa kawaida.

Mhe. Spika, nashauri kwamba tungeweza kujenga skuli maalum tukawaweka vijana hawa nadhani wangepata taaluma ya kutosha pamoja na kuwa sisi tumejiandaa kuwachanganya na wenzao si jambo baya. Ushauri wangu kama utakubalika Mhe. Spika, naomba ufanyiwe kazi. Mhe. Spika, baada ya hayo machache sana nimeona nitoe baraka yangu pamoja na kuleta maombi yangu niliyotumwa na wananchi wangu naona nimeyakamilisha. Baada ya hayo mimi

mwenyewe binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini tunaiunga bajeti hii mkono kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru sana kutia baraka zangu katika bajeti hii kwa bahati nzuri ni Mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii Wanawake na Watoto mara kwa mara huwa tunakutana na wenzetu hawa tunabadilishana mawazo. Kwa hivyo, mambo mengi kimsingi nayafahamu kwa kiasi fulani, lakini hata hivyo nasema huu ni msimu wa bajeti lazima tuzidi kukumbushana yale tuliyoambizana nyuma.

Kwanza nataka niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote na walimu wenzangu wote kwa kazi ngumu ya kuwasomesha watoto wetu na kuisimamia wizara hii. Kwa kweli sisi tunaotoka huko tunafahamu uzito wa kazi ya ualimu, lakini wenzetu wanasema kazi hii ni kazi ya wito malipo hasa utarajie kwa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, jambo la pili na mimi nataka niungane na wenzangu kumpongeza na kumtakia kheri Mhe. Haroun Ali Suleiman kwa ujasiri wake wa kujitokeza kuchukua fomu ya kuania Urais wa nchi hii ni haki yake ya kikatiba na Mwenyezi Mungu *inshaallah* kama kuna kheri na yeye basi *inshaallah* Mwenyezi Mungu atampa, kama hakuna kheri na yeye basi Mwenyezi Mungu hatompa wala hatosikitika nafikiri.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika jimbo langu sasa. Mhe. Spika, katika jimbo langu nataka nizungumzie juu ya ujenzi wa banda la Mkanyageni ambalo tayari limeshamalizika bado kuezekwa, lakini bado hatujabahatika kuezekwa. Kwa hivyo, namkumbusha Mhe. Waziri katika awamu hii akijaaliwa kupata fedha basi naomba anikumbuke pamoja na banda la Michenzani. Nataka nirudie tena wito wangu kuwa Skuli ya Kisiwa Panza ambako kuna mabanda tokea yaliyojengwa miaka ya 69 ilipoanzishwa ile skuli iliyojengwa kwa mawe, chokaa na udongo.

Mhe. Spika, yale mabanda ni mabovu na kweli ni hatari kwa watoto wetu kusoma katika mabanda yale. Hili suala nimeshalizungumza mara nyingi lakini bado Mwenyezi Mungu hajajaalia kutekelezwa haya ninayoyazumza labda mpaka siku moja lije lianguke liwaumize watoto pengine ndio wenzangu watazinduka. Lakini *inshaalla* Mwenyezi Mungu atajaalia hatutafika huko watatekeleza.

Mhe. Spika, pia nataka niulizie juu ya maandalizi ya ujenzi wa sekondari ambao tumebahatika moja ni Jimbo langu la Mkanyageni. Mhe. Spika, sijui maandalizi ya ujenzi huo yamefikia wapi hilo pia nitamuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka ufafanuzi kidogo juu ya hii elimu ya maandalizi. Mhe. Spika, sera ya elimu tuliyoipitisha hapa mwaka 2006 inaeleza kwamba elimu ya maandalizi sasa itakuwa ni elimu ya lazima, imejumuishwa katika elimu ya lazima. Wananchi kwa kuitikia wito huo katika vijiji vingi wameanza kujenga vituo hivi vya maandalizi. Je, wizara inasaidia nini kwa wale wananchi ambao wamejitokeza kuanzisha vituo kama hivi. Kwanza inasaidia nini kwa upande wa vifaa na wale walimu wanaojitolea kusomesha watoto inawapa posho ya kiasi gani?

Mhe. Spika, jengine kwa ujumla mimi katika kazi ambayo ninaiona ngumu ni ya ualimu haidhuri malipo yake ni madogo ni hii ya maandalizi kwa sababu inakuwa unakaa na watoto wadogo wanaweza wakajichafua pale pale kwa kweli ni kazi ya ulezi, maana unafanya kazi mbili kwa pamoja. Mhe. Spika, ndivyo tulivyokuwa tukiambiwa zamani kwamba mwalimu unakuwa unafanya kazi ya ulezi halafu unafanya kazi ya kufundisha, lakini kwa kweli ya ulezi inakuwa ni kubwa.

Kwa hivyo, maandalizi ya haya walimu sijui wizara imejipanga vipi kuwasomesha hawa walimu wa maandalizi wakati sasa hivi tunasema hii ni elimu ya lazima. Hii sera itatuchukua muda mrefu sana kama maandalizi yetu katika elimu ya maandalizi yatakuwa yanasuasua kwa sababu naona wizara huku juu kwenye elimu ya juu, sekondari, msingi naona inajitahidi lakini kwa kweli kwenye maandalizi naona maandalizi yake sio makubwa sana. Mhe. Spika, sera sasa hivi ni mwaka wa nne tokea ipitishwe. Kwa hivyo, labda Mhe. Waziri atwambie hasa wizara imejipanga vipi katika kuwaandaa walimu wa skuli za maandalizi ili kwenda sambamba na hii sera, sera tutakuwa nyuma sana kila tukichelewa kuandaa walimu wa maandalizi. Mhe. Spika, vituo hivi lengo lake itakuwa ni kulea watoto zaidi kuliko kuwapatia elimu.

Mhe. Spika, siku moja nilibahatika kuna skuli moja hapa ya *private* hapa Mbweni kwa kweli nilikwenda pale nikaona watoto wadogo wanavyozungumza Kiingereza, lakini hawa watoto wako katika maandalizi. Mhe. Spika, mimi sitaki watoto wetu wafikie kama wale, mimi najua kama ni ngumu kwa muda mfupi kuwa na *nursery* za aina kama hiyo hasa za serikali, lakini angalau nataka iwe robo ya kama ile. Lakini mtoto kukaa maandalizi miaka miwili akaondoka pale anaingia darasa la kwanza hajui chochote huu ni mtihani mkubwa, hiyo ndio hali ilivyo sasa hivi. Kwa hivyo, inaonekana kama maandalizi yetu bado hayajakuwa mazuri.

Mhe. Spika, pia nataka nizungumzie kidogo juu ya viwango vya kufaulu, nimeangalia ukurasa wa saba kwenye jadueli F. Mhe. Spika, nimeangalia hapa kwa mwaka 2009 idadi ya watahiniwa kidato cha nne walikuwa ni 8725, waliofaulu daraja la kwanza ni 40, daraja la pili, 166 kwa kweli mheshimiwa

hapa ndio unapoona kwamba *quality education* hapa hatujakuwa nayo. Mhe. Spika, wengi wa vijana wetu wanaishia divisheni IV na hao wanaofaulu wengine ni divishen III ni Dini na Kiarabu.

Mimi ni Muislamu na naipenda sana dini yangu ya Kiislamu, lakini najua tu kwamba nchi yoyote inayotaka kuendelea hata hao wenzetu wa Iran nao ni Waislamu mataifa mengine ya wenzetu Waarabuni ni Waislamu kama sisi, lakini pamoja na watu kushughulika sana na Uislamu na dini yao ya Kiarabu lakini hawako nyuma katika mambo ya sayansi. Mhe. Spika, leo Wairan ni tishio ulimwenguni kwa sababu ya kutengeneza mambo ya *nuclear* lakini ni Waislamu na wao wale. Lakini sisi hapa watu wote wanakimbilia diploma, digrii ya dini na kiarabu. Mhe. Spika, kwa kweli hii itasaidia kuimarisha dini kwa upande mmoja, lakini dini vile vile na dunia.

Mhe. Spika, vile vile ukiangalia kidato cha sita utaona kwamba idadi ya watahiniwa kwa mwaka uliopita walikuwa ni 2308. Hii peke yake inatupa ujumbe gani? Inatupa ujumbe kwamba serikali inatumia pesa nyingi sana kuwasomesha watoto, lakini wengi wanamalizia elimu ya msingi na kati. Mhe. Spika, kwa sababu bado idadi ni ndogo sana ukichukua wanafunzi 2308 kwamba hawa ndio vijana waliofanya mtihani wa kidato cha sita. Mhe. Spika, kama utafanya utafiti ukaangalia watoto hawa walipoanzia darasa la kwanza walikuwa ni watoto wangapi ambao mpaka leo wamemalizia 2308, inawezekana pengine walikuwa zaidi ya watoto 100,000 au 150,000. Hii haioneshi maendeleo mazuri ya elimu katika nchi.

Mhe. Spika, hapo hapo ukiangalia hata kiwango chao cha kufaulu utakuta wanafunzi wa daraja la kwanza ni 43 na daraja la pili ni 189, hii wenzetu wa Bara ni sekondari moja tu wanaweza wakafikia kiwango kama hiki. Kwa hivyo, bado nasema tuna changamoto kubwa katika kuimarisha ubora wa elimu kwa kuimarisha wingi tayari tumepiga hatua, lakini sasa naona tuwe na programu maalum ya kushughulikia na ubora wa elimu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije sasa katika Mamlaka ya Mafunzo ya Elimu Amali. Mhe. Spika, mimi nilibahatika katika kamati yangu kutembelea vituo vyote viwili cha Mkokotoni na Vitongoji. Kwa kweli Mhe. Spika, nilivutiwa sana na uzuri wa majengo na mandhari yenyewe kwa ujumla, lakini sasa kinachonivunja moyo kwamba tunaelekea kule kule kama Sekondari ya Ufundi ya Kengeja. Kwa sababu mpaka taarifa niliyonayo hivi karibuni bado Vitongoji wanafunzi wanasoma zaidi lakini hakuna vifaa vyovyote. Mhe. Spika, mwanafunzi pengine anakwenda kusomea pengine fundi bomba lakini hapana vifaa vyovyote.

Kwa ufupi bado vifaa havijakuwepo, sisi tulibahatika kwa kutumia kamati yako unajua tunajifunza sana tunatembelea Bara tunaona vyuo vya ufundi ukenda wewe mwenyewe utaona kwamba hapa kwa kweli ni chuo cha ufundi, kwa sababu muda mwingi vijana wanaupoteza kwa mambo ya *practical* na muda mchache ndio wa *theory*. Lakini hapa kwa kweli majengo ni mazuri, wenzetu wametusaidia hawa kwa pesa za walipa kodi wao lakini ukenda vijana wamejikalia na lengo halipatikani. Kwa hivyo, lazima tujitahidi ili skuli kuzijaza vifaa vinavyotakiwa ili lile lengo lililokusudia lipatikane, lakini ni jambo la kusikitisha na kuhuzunisha sana.

Mhe. Spika, sasa nije katika Chuo Kikuu cha SUZA kwa bahati hotuba ya Mhe. Waziri haikuweza kutueleza kila kitu najua haiwezekani ingekuwa buku kubwa sana, lakini nataka kujua maendeleo ya ujenzi wa Tunguu pengine *inshaallah* ikiwa mambo yatamuendea vizuri mheshimiwa aje aifungue mwenyewe hii. Kwa hivyo, maendeleo ya ujenzi hakutueleza na mimi ninachotaka kujua je, ile azma ya kuanzisha kitivo cha uhandisi bado ipo? Kwa sababu tulipotembelea pale wakati huo ujenzi unaanza katika jengo la utawala, katika maelezo tuliyopewa kulikuwa na azma ya kuanzisha kitivo cha uhandisi na tukafurahi kwa sababu Chuo Kikuu cha *SUZA* bado sasa hivi kinatoa fani moja tu kimejikita na kutoa elimu. Si vibaya kwa sababu ni hatua nzuri ya kuanzia kwa elimu.

Lakini Chuo Kikuu cha Serikali si vyema kujikita na fani moja tu, haidhuru tunayo taasisi ya Karume, lakini nadhani ipo haja kama ile azma yetu tunayo pale basi tuwe *serious* ionekane kweli kitivo cha uhandisi kitakapoanza kazi kiwe cha uhandisi isije ikawa kama hivi Vituo vya Mafunzo ya Amali cha Mkokotoni na Vitongoji. Hilo ndilo lililokuwa ombi langu.

Vile vile ningeshauri Mhe. Spika, wenzetu wa *SUZA* wakafikiria kuanzisha programu ya Shahada ya Pili. Tunguu wameanza angalau kwa fani moja ya sheria, sasa hivi wanatoa shahada ya pili ya sheria. Sasa nafikiri na sisi kutokana na shida au kwa uharaka wa maendeleo yetu mimi nafikiri tungefikiria zaidi kuanzisha shahada ya pili hapa hapa badala ya kutoa pesa nyingi kuwapeleka watu nje. Nadhani ni vyema tungefikiria kuanzisha shahada ya pili. Tukafanya vyovyote vile iwavyo lakini tukafikiria kuanzisha hivyo angalau katika fani yetu ya ualimu tuliyonayo.

Mhe. Spika, kabla ya kufunga hotuba yangu, naomba univumilie kidogo kuna suala la ufafanuzi kwa maslahi yetu sote. Katika jadweli nambari 30(a) kuna mwaka wa kwanza imerudiwa mara mbili. Sijui pale ilikuwa moja mwaka wa kwanza na moja mwaka wa pili, naomba hapo Mhe. Waziri atakapokuja atusaidie ufafanuzi zaidi.

La pili, katika hii stashahada ya ualimu kuna stashahada hii ya kawaida na kuna stashahada ya msingi. Suala hapa vile vile ningeomba ufafanuzi. Sifa za hawa wanaochukua stashahada ya kawaida na hii stashahada ya msingi sifa zao zinakuwa ni moja au wanakuwa sifa tofauti. Halafu viwango vyao vya mishahara wanaoanzia kazi ni sawa sawa au ni tofauti?

Mhe. Spika, sijamaliza lakini kwa kuheshimu muda wako na kwa kumheshimu Mhe. Waziri na kumpa raha na furaha naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia moja.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe. Spika, nami nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (*SW*) kwa kutuwezesha kufika siku hii tukiwa hai. Pia nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu kwa ufupi.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu pia nimshukuru Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa bajeti yake hii ambayo kwa kiasi cha ubinadamu amejitahidi sana kuielezea. Pia niwashukuru watendaji wake wote ambao wamesaidia kufika hapa tulipofikia. Nimshukuru pia Katibu Mkuu kwa kuongoza timu yake ya wafanyakazi ili kufikia malengo ya kukomboa nchi yetu kielimu.

Mhe. Spika, mimi kidogo nataka nichangie hapa katika ukurasa wa 30 Elimu ya Madrasa na Vyuo vya Quran. Mhe. Spika, zamani wakati sisi ni wadogo lakini tunakuwa na wakubwa wetu, tulikuwa tukikaa kwa watu ambao wametuzidi walikuwa wanatuimbisha kwa kusema kwamba, mtoto akitaka kusoma kwanza msomeshe Qurani. Hii nyimbo ilikuwa unaiona kama ni nyimbo lakini ni maneno ya busara sana na hekima mno.

Mhe. Spika, tusisahau kwamba sisi tumeumbwa na Mwenyezi Mungu na ametupa utaratibu wa maisha yetu na utaratibu huo unatoka katika Kitabu cha Qurani hautoki pengine popote pale. Mambo mengine haya yote yanatoka humo na ndio wenzetu ambao wameisoma Qurani vizuri kama alivyosema msemaji aliyemaliza sasa hivi Mhe. Haji Faki Shaali kwamba Wairan wanasoma licha ya kwamba wao ni Waisilamu na wanasoma na wanaongozwa na sheria za Kiislamu.

Lakini Wairani, moja ya siri ya mafanikio yao kwa sababu wao wameisoma Qurani vizuri mno na wameisoma badala yake wakaijua vizuri sana. Ndio maana inawaongoza kujua na vitu vyengine vyote vile. Wao hawakuingia tu kwenye sayansi na nini, lakini waliisoma kwanza Qurani wakaijua vizuri na misimamo hiyo waliyonayo kwa sababu wao wanaongozwa na hiki Kitabu cha

Qurani. Mtu yeyote ambaye anaongozwa na kitabu hiki hana sababu ya kuyumba au kuyumbishwa na mtu yeyote yule.

Sasa na sisi naomba Mhe. Waziri uone kwamba kuna haja ya kuwasaidia walimu wa madrasa. Mhe. Spika, ukija ukiwaangalia watu wanyonge zaidi hapa Zanzibar basi ni walimu wa madrasa. Walimu wa madrasa wametelekezwa, wamekuwa ni walimu wasio thamani kama kwamba hakuna jambo jema wanalolifanya kwa jamii.

Kwa kweli ukimkuta mwalimu wa madrasa hiyo nguo yake anayovaa hasa wa vijijini wewe utamuonelea imani na mwanafunzi wa chuo cha Quran ukimkuta hiyo nguo aliyovaa mwenyewe au kijuzuu chake wakati mwengine kimechanika chanika. Lakini mtoto ambaye anakwenda skuli madaftari yake mazuri, mle anamohifadhi mzuri. Yeye mwenyewe anakwenda akiwa nguo zake amepiga pasi lakini anapoelekea kwenye madrasa anavaa nguo yoyote tu ile, chafu, imechanika chanika, ovyo, basi inakuwa ni mtihani mkubwa.

Mimi naona kwamba Mhe. Waziri ipo haja kubwa sana ya wewe mwenyewe kwa imani yako, kwa sababu mara nyingi unachukua vitabu unasaidia, vile vitabu huvipeleki skuli unavipeleka kwenye madrasa kupitia sisi wawakilishi. Lakini bado kuna haja ya wewe mwenyewe au watendaji wako kuteremka chini kuviimarisha Vyuo vya Qurani ili kusudi kuweza kufikia maleno na matarajio yetu hapa duniani lakini na kesho akhera.

Mhe. Spika, pia pametajwa njia mbadala ya kuwahukumu watoto wetu kupitia zile bakora ambazo zimezoeleka. Mimi Mhe. Spika, hili sikubaliane nalo na kila siku nitaendelea kusema kwamba hakuna njia mbadala katika kufundisha mtoto, suala la elimu Mhe. Spika, ni jambo zito na kubwa, suala si kumpiga mtoto suala ni je, unamhukumu vipi mtoto? Hilo ndio suala la msingi. Lakini huwezi kuepuka mtoto kumpa adhabu chuoni au skuli, hayo ni mambo ya Kimagharibi na hawa wana lengo lao la kuiharibu jamii ili tuishi kama wanavyoishi wao. Sasa tukifika mbele ya Mwenyezi Mungu iwe sote hukumu yetu ni moja tu.

Lakini Mhe. Spika, hata ukija katika Qurani ni kwamba Mwenyezi Mungu anatwambia kwamba, hawa hawatatukubalia lolote lile tunalolitaka sisi mpaka tuwakubalie yale wanayoyataka wao ndipo na sisi yale madogo waturidhie kwa kuona kwamba ni makubwa kwetu kwa sababu sisi tuna shida nayo. Lakini hawa hawana nia njema na ndio maana kila siku wanatutafutia sheria, mikataba ya kimataifa, sijui kuridhia nini na nini na yote hayo anaangaliwa mtoto na mwanamke.

Leo hivi tunaambiwa mwanamke awe na haki sawa na sisi, kesho tutaambiwa tuhiji pamoja sawasawa, keshokutwa tutaambiwa nao watuowe. Kwa sababu hawa wana malengo mabaya, keshokutwa Mhe. Spika, sihasha tukaambiwa na wanawake nao waowe. Mambo ya Kimagharibi, haya masuala ya kuwa mtoto azaliwe asiulizwe ni Magharibi huko.

Leo kuna suala la kwamba mtoto atapozaliwa huna ruhusa maana yake mtoto aende kama vile mbwa umemfunga kamba akifika pahala aamue kupumzika, akifika hapa aamue kufanya hivi, yaani ajiongoze yeye mwenyewe wewe umemkamata umemfunga kamba. Kwa hivyo, mtoto atuongoze yeye yaani akimkosea mtu huna sababu ya kumwambia lolote, mtoto akimfanya mtu kitu huna sababu ya kumkemea wala kumfunza, hayo ndio mambo ya Kimagharibi. Ndio maana unakuta kwamba hata wakija huku kwetu wanadiriki binadamu Mzungu anavaa nguo anayotaka bila ya kujali maumbile yake.

Sasa na sisi wanataka watupeleke huko na bahati mbaya sana akina mama wanaona kwamba ni sawa tu wanapendelewa wawe sawa sawa na sisi kila kitu sawa, lakini tunakopelekwa siko. Lazima hili tuliangalie tena tuliangalie kwa sababu ya sisi tutakwenda kuulizwa mbele ya Mwenyezi Mungu tulikuwa tunachunga vipi familia zetu sasa tutasema nini wakati watoto wote tumewaacha waishi kama ng'ombe.

Mhe. Spika, katika hili mimi sikubaliani nalo hata kidogo. Tena Mhe. Waziri usilitie hili katika bajeti, usilizungumze kabisa liache tu. Kwa sababu utafika mahali utakwenda kuulizwa mbona ulilisema Mhe. Waziri? Mhe. Haroun jina la Mtume, Ali swahaba, Suleiman Mtume. Sasa mambo yote hayo matatu halafu unakuja kutuambia kama hivi? Kwa kweli baadaye majina kama haya yaliyofananishwa na Utume halafu unakwenda kusimama unaeleza vitu kama hivi kwa kweli haiingii akilini Mhe. Spika.

Mimi nakupenda na naomba kama walivyosema wenzangu kwamba umechukua fomu ya urais kutafuta ridhaa za Wazanzibari, una uwezo, unafaa na unataka kuitumikia nchi yako. Mhe. Waziri itumikie nchi na Mwenyezi Mungu *Inshaallah* atakupeleka kwenye malengo yako na sisi tuna matarajio.

Mimi nasema kwamba tutafute njia za walimu kuwaambia watoto wawake hukumu kwa njia hizi. Wasiwe wanawafanya watoto kama wako katika hali ya kupigana, lakini Mhe. Waziri ukitafuta hata huyo Mtume alipoipata elimu hakuipata hivi hivi tu, kabanwa mbavu. Kwa hivyo, inawezekana kwamba kwa wakati huo kubanwa mbavu kule ndio pigo, sasa wewe unapotaka kusema mtoto asipigwe sasa afanywe vipi? Hakuna njia nyengine. Kwa hivyo, hakuna njia mbadala zaidi ya hili, mtoto unamhukumu ili kumpa hofu na wasi wasi afikie yale malengo ambayo ndiyo matarajiao ya wazee wao lakini pia ndio

matarajio ya maisha yake na yako wewe unayemfundisha. Sasa ikishakuwa mnashindana hakuna mwalimu wala mwanafunzi kunakuwa na usomi tena hapo? Kwa sababu lolote lile anakwambia.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niingie katika hili suala la Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima. Mhe. Spika, zamani wazee wetu wengi walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Jitihada za makusudi zinachukuliwa lakini naomba na ninaiomba wizara kupitia watendaji wake kwamba wajitahidi sana kwa sababu hili tatizo bado lipo.

Tunahitaji wazee wetu ambao hawakubahatika kwa sababu mbali mbali kujua kusoma na kuandika, basi wizara ione kwamba ina sababu ya kushuka chini zaidi ili kutoa taaluma na itafute watu hasa waingie katika maeneo mbali mbali hasa kwetu mashamba huko. Wawatafute watu ambao watakuwa na ulazima wa makusudi kwa kuangaliwa na wizara ili kusudi kuwatoa watu katika kiza na angalau mtu ajue kusoma, kuandika na kuhesabu japo kwa uchache.

Nadhani tukifanya hivyo tutakuwa tumetekeleza wajibu wetu na watu kila mmoja anahitaji kujua angalau kusoma barua. Tukifanya hivyo itakuwa tumewasaidia sana.

Nikitoka hapo nije katika Elimu ya Maandalizi. Mhe. Spika, ili tufikie malengo kama alivyosema Mhe. Haji Faki, mtoto ili apate elimu lazima aandaliwe hapa chini. Mtoto huwezi kumuandaa juu. Mhe. Spika, huwezi kuzaa mtoto wa kiume halafu akaishi miaka 25 hajui lolote yeye yupo tu, halafu hata jando hajenda, sasa ikifika siku moja ukamwambia haya leo kaowe. Aka, itakuwa ni mashakil, inabidi umfundishe pale mwanzo, umpe maadili.

Ninachokusudia kukisema hapa ni nini? Ni kwamba kama tunakusudia kuwakomboa watoto wetu ni lazima tuwatafutie walimu wazuri na Mhe. Spika, walimu wa *diploma* wamo wengi ambao sasa hivi hawajapata ajira. Mimi nadhani hawa tuwafanye sasa hivi kwa makusudi kabisa kwamba, wawe ni walimu wa elimu hii ya maandailizi wawaandae vijana watoto. Kwa sababu mtu akishapata *foundation* pale mwanzo basi naamini atakuwa ana uwezo mzuri wa kuongoza.

Lakini unamuacha mtoto mpaka anaingia kwenye madarasa ya *forms* ndio unataka umuandae, unataka umuandae nini na huku nyuma hakupata msingi? Ndio wale leo nakwenda ku-s*olve paper*, ku-s*olve* nini, anafika Chuo Kikuu hajui lolote. Wapo hapa wanafunzi waliajiriwa hapa hapa kwenye Afisi yetu ya Baraza la Wawakilishi, waliajiriwa hapa na wamemaliza Tunguu sijui wapi huko, wamekuja hapa hawajui kazi na ana *degree*, kwa sababu chini hawakupata *foundation* wanataka kuja kupata maandilizi kwenye *forms* tu.

Anatafuta daktari mwenyewe kwa sababu anajua ni daktari kani*solvie paper* baba, sijui Maalim Haroun sijui nani.

Watu tusiishi kwa ku-*solve paper* tuishi kwa kutumia uwezo wetu, ndipo tutaweza kufikia malengo, ndio tutaweza kuikomboa nchi hii. Lakini ikiwa tutakwenda kwa misaada itafika pahali utasaidiwa lakini itafika pahali pia unapewa kazi ya kwamba sasa kazi hii ifanye huwezi. Utaifanya vipi kazi na aliyekuwa akikusaidia hayupo. Kwa hviyo, yule aliyekuwa akikusaidia sio kwamba kakusaidia, alikuwa akikuharibu wewe ulikuwa unaona unasaidiwa.

Kwa hivyo, mimi nadhani wizara iandae utaratibu makini, madhubuti na mzuri zaidi, ili kusudi vijana wetu ambao wamesoma *diploma* sasa hivi na wapo washuke chini waje wawafundishe watoto wetu, ili kusudi wakifika pahali watoto wale wawe wanaendela vizuri.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije kwa ufupi sana kwenye haya masuala ya maambukizi ya UKIMWI. Mhe. Spika, kitengo hiki ni kitengo kimoja wapo muhimu sana, lakini mimi suala hili naliangalia katika mtazamo tofauti labda na michango iliyotolewa na wenzangu. Hii ndio sifa ya kila mmoja kutoa mawazo yake.

Mhe. Spika, tatizo si skuli tu peke yake, mimi nasema mambo mawili yanachangia. Kwanza wazee, halafu haya matumizi ya simu. Zamani ilikuwa ukimtaka mtu hadi ukamdowee kwao au njiani, au umuulize rafikiri yake leo fulani anakwenda wapi. Lakini sasa hivi humuulizi yote hayo, unatafuta nambari yake ya simu tu. Halafu hata kama uko wapi unamwambia mimi ni fulani njoo pahala fulani tukutane. Unakwenda mnakutana, matokeo yake haya ambayo tunayakataza yanatendeka. Lakini wazee katika hili ni masuul.

Mimi siisemi wizara moja kwa moja katika hili, wazee tunajua majumbani kwa sababu wale watoto hawaishi misikitini wanaishi majumbani mwetu. Lakini tunawapa simu halafu akishakuwa na simu unajua mtoto ni mwanafunzi hana kazi pesa ya kutia *credit* iko wapi? Kwa vyovyote atakuwa anapewa na mtu huko, baba huulizi mtoto anasema ninakwenda *tuition* anakuja saa sita ya usiku akija unamfungulia mlango na ikiwa hujamfungulia mama yake anakwambia nenda ukamfungulie, humuulizi mtoto anarudi wapi hujali chochote sasa unategemea apate nini mtoto yule? Apate pesa au UKIMWI.

Kwa hivyo, pale maambukizo ya UKIMWI yatatokea Mhe. Spika, kwa sababu hakuna udhibiti. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake licha ya kwamba kuna kipindi alipiga marufuku suala la matumizi ya simu, bado lipigiwe marufuku suala la matumizi ya simu kwa wanafunzi wakiwa skuli. Hili wazee wao wanalichangia, kwa sababu bila ya mashirikiano

ya wazee jambo hili halitawezekana kwa sababu wazee wanawapa watoto wao simu kwa kuona kama wanawapenda sana matokeo yake unatokea uharibifu.

Kwa hivyo, wewe hata tukipiga kelele za aina gani, lakini madhali tunakosa mashirikiano Mheshimiwa katika hili hatuwezi kufanikiwa ni lazima katika hili wazee waone umuhimu wao, waone kwamba wana sababu ya watoto wao kuwasimamia katika misingi ambayo ni ya uadilifu zaidi.

Mhe. Spika, naomba kitu chengine, hili suala la *tuition* ni jambo muhimu mno, lakini Mhe. Waziri lipangie wakati. Kwa sababu mtoto mwari anapotoka kwao usiku saa moja akenda mpaka saa sita kusoma hiyo si *tuition* tena hiyo ni balaa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi naomba upange wakati na lazima *tuition* zifanyike katika maskuli. Unaweza kwenda skuli ukifika watu wamekaa tu ovyo kama hapo *Jamhuri Garden* na maeneo mengine tena wanawake na wanaume, angalia lililo baya zaidi, amekaa mwanamke na mwanamme mmoja mmoja tu.

Juzi nilikwenda Skuli ya Kiembesamaki usiku ninae mwanangu pale, nilipofika nikamkuta yule mwanangu yuko darasani na wenzake wengi tu wanasomeshwa na mwalimu fulani, lakini nikenda nikakuta kuna miti miti pale wamekaa wanafunzi kila mmoja na mwanamme, nikasema hii ndio *tuition* au nini tena? Kwa hivyo, mambo kama yale yanafanyika katika skuli.

Sasa naomba Mhe. Spika, watu wafuatiliwe waone zile waone, zile balaa bora zitokee huku mitaani kuliko kutokea skuli ni aibu.

Mhe. Spika: sawa naomba umalizie.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe. Spika, sawa, naomba nimalizie kwa kuheshimu wito wako. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria kikao cha Baraza kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, pia nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji wa Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa 2010/2011.

Mhe. Spika, nikianza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote. Wizara ya Elimu ni kati ya wizara moja ambayo inajitahidi kusimamia suala zima la elimu lakini pia

wenzetu hawa wamejitahidi sana katika kuhakikisha kwamba Waheshimiwa Wajumbe wanapokuwa na matatizo yao mbali mbali ukifika pale basi wanathamini kwa yale uliyoendea pale na kwa kweli wanatusaidia katika utekelezaji wa majukumu yetu katika majimbo.

Mhe. Spika, nianze na mchango wangu kwanza kwa kumkumbusha Mhe. Waziri kwamba, kuna Skuli ya Kinyasini ya Msingi ambayo alitembelea Mhe. Waziri Kiongozi na baadae kuahidi kuwa skuli ile itaezekwa. Lakini pia skuli ile ilipelekewa maombi kwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na akalikubali hilo ombi na tayari tathmini zimefanywa. Nilikuwa nazungumza naye muda mfupi akanambia kwamba ni vizuri pengine ulizungumze kwa sababu watendaji wetu watalisikia na najua watendaji hawa hawana tatizo.

Mkurugenzi Bi Khadija pale nafikiri ananijua vizuri na yeye ndiye anayesimamia haya katika mambo ya misaada ile nategemea kwamba msaada huo utakapokamilika basi skuli hii itaezekwa kama vile ambavyo wameahidi. Hilo la kwanza.

Lakini la pili Mhe. Spika, nataka nimuombe Mhe. Waziri kwa makusudi. Mimi nina skuli nyingi katika jimbo langu, lakini skuli tatu hizi zina sekondari, nazo ni Kinyasini, Gamba na Chaani. Mhe. Waziri tuna tatizo kubwa la kompyuta katika skuli hizi, sasa ningeomba angalau kompyuta moja moja wizara yako ikajitahidi kutusaidia katika kila skuli hizi nilizozitaja za sekondari ili na wanafunzi wetu nao waende na wakati katika masomo ambayoa tunajua ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia. Kwa hivyo, ombi hili Mhe. Waziri nalileta kwako kupitia watendaji wako nao walithamini kuona kwamba tunawataka msaada huo.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningetaka kulizungumza ni kuhusu ujenzi wa Vyuo vya Amali. Mimi naipongeza wizara kwa ujenzi huu wa vyuo vya amali. Kwa bahati nzuri Chuo cha Amali cha Mkokotoni kilipofunguliwa mimi mwenyewe nilikuwepo na tulitembelea tukaona vifaa mbali mbali ambavyo vimo. Inawezekana kama wajumbe wenzangu kuna baadhi ya mapungufu hayo ni mambo ya ufuatiliaji, sasa pale ambapo pana mapungufu basi ningemuomba Mhe. Waziri akaliona hilo kama wajumbe walivyopendekeza. Lakini mimi nashukuru katika hilo kwani hivi sasa limetusaidia sana. Tuna vijana wetu wengi ambao wako pale chuoni wanasoma badala ya kukaa mitaani pengine bila ya kazi za msingi.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulichangia pia nipongeze suala zima la ajira za walimu. Mhe. Waziri wa Elimu alituahidi kwamba atajitahidi kuondoa tatizo au kupunguza kama sikuondoa kabisa, walimu Mkoa wa Kaskazini. Naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Mkoa wa Kaskazini Unguja

kwamba, niwapongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kuwa wamejitahidi na vijana wetu wamepata nafasi hizo za kwenda kusoma.

Pale palipokuwa na matatizo hatukusita kwenda katika wizara yake na walitusaidia kwa nguvu zao zote kuona wale ambao walikuwa na tatizo pengine mtu hakuji-*address* vizuri na wizara ikawa haikuelewa huyu mtu kama ameomba, pengine anakaa wapi kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba, tunachotaka ni lazima mtu anaajiriwa basi awe anatoka Kaskazini. Hilo wamelifanya, kwa hiyo hatuna budi kuwashukuru kwa nguvu zetu zote. Mhe. Waziri ahsante sana pamoja na watendaji wote.

Jengine ambalo ningetaka kuzungumza ni kuhusu ujenzi wa Chuo Kikuu Tunguu (*SUZA*). Mhe. Spika, vile vile nataka nipongeze hili na kwa dhati kabisa kwamba, bila ya kuwa na majengo yanayofanana na vyuo pamoja na afisi za serikali tutakuwa tunajidanganya kwa sababu tunakwenda na wakati. Sawa kwa kuwa Mhe. Waziri ni mtu ambaye ameliona hilo mapema yeye mwenyewe kuona ana mahala pazuri pa kufanyia kazi lakini pia ameanza kujenga vyuo ambavyo vinakwenda na wakati basi tunashukuru.

Vile vile kazi hiyo inakwenda na Mhe. Waziri tunashukuru na tunakupongeza kwa hilo na ningeomba watendaji wako wasimamie vizuri ili tuone tunafika mahala ambapo tumekusudia.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumza ni kuhusu haya mabo ya magofu na mambo ya kale ambayo yako katika wizara yake Mhe. Waziri. Nataka nipongeze kwa hilo katika kushughulikia hili kwa sababu ni mambo ya kihistoria pia ni kielelezo kwa nchi yetu kwa wale wageni ambao wanakuja.

Lakini pia juzi nilikuwa namsikiliza kwa makini Mhe. Mtumwa Kheir Mbaraka alipokuwa akichangia. Alizungumzia kwamba kuna gofu la Chwaka kama sikosei, lile gofu lina kamati ambayo inashughulikia. Sasa wasi wasi wake Mhe. Mtumwa ni kwamba wale wajumbe wa kamati karibu wote ni watu wa familia moja kitu ambacho kimeshaanza kuleta matatizo kwa maoni yake kuwa kuna watu wameshaanza kuuza baadhi ya sehemu za gofu hilo. Sasa na mimi naomba kwa dhati kabisa Mhe. Waziri mwenyewe ulifuatilie uone kama kuna tatizo hilo basi linaondoka na hasa ukizingatia gofu hili kuwa liko Chwaka nako ni Mkoa wa Kusini Unguja ambapo Mhe. Waziri unatokea.

Jengine ambalo nataka kuzungumza ni kuhusu Elimu ya Mbadala na ya Watu Wazima. Mhe. Spika, sina budi kutoa shukurani zangu za dhatui katika hili, lakini pia kupongeza kwamba imeleta tija kubwa. Mhe. Waziri utakumbuka ulipofanya ziara katika Skuli ya Gamba ambayo iko katika jimbo langu.

Ulioneshwa vijana ambao tayari wameshaacha skuli lakini hivi sasa wako pale skuli na wanasoma.

Mhe. Spika, vijana wale kwa kweli ni wengi hivyo kitendo hiki cha kuanzisha skuli mbadala kwa wale ambao walitoroka skuli kwa njia moja au nyengine, kitaleta faida kubwa kwa vijana wetu kuwaondoa pale ambapo walishapoteza mwelekeo na kuwarudisha katiak mwelekeo sahihi. Mhe. Spika, tokea zamani, lakini sasa hivi lazima watoto wetu tuhakikishe wanasoma. Bila ya kusoma hutokuwa na maisha mema huko unakokwenda.

Suala la Elimu ya Watu Wazima. Suala hili nalo vile vile nataka nipongeze wizara. Kwa sababu tunawaona wazee wetu pamoja na watu wako katika rika zetu na wa chini yetu ambao hawakupata nafasi ya kwenda skuli basi wanapita katika kwenda kusoma elimu ya watu wazima na wanajitahidi. Kwa hivyo, tunaomba hili liendelezwe vizuri kama mnavyoliendeleza msichoke kuona kwamba tunafuta ujinga wa kutojua kusoma na kuandika.

Mhe. Spika, katika hili ningetaka nitoe mfano mmoja hai. Nina jirani yangu anaitwa Mzee Issa Hakimu Issa, yeye ni muajiriwa wa Idara ya Majenzi na ni Afisa wa Majenzi katika Mkoa wetu wa Kaskazini. Kwa bahati mbaya ndugu Issa hakupata nafasi ya kwenda skuli, lakini pamoja na kuwa hakupata nafasi hiyo yeye mwenyewe binafsi amejiendeleza kiasi ambacho Mhe. Spika, huwezi kuamini. Ndugu Issa hivi sasa ana uwezo wa kufanya shughuli zake zote kielimu tena huwezi kuamini kwamba huyu hakupita darasani. Sasa hayo ni mafanikio makubwa ya wizara yako Mhe. Waziri kwa hivyo tunakupongeza katika hilo.

Jengine Mhe. Spika, ni suala la elimu ya Vyuo vya *Qur-an* kwamba vile vile Mhe. Waziri analichukua katika wizara yake na kulisaidia kwa nguvu zake zote. Na hili nataka nikiri kwamba Mhe. Waziri amefanya ziara katika Jimbo langu la Chaani, kwa bahati nzuri ametembelea katika maeneo karibu yote, amejionea mwenyewe maendeleo ya elimu ya qurani lakini pia ameona yale ambayo yanamuhusu moja kwa moja ya skuli.

Katika hili kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri ametusaidia sana katika jimbo leto kwenye harakati hizi za elimu hasa ukizingatia kwamba baadhi ya shehia hakukuwa na skuli. Kwa mfano, Shehia ya Bandamaji haikuwa na skuli, lakini leo tuna skuli na vijana wanasoma pale lakini chanzo na sababu za kuwepo skuli hii ni ziara ya Mhe. Waziri wakati tulipokuja kumuomba kutembelea jimbo letu na akatembelea, bahati nzuri alitembelea Chuo cha Maalim Sharifu pale Bandamaji. Chuo kile kilikuwa na watoto wengi kiasi ambacho huwezi kuamini.

Lakini bahati mbaya kabisa Mhe. Waziri alipokuwa akiwauliza maswali wewe unasoma skuli? Kila mmoja akawa hasomi na umri wao bado ni wa kuruhusu kusoma. Kwa kweli pale pale Mhe. Waziri akaanza kutoa mchango wake akasema kwa vyovyote tafuteni eneo na wizara itasaidia kwa hali na mali. Skuli sasa hivi tunayo Mhe. Spika, na bahati nzuri *TASAF* walikuja pale tukaanza nao lakini sasa hivi tumeimarisha kuongeza mabanda. Kwa hivyo, tunakushukuru sana katika kuhakikisha kwamba unalitekeleza vizuri jukumu lako la kuondoa ujinga.

Mhe. Spika, pia Mhe. Waziri amevisaidia vyuo katika ziara yake hiyo ya kwanza ambayo tumefanya hivi karibuni. Mhe. Spika, nataka nirejee tena, nilikuwa namzungumza sana Mhe. Waziri kwamba amekuwa akitusaidia sana. Mhe. Spika, katika hili nataka nimwambie Mhe. Waziri ambapo pia nimemueleza, lakini nataka nitumie nafasi yako kupitia Baraza lako tukufu kwamba anapokabidhi kitu chochote ambacho kinatokana na wizara yake lazima atushirikishe sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mimi naona uchungu sana kuona kwamba Mhe. Waziri anajitahidi lakini wale anaowakabidhi dhamana kwenda kukabidhi mahala hawasemi ipasavyo. Mtu mwengine anakwenda kujipendelea mwenyewe kwamba kitu hichi anakipeleka yeye wakati Mhe. Waziri amekabidhi kitu kile kwa niaba ya jimbo kutekeleza ahadi zake.

Mhe. Spika, nimemueleza Mhe. Waziri hapa na nashukuru kaniahidi kwamba kesho niwapeleke wajumbe wa chuo cha Maalim Kali kule Moga ili aweze kujua ni kweli kwamba hawajawahi kupata huo msaada ambao anaupeleka. Kwa sababu mimi wamekuja kunilalamikia nikawaambia nitamwambia Mhe. Waziri, lakini kwa kweli kuna baadhi ya viongozi wanaharibu. Ni vizuri unapopewa kitu ukikabidhi kama ulivyopewa. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ama waziri mwengine yeyote, ama Mhe. Rais, au Mkuu wa Mkoa wanatoa kutukabidhi sisi viongozi katika majimbo yetu basi tukifika tuseme msaada huu aliahidi Mhe. Haji Omar Kheir.

Mhe. Spika, kwa kumalizia hotuba yangu niseme kwamba mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chaani tunaikubali hotuba ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja na apewe mafungu yote ambayo ameomba ili kutekeleza vizuri majukumu yake. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na ninazo pointi zangu nne naomba univumilie nizimalize ili niweze kumchangia Mhe. Haroun Ali Suleiman rais tunayemtarajia *inshaallah* atakuwa Zanzibar.

Mhe. Spika, ukurasa wa 38 hotuba ya Mhe. Waziri imesifu sana maendeleo ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar *(SUZA).* Lakini nilipochunguza zaidi nimeona kwamba wamesifu zaidi kwenye idadi ya ongezeko la wanafunzi. Sasa Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametuonesha jinsi kiwango cha wanafunzi kinavyoendelea lakini hakufafanua zaidi *quality* ya wanafunzi wa *SUZA* ilivyo.

Mhe. Spika, kwa mtazamo wangu hatuwezi kuwa na *quality education* bila ya kuwa na *quality laboratory*. Sasa bado naungana na wenzangu kwamba hatuwezi kuwa na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar chenye ufanisi bila ya kuwa na maabara ya kisasa iliyotengeneza. Kwa msingi huo Mhe. Spika, nakataa kata kata kwamba mpango wa serikali wa kuipangia fedha kidogo *SUZA* kwa maabara yake kwa kweli haikubaliki. Namuomba Mhe. Waziri alizingatie hili kwa kuongeza uwezo wa kifedha kwa matumizi ya maabara ya *SUZA* ili wanafunzi wetu waendelee kubakia hapo badala ya kwenda Tanzania Bara.

Mhe. Spika, pia *quality education* itapatikana kwa maslahi ya walimu. *SUZA* ina wakufunzi wazuri, ina maprofesa lakini kwa kweli maslahi ya walimu wetu ni madogo na kwa hivyo tusitarajie kiwango kikubwa cha ufanisi kwa wanafunzi ikiwa wasomi wetu hawa wataendelea kupata maslahi madogo.

Mhe. Spika, maprofesa mbali mbali wanapostaafu utawaona wanaendelea kufanya biashara za kitoto. Si malengo ya kuwafanya wasomi wetu wale waishi katika maisha duni lakini ni kutokana na maslahi madogo ambayo wasomi hawa wanapatiwa.

Mhe. Spika, hapo hapo *SUZA*, niseme kwamba tumekuwa na kilio cha kuhoji kwa nini serikali haitumii tafiti za *SUZA*, badala yake serikali wanatumia tafiti za nje ya Zanzibar wakati *SUZA* ndio Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar. Sasa ushauri wangu Mhe. Spika, ni kwamba serikali ijenge utamaduni wa kuwatumia *SUZA* kufanya tafiti mbali mbali na kutumia tafiti zao kwa maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Zanzibar tumekuwa na upungufu wa walimu wa sayansi na *SUZA* wameweka mkakati maalum kwa ajili ya kuongeza walimu wa sayansi hapa Zanzibar. Mhe. Spika, ukweli ulivyo si kwamba tuna upungufu wa walimu wa sayansi, lakini tatizo ni kuwaenzi walimu wa sayansi.

Mhe. Spika, tulipoangalia mtandao juzi niwapongeze *SUZA* nimeiona *press release* yao ambayo *SUZA* wamemtoa mtaalam wao kwenye wataalam mia bora wa dunia. Dk. Moh'd Shehe ni mtaalam mmoja miongoni mwa wataalam mia wa dunia ambao kituo cha *IDC* kimemchagua kama ni mtaalam mmoja wa dunia. Huyu ni Mzanzibari, mdogo sana na ni mwalimu wa somo la *Chemistry* pale *SUZA*. Sasa mtu huyu kama hatukumhifadhi maana yake ni kusema

kwamba atakimbia, tukimpa maslahi madogo usimtarajie huyu kwamba atakufa Zanzibar, atakimbia na atakuwa tayari kuondoka Zanzibar kwenda kutafuta pahala pakufariki.

Mhe. Spika, kwenye uchaguzi huo wa *IDC* Makerere nchini Uganda pia tumebahatika Profesa Iddi Sarai, huyu ni Mmakunduchi kwa Mpemba amechaguliwa kuwa ni profesa mia bora wa dunia mwaka huu. Ninahakika huyu asingependa kuondoka Zanzibar, asingependa kuondoka Makunduchi wala Mkoani, lakini ameondoka kwa sababu maslahi madogo.

Mhe. Spika, pia tukiangalia mbali ya hilo kwamba yeye ni profesa bora kati ya mia lakini ameichangia Makerere bilioni moja za Uganda kwa mwaka 2010. Yeye ameandika kutafuta ufadhili, kutafuta misaada duniani chuo kimeingiziwa bilioni moja za Uganda kama mchango wa msomi huyu. Sasa fedha hii ingebakia Zanzibar akahangaika maana yake fedha hii ingeingia kwenye mfuko wa serikali, ingeingia kwenye mfuko wa chuo cha *SUZA*.

Mhe. Spika, hii inaonesha jinsi gani ambavyo Wazanzibari wanavyowapoteza wasomi kutokana na maslahi duni. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri azingatie sana mchango wa wasomi, azingatie sana jinsi ya kuwaenzi wasomi, ili kilio cha upungufu wa wasomi wetu hapa Zanzibar kiweze kuondoka.

Mhe. Spika, jengine ni Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume. Mimi nipongeze uamuzi wa serikali kwa kuanzisha taasisi hii, lakini niseme tu kwamba umuhimu wa taasisi hii utabakia huko huko kwenye mtu mmoja mmoja, kwenye nchi na utabakia huko huko kwenye dunia. Mhe. Spika, hadi leo Mhe. Waziri anatwambia amejaribu kutoa mafunzo ya walimu wasiozidi ishirini wa kompyuta, wakati maskuli mengi ya Zanzibar hayana kompyuta. Lakini tumeingia kwenye soko la ajira la Afrika Mashariki tukiwa tuna watu wachache sana wa utaalam wa kompyuta.

Mhe. Spika, tukiangalia nchi kama Kenya wao bajeti hii ya juzi wameamua kila jimbo kupeleka kompyuta mia tatu, nchi ya Rwanda wameamua kila mwanafunzi awe na kompyuta moja. Sasa hawa ni watu ambao kesho kutwa tunaingia kwenye soko la ajira ya Afrika Mashariki tujiulize watatuacha wapi. Ikiwa kila mwanafunzi wa Rwanda ana kompyuta moja na Kenya kila jimbo moja kompyuta mia tatu, lakini Zanzibar walimu ishirini kwa kompyuta ndio waliofundishwa. Tuangalie tuko wapi kwenye soko la ajira la Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, nadhani serikali ingejipiga zaidi na kuona kwamba kuna umuhimu wa kuanzisha taaluma hii ya sayansi na teknolojia hapa Zanzibar na sio kwa maeneo lakini kwa kila mwanafunzi mmoja mmoja.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningelichangia kwa ufupi ni maslahi ya walimu kama ambavyo wenzangu wamezungumza. Mhe. Spika, niipongeze serikali kwa kuamua kufanya marekebisho ya mishahara ya walimu lakini bado malalamiko ya walimu yanajitokeza. Kuna walimu ambao walitegemea kupata nyongeza ya shilingi 40,000 lakini wamekosa. Suala hili ni kwamba labda kuna tatizo la kiufundi lililojitokeza. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri na watendaji wake waangalie tatizo gani lililojitokeza ambapo walimu waliostahiki kupata maslahi zaidi wamepata maslahi madogo.

Lakini pia walimu wetu wengi wanahoji vigezo gani ambavyo serikali imetumia kuongeza nyongeza hizi za maslahi ya walimu. Kwa sababu wapo walimu wenye kiwango kimoja cha elimu na umri sawa sawa lakini maslahi yao yamekuwa ni madogo. Sasa kigezo ambacho serikali imetumia walimu wengi hawajakijua, kwa hivyo inahitaji kuelimisha ili kuondosha malalamiko ya walimu.

Mhe. Spika, la mwisho kwa upande wangu ni ombi maalum. Mhe. Spika, tuna tatizo eneo la Mahuduthi Kengeja. Mahuduthi ni baina ya Kengeja na Mtambile, kutoka Mtambile mpaka Kengeja ni karibu kilomita saba na nusu. Lakini pale Mahuduthi kuna wanafunzi ambao wanasoma wengine Mtambile na wengine Kengeja. Mhe. Spika, jinsi wanafunzi wale wanavyopata tabu basi huwa nawaonea huruma siku za mvua. Kwa hivyo, ushauri wangu kwa Mhe. Waziri wajipange kama wizara kuanzisha skuli ya msingi pale Mahuduthi, ili kuwapunguzia mzigo wa usafiri wanafunzi wa Mahuduthi wanaokwenda Kengeja na Mwambe.

Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Waziri juzi alituomba tusimchoshe na kwa kuwa mimi binafsi kama mwalimu wangu namheshimu sana na namtakia kheri. Mhe. Spika, naomba nifikie hapo na naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pia natumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa tuko hai na tuko katika hali ya furaha sote tukichangia hotuba ya rais mtarajiwa Mhe. Haroun Ali Suleiman.

Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa ujasiri wake kwa kujitolea kuchukua fomu na kuomba nafasi hiyo. Namtakia kila la kheri katika mbio zake hizo.

Mhe. Spika, pili namshukuru yeye binafsi pamoja na jopo zima la wataalam wa wizara yake kwa namna ya kitabu alivyokitengeneza ambacho kimejumuisha maendeleo ya miaka kumi ya awamu ya sita kwenye shughuli za elimu. Pia wametoa data zote ambazo zitatusaidia sisi katika kuchangia hotuba hii na

kuona kwamba maendeleo gani ya elimu yamepatikana kwa muda huu wa miaka kumi katika awamu ya sita.

Mhe. Spika, vile vile nampongeza sana Mhe. Waziri kutokana na kwamba ni wizara chache tu ambapo yeye akiwa wa kwanza kuonesha mfano mzuri wa kujenga jengo zuri na safi likiwa nje ya Mji Mkongwe. Ukiingia ndani utafikiri ni jengo la Ulaya sio la Zanzibar, zile ofisi tulizozizoea sio ofisi kama ile.

Mhe. Spika, halikadhalika, nampongeza kutokana na sera yake ya elimu ya mwaka 2006 ambapo kweli ikitimizwa inaweza ikaleta manufaa makubwa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, vile vile nampongeza Mhe. Waziri kutokana na rasimu yake ya sheria ambayo imo katika mchakato na kwa kweli tunaomba ifike katika Baraza hili ili ipate baraka zake na iweze kuweka hiyo sera katika ulingo mzuri.

Mhe. Spika, pia nampongeza sana kwa kuweza kufanya Chuo cha Karume kuwa ni Chuo cha Sayansi na Teknolojia na jitihada za wizara hii katika suala zima la elimu ya maandalizi, elimu mbadala na elimu ya chekechea.

Mhe. Spika, vile vile nampongeza kwa kutayarisha angalau kuwa na kambi za sayansi za kushughulikia wale wanawake ambao wapende somo la hisabati na sayansi.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuchangia kama hivi ifuatavyo. Mhe. Spika, Zanzibar kama ni kisiwa na uchumi wake ni wa kisiwa. Katika kujenga uchumi huu tunatakiwa tuwe na mambo mbali mbali ambayo yataweza kutusaidia kukuza uchumi wetu, moja ni kuwa na *quality education*. Kwa kweli hili ni suala muhimu sana kwa sababu sisi tunataka kutoa huduma, sasa lazima tuwe na elimu ya juu kama si hivyo tutashindwa kutoa huduma bora. Kwa sababu hatuna nyenzo nyengine isipokuwa kutoa huduma za utalii, biashara, uzalishaji, tunatakiwa tuwe na watu wasomi.

Mhe. Spika, tukiangalia ukurasa wa 4 hadi wa 5 wa kitabu chetu hichi tumeelezwa kwa vizuri kabisa jinsi gani wanafunzi walivyokuwa *enroled* katika miaka hiyo kumi na vile vile katika ngazi ya msingi. Katika jadweli (b) na (c) ukurasa wa 5 utakuta pale ndio penye masuala yote ya kidato cha pili. Lakini kama unakwenda mbele ukurasa wa 5 kifungu cha 17 kinasema “Uwiano wa wanafunzi na walimu hupungua kutoka wastani wa wanafunzi 33 hadi 28 kwa mwalimu mmoja”.

Hapa mimi nimeshtuka sana, nikitembelea madarasa nakuta yana wanafunzi wengi sana lakini mwalimu mmoja. Nimetembelea madarasa mengi nimeona

yana wanafunzi zaidi ya 70 mwalimu mmoja. Baadhi ya wakati walimu wawili darasa moja wamejaa wanafunzi hata hawasikilizani. Sasa husemi kwamba mwaka 2010 kufikia katika juhudi hii kuona kwamba wanafunzi 33 hadi 28 kwa mwalimu mmoja. Naomba nipate ufafanuzi wake kwa sababu naona madarasa bado yamejazana na mwalimu ni mmoja katika darasa lenye wanafunzi wengi sana.

Mhe. Spika, jengine linalonishtua mimi ni kwamba wanafunzi wanaoandikwa ni wengi, ukiangalia hapa katika skuli ya maandalizi tuna wanafunzi 29,739 kwa mwaka 2010. Ukenda skuli ya msingi mwaka 2010 kuna 2,026,812 na katika jadweli © kuna hiyo ya kidato cha pili 285,695. Ukiangalia wimbi hili la wanafunzi wanaoongezeka mwaka hadi mwaka katika *enrolment which is good*, lakini je, wizara yetu imejitayarisha vipi. Naona huku mbele kuna mpango wa miaka minane kwa muda mrefu na muda mfupi ni miaka mitatu, lakini sijaona kwamba kuna malengo maalum ya kuweza kudhibiti hali hii. Wanafunzi wote hawa wanataka washughulikiwe na tupate hiyo *quality education.*

Tukenda katika ukurasa wa 6 na 7 utakuta katika kidato cha pili wanafunzi waliofeli mwaka 2009/2010 ni 9,740 na mwaka 2008 vile vile waliofeli ni 13,770. Ukiangalia hawa wote hizo ni *drop out* ambazo wakitoka pale tayari ni mzigo kwa taifa. Watafanya kazi gani, watakuwa hawa jamaa ni *trendable* au vipi.

Tukiangalia kwa mfano Uchina wanaposema kuna *cheap labour* sio kwamba unakwenda unakuta watu *very cheap* kuwaajiri hapana. Wale ni *skilled cheap labour*, ni *trendable cheap labour*. Sasa ikiwa wanafunzi wanatoka *in this volume* na wamefeli, hawa sio rahisi kuwa-*trend*, ni vigumu kuwa-*trend* na hiyo *trend* ni kubwa sana inatisha.

Ukiangalia pia katika jadweli hilo la ukurasa wa 7 utakuta kwamba wanafunzi ambao wanapata *division I* ni 40 kidato cha nne na wanaofaulu katika *division II* ni 266. Hali hii pia si ya kujivunia wala kufurahisha, bado hatujapata kitu kinachoitwa *quality education*.

Mhe. Spika, vile vile ukiangalia mkumbo wa chini huko ni mkubwa sana, wanafunzi 21,000, 29,000. Ukija katika kidato cha 4 wanafunzi 8,000, wanafunzi wote hawa wengine wamekwenda wapi na ni mzigo wa serikali. Vipi wanafunzi hawa wataweza kuendelezwa katika kulijenga taifa au watakuwa ni wala unga au wazururaji. Masuala haya ni muhimu sana kuyazingatia.

Mhe. Spika, ukenda mbele zaidi utakuta kwamba katika mwaka 2009 waliofaulu katika *division I* na *II* ambao wanaweza kwenda chuo kikuu ni hao 206, waliobakia wote wale wako chini wanagaragara na wengine kabisa 659 hatujui watakwenda wapi. Huu pia ni mzigo kwa serikali, ni mzigo kwa nchi. Katika kidato cha 6 utakuta katika wanafunzi hawa 368 wamefeli, lakini utakuta 230 ndio wamepata daraja la kwanza na daraja la pili. Hawa ndio tunatarajia waende wakasome zaidi waje kuwa walimu wetu watusomeshe katika vyuo vikuu vya Zanzibar.

Mhe. Spika, ukiangalia vyuo vya Zanzibar vinakua, sasa hivi tuna vyuo vitatu na vitaongezeka zaidi na zaidi. Mhe. Spika, mimi nimo katika ile Bodi ya Ushauri ya Chuo Kikuu cha Tunguu na Chuo cha Elimu Chukwani. Matatizo tunayoyakabili kule kwa kweli hatupati wahadhiri na wakufunzi ambao wana sifa za kuja kufundisha kutoka Zanzibar lazima uchukue kutoka nje. Kutoka Zanzibar tunataka *first credit* lakini kwa kweli hakuna. Kwa hivyo, ipo haja ya kuweka msimamo kwamba tutawasomesha vijana wetu waweze kuja kuokoa jahazi.

Hivi tunavyokwenda huko mbele kuna hatari ya kuja kukwama zaidi. Ningeomba mkazo uwekwe kwamba ili tuweze kuendelea Zanzibar tusidanganyane, tunahitaji watu wawe na elimu ya sayansi na teknolojia. Ikiwa hatuna watu wenye elimu ya sayansi na teknolojia hatuwezi kabisa kuendelea kama kisiwa tukilinganisha na visiwa vyengine vya Singapore, Mauritius na vyenginevyo. Kwa hivyo, masuala ya sayansi na teknolojia yataweza kutuokoa kiuchumi hapa Zanzibar. Mhe. Spika, ningeomba Mhe. Waziri suala hili alitilie maanani na atueleze ana utaratibu gani ambao ataautumia.

Mhe. Spika, ukurasa wa 13 Chuo cha Karume kimefanywa ni chuo cha sayansi na teknolojia. La kushangaza na la kusikitisha sana kwamba katika mwaka uliopita kilitengewa kupewa shilingi milioni 650 ambako ndio kwenye sayansi na teknolojia, elimu ya maandalizi wamepewa shilingi milioni 800. Walizopewa hasa katika hizo shilingi milioni 650 ni shilingi milioni 130 tu. Hali kama hii haioneshi sura nzuri ya kuweza kutusaidia sisi kufika pahala tunapopataka.

Mhe. Spika, hichi chuo tumekifanya ni Chuo cha Sayansi na Teknolojia tunakipatia shilingi milioni 130 tu katika bajeti yake ya mwaka uliopita kutoka shilingi milioni 650 halafu yake tunatarajia nchi yetu itapata uokovu. Haiwezekani kabisa kwa sababu hiyo sayansi na teknolojia itakayotuokoa katika nchi hii hatuwezi kuipata kwa kutoa bajeti hii ya shilingi milioni 130 katika chuo ambacho tumekipa hadhi kama hiyo hakilingani kabisa.

Mhe. Spika, hata mwaka huu ukiangalia bajeti yake iliyowekewa ni shilingi milioni 500 tu ambayo itakuwa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbweni na Chuo cha Ufundi kule Kengeja Pemba. Naamini pia hizi hawatopewa, ikiwa mwaka jana wamepewa shilingi milioni 130, mwaka huu labda watapewa milioni 100. Nasema kwamba imezidi kupunguzwa bajeti kutoka shilingi milioni 650 kuja shilingi milioni 500. Hii haileti sura nzuri ikiwa kweli tunataka taifa hili liendelee. Sayansi na teknolojia ndio ukombozi wetu tusidanganyane.

Mhe. Spika, ukurasa wa 14 kifungu cha 37 Mradi wa Upanuzi wa Uimarishaji wa Huduma za Maktaba. Katika mwaka uliopita kulikuwa na maktaba ya Pemba, lakini naona ukiangalia na mwaka huu vile vile ukurasa wa 19 kuna kuanza kazi za ujenzi wa tawi la maktaba huko Pemba. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha hapa atupe taarifa hii maktaba ya Pemba imekosa nini.

Mhe. Spika, ukurasa wa 22 habari ya mambo ya kale. Mhe. Spika, hili naona mimi ni mzigo mkubwa sana umepewa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Spika, Wizara ya Elimu imepewa majukumu ya kutusomeshea watoto wetu na hii ni kazi kubwa sana, naamini kwamba kazi hii si kazi nyepesi.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri yeye mwenyewe alikuwa mwalimu na kafanya kazi Wizara ya Elimu kwa muda mrefu sana, katumia ujuzi wake wote, hekima zake zote na jitihada zake zote za ualimu tumefika hapa. Halafu tumekwenda kumpa mzigo mwengine mkubwa kama huu ambao kwa kweli hizi historia na hifadhi za mambo ya kale ni masuala muhimu sana katika utalii na ni moja ya nyenzo za kuingiza mapato nchini kwetu. Kwenda kuitwika mzigo huu Wizara ya Elimu kwa kweli mimi nahisi ni mzigo mkubwa sana unaielemea wizara, ningeomba suala hili lingehamishwa huku likapelekwa sehemu nyengine ili kuwapunguzia uzito wake. Suala hili ni zito sana, linataka fedha nyingi sana na ni muhimu sana katika nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine ukurasa wa 29 ni masuala ya tovuti. Mhe. Spika, hapa imeelezwa vizuri lakini nimuombe Mhe. Waziri anieleze wizara yake ina *web site*, kama ina *web site* atupatie hiyo *web site* yake iko sehemu gani. Hilo ni suala muhimu sana la kuonesha mfano kwa mawizara yote yawe na tovuti yake ambayo kila mtu aweze kuingia na akapata hizo *information*.

Mhe. Spika, hivi sasa ukifungua web site ya Bunge la Mauritius unapata bajeti zote za mawizara ya Mauritius na *full detail* zipo. Sasa Mhe. Spika, tungemuomba Mhe. Waziri kama wanayo watueleze kwa sababu ni mfano mzuri sana wa kuanzia hapo.

Mhe. Spika, ukurasa wa 30 na 31 nampongeza Mhe. Waziri kuhusiana na masuala ya vyuo vya kurani angalau kuwa kuna takwimu. Lakini isiwe kwenda kule kupata hizi data na kutoa *information* hiyo *just* kutokana na msukumo tu wa wahisani kwamba wanafunzi kule wanachapwa sana, tumepata ufumbuzi wanafunzi wasichapwe, yakaishia hapo. Ningeomba wizara ichukue hatua ya kusaidia vyuo hivyo.

Ukiangalia walimu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni 10,000 na walimu wa vyuo vya kurani ni 8,057 karibu walingane. Mhe. Spika, ningeomba Mhe. Waziri asitumie fursa hii *just* ya kwenda kuwaridhisha wahisani, lakini kuona kwamba haya ni mambo ya msingi na kuwashughulikia ili wanafunzi wapate kudhibitiwa kwa upande wa vyuoni na upande wa maskuli. Hapo patakuwa na uwiano mzuri wa kutoa elimu itakayofaa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, ukurasa wa 36 na 37 ambao umezungumzia sana juu ya suala la sayansi na teknolojia. Mhe. Spika, mwaka jana ilitengwa shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi ambao wanakwenda katika elimu ya juu ya sayansi na teknolojia na ndio tunaotaka kuweza kusomesha vyuo vyetu. Kwa bahati mbaya fedha iliyotoka Wizara ya Fedha ni shilingi bilioni 1.5 tu, kwa kweli hichi ni kitu kidogo sana ukilinganisha na ile idadi ya wanafunzi waliopo, yaani ni asilimia 65.2 tu.

Mhe. Spika, naomba Wizara ya Fedha suala hili lisifumbie macho wala lisifanye muhali, litoe fedha za kutosha ili wanafunzi wakopeshwe, tupate wanafunzi ambao wataweza kuja kuokoa jahazi. Zanzibar kitakachotuokoa ni *quality education*, lakini haipatikani kama tutakuwa hatusomeshi watu wetu. Shilingi bilioni 2.3 ni kiwango kidogo sana, mwaka 2010/2011 imewekwa makisio ya bilioni 2.5. Pia ni kidogo sana lakini angalau bilioni 2.5 Mhe. Waziri wa Fedha azipeleke Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili wanafunzi hawa walipiwe kwa wakati.

Mhe. Spika, mimi niko vyuoni kule naona wanafunzi wanavyo-suffer, ikiwa pesa hazijatiwa tunaanza kuwazuia zuia wasifanye mtihani, wasipewe matokeo na mambo mengine.

Mhe. Spika, kwa kweli hili suala ni muhimu sana. Sayansi na teknolojia ndio ufumbuzi wa kweli wa visiwa hivi. Elimu nyengine hizi tunastahia, lakini tukitaka tuendelee na tukitaka kupata faida kubwa katika nchi hii, vijana wetu wawe na sayansi na teknolojia *as a basic education* ya nchi yetu. Mhe. Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi, ahsante sana.

Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe.

Spika, kama kawaida yangu dakika zangu ni tano tu, nitazungumza yale yaliyokuwa ya muhimu na ninayoyajua zaidi.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 51 Program za Wanawake. Nanukuu kidogo. "Mhe. Spika, juhudi za kuwaendeleza wana kisomo wanawake pamoja na kuwahamasisha kujiunga pamoja katika vikundi vya uzalishaji mali ziendelezwe".

Mhe. Spika, hapa nampongeza Mhe. Waziri, kwa sababu kitu kikubwa sasa hivi kinachosababisha wanawake vijijini hasa wanaojiunga na vikundi vya ushirika kutokana na kutokuwa na elimu. Elimu ni ndogo Mhe. Spika, wanaweza kugombana hata huo ushirika wenyewe ikawa hauendelei kutokana na kutokuwa na elimu. Suala hili namuomba Mhe. Waziri aliendeleze zaidi vijijini, kwa sababu vijijini ndiko kunakotokea wazalishaji mali kwenye vikundi vya ushirika kama ufugaji wa kuku, ufugaji wa ng'ombe, kilimo na mengine. Hili Mhe. Spika, ni tatizo kubwa sana kutokana na elimu yaani kutokujua elimu ya vikundi hasa kwenye kuweka kumbukumbu hawajui kabisa. Suala hili namuomba Mhe. Waziri alifuatilie zaidi.

Mhe. Spikia, katika ukurasa wa 55 unahusu mambo ya kale. Mhe. Spika, kule Kangani liko gofu, hilo nalikumbuka tangu mimi sijazaliwa, nimezaliwa na nimekua bado naliona hivyo hivyo. Mhe. Waziri gofu hilo linaitwa Kwa Shariff na umaarufu wake ni Shariff Jini. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri gofu hili alitembelee ili nalo liingizwe katika hizo programu zao.

Mhe. Spika, vile vile mimi na Kamati yangu ya Fedha na Uchumi tulitembelea katika kijiji cha Tumbe, tulipofika huko wananchi wale walitutaka tukaangalie magofu, wakaatuambia yapo magofu ambayo mpaka hivi sasa hayatambulikani na wala hayajulikani kabisa.

Mhe. Spika, kwa mfano kuna vyuo vya *Qur-an* vinasemekana vipo ambavyo vilizama na mpaka sasa hivi havijajulikan. Pia kuna sehemu nyengine ambayo ilifukuka na inasemekana kuwa ilikuwa ni sehemu ambayo walikuwa wakihifadhiwa watu waliokuwa wakifanya makosa mbali mbali na hii nayo inasemekana kuwa ipo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba suala hili ushirikiane na wananchi pamoja na wazee wa Tumbe, ili kuyafuatilia na kuyafanyia utafiti ni vitu gani hasa vilivyokuwa havijaonekana na kitu gani kilichosababisha kujifukia kwa vyuo kama hivyo.

Mhe. Spika, nije kwenye walimu ambao wamemaliza masomo yao na hawajaajiriwa. Mhe. Spika, wapo walimu ambao wamemaliza masomo yao tangu mwaka 2007/2008. Mhe. Spika, walimu hawa bado mpaka hivi leo hawajaajiriwa. Hususan ukizingatia Mhe. Waziri yapo maskuli ambayo hayana

walimu wa kutosha. Je, Mhe. Waziri suala hili utalichukulia hatua gani ya kuwaajiri walimu hawa ambao wamemaliza masomo yao.

Mhe. Spika, nije kwa wanafunzi ambao wamefutiwa masomo yao. Mhe. Waziri hili ni suala zito na ni gumu sana. Ukiangalia hasa mtoto kusoma toka darasa la kwanza mpaka kufikia darasa la kumi na mbili na halafu mtoto yule akafutiwa masomo yake yote, aangaliwi angalau somo ambalo kalikopia ndio akafutiwa moja, lakini masomo yote Mhe. Spika, akafutiwa mtoto kama yule. Je, huoni kwamba huko ni kummaliza kisaikolojia mtoto huyu na utamweka vipi ili arudi katika elimu yake, ili aweze kujiendeleza tena. Mhe. Spika, naomba nimalizie hapa. Ahsante.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu. Nina mambo mengi lakini nitajitahidi kwa pale nitakapojaaliwa kuchangia.

Mhe. Spika, kwanza nichukuwe nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi, nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri waliyoifanya. Ninawatakia heri wote, kuanzia wewe Mhe. Spika, Mhe. Waziri, Wajumbe wa Baraza lako kila mmoja, pamoja na watendaji nao wana mambo yao mbali mbali Mhe. Mwenyezi Mungu kila mmoja ampe lenye heri. Lakini ningemuomba Mhe. Waziri asiudharau wito wa Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi wa kwenda kulitembelea hilo gofu. Ikiwezekana aende kabla ya uteuzi inaweza ikasaidia. *(Makofi/Vicheko)*

Mhe. Spika, nikitoka hapo moja kwa moja niende katika ukurasa wa 30, hapa nimekusudia kuzungumzia kuhusu mambo haya ya elimu ya madrasa na vyuo vya amali. Wenzangu wameshazungumza vitu vingi sana Mhe. Spika, lakini mimi nilikuwa napenda kusisitiza, kama kifungu cha 77 kinasema kwamba wizara ilitembelea vyuo na inaonekana kutokana na msukumo pengine wa wafadhili. Kwa sababu *specifically* wamekwenda pale kuelezea mambo ya bakora na vitu kama hivyo.

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye suala hili la mambo ya elimu ya madrasa na vyuo vya *Qur-an*. Mhe. Spika, inaonekana kwamba kwa mujibu wa hiki kifungu cha 77 ni kwamba hiyo ziara ilifanyika labda kwa kukidhi mahitaji pengine ya wahisani. Kwa sababu iko sheria inayohusiana na masuala haya ya mambo ya watoto kuchapwa ambapo bado wengi wa wajumbe wako pamoja na waumini wa Kiislamu hatujakubaliana nayo na itahitaji ifanyiwe marekebisho makubwa kulingana na hali halisi ya desturi zetu, utamaduni wetu pamoja na dini yetu.

Sasa katika hili Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri isiwe ni suala la bakora tu, lakini jambo ambalo nadhani bakora ni lazima kidogo, kwa sababu ile ni elimu na kwa mujibu wa maadili yetu ni lazima ili mtoto awe makini kuweza kusikiliza maagizo ikiwa ni ya elimu na ikiwa ni mambo mengine basi ni lazima umuweke katika mstari kwa kupitia mambo kama hayo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ninaloomba kwa wizara hapa ni kwamba hawa walimu wa madrasa basi tusiwatambuwe tu kuwa wako wangapi, lakini wizara ichukuwe jukumu na ifanye utaratibu wa kuona jinsi gani ya kuwasaidia.

Pia sio kuwasaidia tu, lakini kuwawezesha au kuwaendeleza kielimu. Mhe. Spika, inazungumzwa sayansi kwamba ni muhimu sana kuliko mambo mengine. Lakini mimi nataka nikuhakikishie kwamba sayansi yote imo ndani ya *Qur-an*, kama tulivyoambiwa ni kitabu ambacho ni *laa raiba fihi,* yaani hakina shaka, hakina kasoro wala hakina doa. Kwa hivyo, mambo yote yamo.

Labda nikupe mfano mdogo Mhe. Spika, univumilie, kuna *topic* katika Biology inaitwa *photosynthesis.* Hii imo katika sura ya amma, na kuna aya moja inayosema *Wajaalna nnahaara maasha*. Aya hii maana yake inasema Mwenyezi Mungu ameujaalia mchana kuwa ni maisha. Sasa ukenda katika kwenye *topic* ya *photosynthesis* maana yake ili ile *process* iweze kuendelea jua lazima liwepo, kwa hivyo *photosynthesis* haiwezi ku-*take place* usiku.

Kwa hivyo, utakapokwenda zaidi, sitaki nichukuwe muda wako Mhe. Spika, ni kwamba mambo yote, ikiwemo *atomic bomb*, kwa kupitia *Suratil fiyl* basi imo ndani ya Qurani. Kwa hivyo, ni muhimu sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri aone haja ya kuwaendeleza walimu wetu wa vyuo vya *Qur-an*, lakini na wizara iwe sambamba na mafunzo haya, ili tuweze kupata wataalamu wa kutosha.

Mhe. Spika, nikiacha hapo natakaniendelee kidogo katika suala zima la maslahi ya walimu. Wenzangu wamezungumza hapa kwamba wizara na serikali imechukua hatua kwamba kuna vijisenti ambavyo vimeongezwa. Lakini mimi nasema tusiishie kudhani kuwa maslahi ya mwalimu na sio mwalimu tu, inawezekana mpaka wataalamu wengine, wakiwemo wa afya na kadhalika, kwamba wahitajio yao sio tu kuwaongeza mshahara, lakini ni kuwatazama katika utendaji mzuri wa kazi zao.

Walimu wetu Mhe. Spika, wanakosa sana pamoja na kwamba wameongezwa posho, lakini suala la usafiri ni kitu kimoja ambacho ni sugu kwa lugha ya sasa hivi. Tunapokwenda katika shughuli zetu, ikiwa binafsi au ikiwa za kazi basi unakutana na walimu wanaomba *lift.* Wengine wanafika mpaka usiku wanafanyakazi mbali na wanakoishi hii haileti picha nzuri. Kwa hivyo, tungeiomba wizara hii lakini pia tungeiomba serikali kwamba ili basi katika

kuwaenzi wataalamu wetu mbali mbali wakiwemo walimu tuone kwamba kuna vitu vyengine minghairi ya mshahara. Kama usafiri na makaazi ni vitu vya kuzingatiwa kwa walimu pamoja na wataalamu wengine.

Mhe. Spika, kuna jambo jengine dogo, lakini inawezekana ni kubwa nina wasi wasi, lakini naomba Mhe. Waziri labda aje atuambie. Kuna tetesi huko njiani zinazungumzwa kuhusiana na suala zima la ajira kwamba kuna walimu ukenda kumtafuta kwa jina lake basi humpati. Ikitafutwa na kupekuliwa kumbe wengine ajira zao zinasemekana zinapitia kwa vyeti vya watu wengine, sasa sijui kama hili lipo analijua Mhe. Waziri au halipo linasemwa tu huko barabarani. Kwa hivyo, tungeomba tuondoshewe wasi wasi huo kwa sababu kuna malalamiko ya aina hiyo.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nataka kidogo nizungumzie suala zima la malengo ya milenia. Katika malengo ya milenia Mhe. Spika, kwa upande wa elimu nadhani kidogo tumepiga hatua kwamba idadi ya uandikishaji ni nzuri maskulini, ingawa Mhe. Waziri hakuipambanua vizuri, au pengine sababu nimechewa kidogo kumsikia, sijaona kijinsia kaipanga vipi kwamba wanawake ni wangapi na wanaume ni wangapi katika wale waliokuwa wameandikishwa.

Pia Mhe. Spika, bado kama walivyosema wenzangu idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa na wale ambao wanamaliza kama takwimu zake alivyoeleza hapa na nitowe mfano tu kwa hili jadweli E katika ukurasa wa 6. Idadi ya waliofaulu hapa kutokana na wale waliofanya mitihani ni 11,515. Lakini ukitoka kidato cha pili mpaka ukija kidato cha sita tunabakia na watu 1,940 na sijui hapa wanawake wanakuwa ni wangapi. Kwa hivyo, nadhani kuna haja ya kuona kwamba angalau ile *dropout*, basi isiwe kwa kiasi hiki, tuwe tunajitahidi. Ndio ile wenzangu waliosema kwamba *quality education* ni muhimu, ili hata ikitokezea bila shaka watakuwepo wanaoanguka, lakini isiwe kwa kiwango hiki kutoka 11,515 mpaka tunabakia na 1,940.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo bado hatujalifikia na sioni pahala popote lilipozungumzwa nalo limo miongoni mwa malengo ya milenia. Ni jinsi ya kumpatia chakula mtoto anayesoma. Mwenyekiti wangu siku zote anasema mtoto mwenye njaa hafundishiki, maana yake atakuwa anapiga miyao, akihesabu boriti, akihesabu kila kitu na kutizama mambo mbali mbali, lakini yanayotokana na njaa. Kwa hivyo, tujitahidini angalau basi kwa bakuli ya uji kwa kuanzia, lakini tulenge kwamba ifike pahala Mhe. Spika, watoto wetu waweze kupata chakula ili waweze kufundishika. Mtoto mwenye njaa Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema ni kwamba hafundishiki, lakini wanajilazimisha tu.

Kwa hivyo, tukilenga huko tutakuwa tunapata nambari nzuri ya watoto ambao wanafaulu. Nadhani pengine hii *dropout* kama nilivyoieleza inatokana na miongoni mwa sababu moja ikiwa ni hiyo.

Jengine Mhe. Spika, ni suala zima la masomo ya sayansi, hatua imepigwa tunaambiwa. Mimi nilikuwa nina pendekezo Mhe. Spika, kwa sababu kila mmoja wetu hapa amechangia kuhusiana na ukosefu wa vifaa vya sayansi, hasa maabara hizi za upande wa skuli za sekondari.

Sasa mimi nilikuwa nina pendekezo Mhe. Spika, kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini serikali ichukuwe jukumu hilo ili tujenge maabara mbili kubwa, moja iweko Pemba na moja iweko Unguja. Lakini ziwe kamili kusipunguwe kitu, halafu badala ya huu utaratibu ambao umesemwa hapa kwamba wanafunzi wanatoka Unguja kwenda Dar es Salaam kufuata kufanya mambo mbali mbali ndani ya maabara, basi iwe ni humu ndani ya nchi yetu, kwa sababu sasa hivi hatuna uwezo wa kila skuli ya sekondari inayojengwa kuwa na maabara yake iliyojitosheleza, basi kuwe na maabara moja tu kwa Unguja nzima na nyengine kwa Pemba nzima. Kisha utapangwa utaratibu ambao wanafunzi wataweza kwa umaskini wetu na kwa kuanzia iwe wanakwenda kujifunza kwa utaratibu mzuri ambao utapangwa, ili watoto wetu waweze kujua hizo sayansi ambazo wanasomeshwa badala ya kuwa wanasoma *theoretical* zaidi, lakini angalau wakenda pale kwenye maabara kila kitu kiwe kinapatikana.

Kwa mfano, akiambiwa *Bunsen burner* anajua na akiambiwa *burette pipette* na vitu vyengine vyote awe anaelewa. Kwa sababu kuna watoto Mhe. Spika, wanamaliza kusoma lakini kuna baadhi ya vifaa vinaitwa *instruments* za ndani ya maabara hawazielewi. Kwa hivyo, naiomba sana wizara na naiomba sana serikali kweli ni maskini hawawezi kuzitosheleza maabara za skuli moja moja, lakini angalau basi iweko maabara moja kubwa kwa Unguja na nyengine kubwa kwa Pemba, lakini zilizokamilika.

Aidha, Mhe. Spika, suala zima la walimu. Limesemwa hapa na tutaendelea kurudia bado hawajatosheleza. Sasa tutakapokuwa na hili ombi au pendekezo ambalo naomba, basi wawepo na walimu kamili waliotimia katika hizo maabara. Bilashaka nikisema hivyo Mhe. Spika, nakusudia hizo maabara zijitosheleze kwa fani zote. Kwa mfano, Chemistry, Biology, Physics na kadhalika, basi na walimu wake waweze kupatikana kwa kuanzia nafikiri tunaweza kupiga hatua.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe muda unamalizika.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante Mhe. Spika, namalizia kwa suala zima la majengo. Katika kitabu hapa imeelezwa kwamba kuna kesi za majengo, wanasema kesi za ardhi za skuli. Hizi Mhe. Spika, kwa kweli tumeshalisemea sana, lakini napenda nilisisitize kwemba wizara ifanye hima kufuatilia suala hili la hati miliki. Lakini bado nilikuwa naomba sana na Mhe. Spika, suala hili nimelisema zamani tangu mimi nikiwa katika kamati hiyo, bahati mbaya kwa utaratibu ambao tunao katika Baraza nimekwenda kwenye kamati nyengine.

Mhe. Spika, lakini ujenzi wa majengo ya skuli bado hauridhishi. Ndio maana vitabu vya Mhe. Waziri anapokuja hapa, kama humu imeelezwa kuwa kuna madarasa 500 ambayo bado yanasubiri nafasi ya serikali kuweza kuyakamilisha. Hili linakuja kutokana na kwamba tunamuelekeo bado wa kizamani wa kujenga majengo ya skuli. Kwa hivyo, tujenge majengo ya kisasa ya ghorofa, nafikiri hata mzigo wa serikali utakuwa umepungua, lakini tutaweza kupata maeneo ya kutosha kwa ajili ya kujenga skuli zetu ambazo zitakuwa na mambo mengi. Ukiacha jengo la skuli, lakini pia tutakuwa na eneo zuri ambalo watoto wetu wanaweza kupata mpaka kufanya mambo ya michezo na kadhalika.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini bado nilikuwa nina mengi sana. Nakushukuru sana.

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuzungumza machache katika wizara hii muhimu sana, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwamba hotuba yake hii imeandikwa kitaalamu ni nzuri sana, kwa ufupi kabisa pamoja na ukubwa wa wizara yake na kila alilolieleza lina takwimu kuhusiana nalo. Japokuwa kuna tatizo kidogo Mhe. Spika, kwamba kwingine alikoelezea basi unataka utafute takwimu zake, kwa sababu hajakupa dondoo hapa kuwa nenda kwenye kumbukumbu ya dondoo ukurasa fulani au zile *subheading* namba gani. Lakini pamoja na hayo ni kwamba ukikaa ukikisoma, basi zote unazipata.

Mhe. Spika, na mimi michango yangu itabidi niifupishe sana kutokana na muda. Nitaanza na mradi wa upanuzi na uimarishaji wa huduma za maktaba. Nataka kwa kupitia kwako Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwamba hatimaye sasa lile jengo la maktaba limekamilika.

Sote tunafahamu kwamba ujenzi wa maktaba hii umechukua muda mrefu, kwisho tukaona ni ndoto isiyoweza kukamilika. Lakini kwa jitihada zake Mhe. Waziri na wajumbe wa bodi imara aliowaweka chini ya uongozi wa Mkuu wa Mkoa wa Kusini, basi wamehakikisha kwamba jengo hili limekamilika.

Pia nimkumbushe Mhe. Waziri kwa kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba bado kuna kazi ya kujenga jengo kama hilo au linalolingana na hili Pemba kwa madhumuni hayo hayo. Lakini nikumbushie Mhe. Spika, kwamba mwaka jana wakati tulipokuwa tukichangia hotuba ya wizara hii kuhusu suala hili, palijitokeza wizi wa fedha zilizoibiwa na mshika fedha pale katika ujenzi wa maktaba hii. Nitamuomba Mhe. Waziri aje atuelezee hatua ile imefikia wapi, asituambie tu kwamba iko polisi au kesi iko polisi. Atuambie kama wizara wao wenyewe hasa suala hili limefikia wapi.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri katika ukurasa ule wa 24 kuhusu masuala mazima ya jinsia. Katika wizara zilizokuwa katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, wizara ninayoiona ambayo imezingatia kwa kiasi kikubwa masuala ya jinsi ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Wizara hii Mhe. Spika, sio tu kwa wanafunzo kwamba wanawake wameandikishwa kwa asilimia kubwa sana, au labda wamepasisha wanawake kwa asilimia kubwa sana. Lakini pia katika ngazi ya uongozi. Mhe. Waziri amezingatia hili, ndio maana katika ngazi za juu za uongozi utaona kuna wanawake wenye uwezo na uzoefu wengi sana katika wizara hii ya elimu na mafunzo ya amali. Mhe. Waziri nimpongeze kwa hili.

Mhe. Spika, lakini kidogo angenifafanulia katika kifungu kila cha 57, kwa sababu amezungumza masuala ya jinsia. Alizungumzia kwamba wamepatiwa mafunzo ya kuhamasisha juu ya masuala mazima ya jinsia. Katika hawa waliopatiwa mafunzo hayo wanawake walikuwa wangapi na wanaume walikuwa wangapi.

Pia Mhe. Spika, sio hayo tu, angetueleza kutokana na mafunzo hayo wamefaidika kwa kiasi gani, maana yake *target* ilikuwa ngapi na mafanikio yamefikiwa kwa kiasi gani.

Mhe. Spika, nikitoka kwenye masuala ya jinsia, niendelee kumpongeza Mhe. Waziri kwamba hotuba yake hii amezungumzia masuala ya madrasa na vyuo vya Qurani. Mhe. Zakiya Omar amelizungumza vizuri sana hili. Mimi pia niungane naye kwamba ni vyema Mhe. Waziri, najua kwamba anafahamu umuhimu wa madrasa hizi. Ndio maana katika kitabu hiki ameona umuhimu wa kuandika, pia kuziorodhesha na kuzifanyia tathmini na kujua ziko ngapi, pamoja na walimu na wanafunzi wako kiasi gani.

Kwa hivyo, nimuomba aangalie pia uwezekano wa kuwahudumia kama sio wanafunzi kwa kuanzia basi hata walimu wa madrasa hizi. Kwa sababu walimu Mhe. Spika, wana kazi kubwa katika madrasa. Mimi ni mlezi wa baadhi ya madrasa hapa mjini, lakini pia nje ya mji. Tatizo kubwa linalojitokeza ni kwa

walimu wake. Mhe. Waziri amesema hapa atawapatia mafunzo. Lakini namuomba isiwe mafunzo peke yake, awawezeshe pia kwa kiasi. Awawezeshe kwa sababu hawana mishahara, ni kama vile wanajitolea kwa suala hili, ili na yeye mwenyewe Mhe. Waziri liweze kumfungulia milango yake katika anayoyakusudia basi akija hapa atuambie kwamba amewalengea kiasi gani walimu hawa wa madrasa Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 31 pia nimpongeza Mhe. Waziri kwa suala zima la maandalizi ameliona na amelizungumza. Lakini nimuombe kwamba skuli nyingi za maandalizi ziko karibu na barabara, magari yanapita kwa kasi, pikipiki na mavespa yanapita kwa kasi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri aone haja ya kuweka matuta katika skuli ambazo ziko karibu na barabara kwa ajili ya kuwalinda watoto wetu hao wanaokwenda katika skuli hizo za maandalizi.

Mhe. Spika, kwa kuanzia kama anataka Mhe. Waziri mimi nimuoneshe basi nitamuonesha zipo nyingi sana na maombi tumeshapata mengi sana. Watoto wetu ni watoto, madamu ni skuli za maandalizi basi bado ni wadogo, hata ukimuambia subiri basi ikimjia yeye akate njia anakata tu. Sasa pamoja na kwamba maaskari wamezungumziwa suala hili na askari wawepo wakati watoto wanapotoka maskuli, ili kuwavusha njia. Lakini ipo haja pia ya kuweka matuta ili kupunguza kasi ya magari na kupunguza hatari ambazo zinawakabili watoto wetu Mhe. Spika, wakati wanapokata barabara.

Mhe. Spika, nakwenda mbio kwa kuheshimu muda wako. Nizungumzie suala zima la makumbusho katika ukurasa ule wa 56. Mhe. Spika, suala la uhifadhi wa makumbusho zetu ni jambo jema na ndio historia yetu tunavyoiendeleza na kuiwekea kumbukumbu isije ikapotea. Lakini kinachojionesha hapa ni nini Mhe. Spika. Majengo ya makumbusho haya tumekuwa tukiambiwa na tunaendelea kuambiwa kwamba zitafanyiwa matengenezo. Hizi ambazo ziko hapa mjini tunaziona kwamba matengenezo yake bado.

Mhe. Spika, ningemuomba basi Mhe. Waziri atakapokuja atuambie. Yuko *serious* kiasi gani katika kuyafanyia makumbusho haya matengenezo. Kwa sababu, mimi siku nyingi sijaingia katika majengo hayo. Lakini nikipita nje tu hainivutii mimi kuingia kwenye makumbusho yale, ninaona kwamba ninaingia kwenye magofu na sote tunaamini kwamba majengo yakishafika katika hali ile na yakionekana kigofu gofu namna ile Mhe. Spika, unaweza ukaingia peke yako lakini ukatoka na mwenzako. Sasa hapo ndio panapotisha, utakuja kukumbwa halafu tena ujute kwenda kwenye makumbusho.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri atuambie kama kweli yuko *serious* kwenye kuzitengeneza hizi. Ametenga kweli pesa na zitafanya kazi hii au kuna

haja ya kuundia kamati maalum ya kuangalia suala hili linatekelezeka. Kwa sababu Mhe. Spika, tunakwenda kwa wenzetu tunaona makumbusho zao zinavyohifadhiwa na tunaona choyo ya kimaendeleo kwamba sisi tuna historia nzuri, ni *very rich history* lakini kwa nini inakuwa kama vile tumeisahau Mhe. Spika.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwa hili alitilie mkazo wa aina yake na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akimrudisha katika kipindi kinachokuja, akija hapa atuambie basi zimefanikiwa kiasi gani katika kuyafanyia marekebisho makumbusho haya. Anaweza akarudi kama mwakilishi, lakini pia akapanda kwa ngazi ya juu zaidi Mwenyezi Mungu mwenyewe ndiye ajuaye.

Mhe. Spika, nimalizie haraka haraka katika suala zima la ardhi za skuli. Mhe. Waziri amewasilisha hapa kama kesi za ardhi za skuli. Kawasilisha kesi mbili, lakini sisi tumepata kesi nyingi sana na tatizo kubwa linalozungumziwa hapa ni ukosefu wa hati miliki ya maskuli hayo, pamoja na kwamba ni ya serikali lakini kwa kuwa hazina hati miliki basi zinavamiwa na matokeo yake ule ukubwa wa eneo unapungua. Maskuli badala ya kuhifadhika yakawa kwamba ni maeneo ya kupatia elimu, watu wanayageuza kuwa sasa ni maeneo ya makaazi, kunakuwa hakuna usalama kwa wanafunzi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri basi suala hili kwa kupitia kwako Mhe. Spika, aliangalie na awaweke watu madhubuti kulisimamia, kwa sababu sidhani kama kuna utata. Jengo la skuli linajulikana na eneo la skuli linajulikana kwa nini livamiwe. Sidhani kama kuna utata Mhe. Spika. Mhe. Waziri akishaweka watu madhubuti litafanyiwa kazi na nina amini chini ya uongozi wake kama alivyo basi litafanyiwa kazi.

Vile vile anifafanulie kidogo pale kwenye kifungu cha 186 katika suala zima la maombi ya usajili wa walimu yaani leseni za walimu. Sijafahamu naomba aje anieleweshe. Mimi najua walimu wanapewa vyeti vya kumalizia, wanapomaliza elimu, lakini inapokuwa tena wakishapata vile vyeti basi awe sasa na leseni yeye. Mimi nilidhani leseni zinakatia yale majengo ambayo yanatoa elimu kama mafunzo au masomo yaani skuli. Lakini sasa leseni ya kusomesha kumbe mwalimu pia awe nayo. Ningeomba anifafanulie kidogo kwa hili aweze kunielewesha.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache na kwa kuuheshimu muda wako, niseme kwamba mimi mwenyewe binafsi pamoja na wanawake wa Mkoa huu wa Mjini Magharibi, tunaunga mkono hotuba hii ya Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni, hapa itakuwa mwisho wa shughuli zetu kwa mchana wa leo. Jioni tutakuwa na wachangiaji kidogo kabla ya kumwita Mhe. Naibu Waziri na Waziri kwa ajili ya majumuisho.

Wachangiaji kwa jioni watakuwa ni Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Abass Juma Muhunzi na hatimaye Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, baada ya hapo tumwite Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na hatimaye Waziri mwenyewe wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7:00 Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Spika, jioni hii ya leo kunipa fursa na mimi kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa jioni hii.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa utendaji wake pamoja na watendaji wake wote. Vile vile namuomba Mwenyezi Mungu awawezeshe zaidi kwa lengo la kufanikiwa kwenye majukumu yao, katika kuwapatia elimu watoto wetu, kwani elimu ndio msingi wa maendeleo ya nchi yoyote duniani.

Nianze mchango wangu kwa kuzungumzia suala la walimu wa vyuo (madrasa) aliangalie kwa umakini kabisa. Kwa kweli walimu hawa wanao umuhimu mkubwa, tukizingatia katika nchi yetu hii ya Zanzibar naweze kusema asilimia 90 ni waislamu. Kwa maana hiyo, walimu hawa wanawafundisha watoto wetu Dini ya Kiislamu, hivyo umuhimu wao ni mkubwa.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia kwako Mhe. Spika, awaangalie walimu wa vyuo, yaani kama upo uwezekano basi serikali iwasaidie angalau kwa sabuni ikiwa hakuna mishahara, kwa sababu kazi yao ni kubwa ya kuwaelimisha watoto wetu.

Mhe. Spika, suala jengine ni kwamba vyuo vinahitaji kusaidiwa kama anavyofanya Mhe. Waziri, kwa sababu pale kwetu kuna chuo kimoja tayari ameshawahi kutusaidia mabati ya kuezekea. Kwa hiyo, namuomba awe na moyo wa kuendelea kuvisaidia vyuo, kwa lengo la kuviwezesha zaidi.

Vile vile kuna suala la Chuo cha Kiislamu Kiyuyu Micheweni. Mhe. Spika, tukiangalia bajeti ya chuo hiki kila mwaka wanapewa shilingi milioni 50. Lakini bajeti hii ni ndogo sana na wala haikidhi haja kwa chuo kile, kwa sababu kunahitajika kufanywa mambo mengi chuoni kule, kwa hivyo fedha hizi hazitoshi.

Sasa nadhani Mhe. Waziri angeomba kuwezesha angalau bajeti ya chuo hiki ikawa shilingi milioni 200, kwa sababu kuna mambo ambayo yanahitaji kutengenezwa. Kwa mfano, kuna wanafunzi na tukiangalia zile dakhalia wanazokaa ni ndogo sana, yaani hazitoshi.

Vile vile bajeti iliyopita nilimwambia Mhe. Waziri kwamba katika chuo hiki kuna haja ya kujengwa msikiti, lakini kama bajeti yake ingekuwa kubwa basi hilo lingekuwa ni suala dogo sana la kujenga msikiti, kwa sababu haifanani Chuo cha Kiislamu ikawa hakuna hata msikiti. Mhe. Spika, hiki ni Chuo cha Kiislamu sasa nilimwambia Mhe. Waziri kuna haja ya kujengwa msikiti, lakini leo yale madarasa wanayosoma ndio misikiti.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwamba bajeti iliyopita nilimwambia kuhusu suala hili, lakini hakulizingatia. Kwa hivyo, namuomba tena na kwa sababu yeye ni mtu mzima mwenye heshima na hivi sasa Mwenyezi Mungu akipenda tunataka tukukabidhi nchi yetu uiendeshe *Inshaallah. (Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi anipe maelezo kuhusu suala hili la msikiti limefika hatua gani.

Nikiendelea na mchango wangu kuna suala wakati wa zamani kulikuwa na utaratibu wanafunzi ambao wanaokuwa dakhalia serikali ilikuwa ikiwasaidia chakula, lakini hivi sasa hakuna tena utaratibu huo mpaka wanafunzi wajilipie kwa ajili ya chakula. Mhe. Spika, kwa kweli kuna watoto wengine ambao wazee wao ni wanyonge sana, kwa hiyo wanakuwa wanapata tabu sana na hasa tukizingatia wako mbali na familia zao. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, kwa maana hiyo wanakuwa wanateseka sana kwa sababu mimi niko karibu nawaona, yaani wanakuwa wanapata shida pamoja na njaa, wakati elimu na njaa haviendani. Kwa hiyo, Mhe. Spika namuomba Mhe. Waziri alizingatie suala hili kwa lengo la kuwasaidia angalau kwa chakula kidogo.

Mhe. Spika, kuna suala la *transformer* ya Kiyuyu na Mhe. Mjumbe mwenzangu amelizungumza. Suala hili pamoja na kuwa la Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Lakini yeye Waziri mhusika aliangalie kama kule

Kiyuyu ikiwa hakuna umeme wanafunzi wanakosa masomo yao. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kama mwenzangu alivyomuomba kwamba alivalie njuga suala hili, ili *transformer* ipatikane kwa haraka, kwa ajili ya kuondosha tatizo liliopo.

Hata hivyo, kuna suala jengine ambalo nataka nilizungumze na Mhe. Mjumbe mwenzangu amelizungumza kuhusu wanafunzi wanaofutiwa mitihani. Mhe. Spika, hivi mwanafunzi anaadhibiwa adhabu ambayo haistahiki kupewa. Kwa mfano, mwanafunzi amekopia mtihani mmoja, kama ni sayansi kuna *Biology*, *Physics*, *Mathematics* na mengineyo, sasa kwa kuwa amekopia mtihani mmoja anafutiwa mitihani yote. Mhe. Spika, hali hii ni kuwaonea wanafunzi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba mwanafunzi aadhibiwe kutokana na kosa alilolifanya, kama ni mtihani mmoja aliofanya lile kosa, basi afutiwe ule mtihani mmoja na halafu aangaliwe na masomo mengine, kuondosha adhabu ya kufutiwa yote, kwani tukiwapa adhabu hiyo ni kuwadumaza wasiendelee na masomo yao.

Kutokana na hali hii inakuwa sawa na mwanafunzi ambaye hakufanya mtihani hata mmoja au yote amefeli, pengine kama kukopia ni somo moja tu. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie kwa makini kabisa, ikiwa ni amekopia mmoja basi afutiwe ule tu ambao amekamatwa na bomu.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naomba nimalizie hapo.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mambo machache katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuendelea kutuletea hotuba ambayo imejaa takwimu, kwa sababu si wizara nyingi ambazo utafungua vitabu vyao ukaona kuna maneno na takwimu.

Kwa mfano, kuna wizara moja naogopa kuitaka kwa sababu tayari tumeshaijadili, lakini zile ambazo hazijapita zitajirekebisha. Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, yaani huwezi kuona namna umeme unavyopanda bei na kushuka, matumizi ya umeme, maji yako vipi, *data* hizo maisha huwezi kuziona.

Kwa hivyo, Mhe. Spika hili ni jambo la kupongezwa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwenye kitabu hiki, majadiliano yetu katika Baraza hili pamoja na semina nyingi, tumekipa umuhimu suala hili la uendelezaji wa watu kielimu na kiafya kama njia moja ya kupata nguvu kazi itakayoshiriki katika kuondosha umasikini na kujenga uchumi wetu. *(Makofi)*

Kwa kweli suala hili linafanyika pole pole, lakini bado matumizi yetu katika bajeti ya elimu ni kikwazo kikubwa katika kufika lengo hili. Kwa mfano, tukiangalia na kwa kuwa hatuna muda mkubwa wa kutoa maelezo mengi. Lakini tukiangalia bajeti ya juzi Tanzania Bara ilivyotangazwa kuhusu matumizi ya elimu na tukiangalia ya kwetu sisi kasma ambayo tunaitengea elimu, basi tumetofautiana Kenya, Uganda nadhani na nchi nyengine za Afrika ya Mashariki itakuwa tunatofautiana.

Kwa hivyo, jambo la mwanzo la kuzingatia kwa serikali ni kuipa umuhimu elimu kwa kuiongezea bajeti.

Mhe. Spika, tukiangalia katika *data* chache ambazo tunaweza kuzinukuu katika kitabu hiki. Kwa mfano, tukiangalia ile *ratio* wanafunzi kwa walimu kwa skuli za serikali ni kubwa wakati skuli hizi za *private* ni 15 na *government* 30. Nadhani kuna haja ya kuipunguza, inawezekana ufaulu mdogo wa wanafunzi ukachangiwa na wingi wa wanafunzi katika darasa.

Mwalimu ambaye anatakiwa kuhudumia, mwenye kulipwa maslahi madogo na halafu ukimuongezea mzigo wa kufundisha inaweza kuwa ni tatizo. Kwa hivyo, ni matumaini yangu kwamba tutalizingatia hilo na wizara itazidi kuongeza ajira katika elimu na serikali nayo itaongeza matumizi katika elimu, kwa lengo la kufikia kwenye kiwango ambacho skuli zetu za *private* zinafikia.

Mhe. Spika, nilipoangalia takwimu nyengine kidogo zilinifadhaisha na hivi ni viwango vya kufaulu. Kwa mfano, tukiangalia *average* ya miaka mitano kuanzia 2005 hadi 2009 kwa wanafunzi wa *Form IV Division One* wamepata 0.95 *percentages* na tukiangalia kwa *Form VI Division One* ni 3.6 ya wanafunzi wote.

Lakini katika mwaka husika 2009 wakati *Division Four average* 0.95 *percentages*, mwaka 2009 imeshuka na kuwa 0.5 *percentages*. Vile vile kwenye *Form VI* wakati *average* ya *Division One* ni 3.6 *percentages*, mwaka 2009 imekuwa 1.9 *percentages*.

Mhe. Spika, *data* kwenye *Division Four* zinaonekana kwamba *Form IV on average*, wakati *Form VI* ilikuwa 25 *percentages*. *Data* hizo zimekuwa *maintained almost* katika mwaka 2009 ziko sawa na *evarage*.

Sasa tukiangalia data hizi basi unaweza kuona namna gani kiwango cha kufaulu katika elimu kilivyo kidogo hasa kwa *Division One*. Kwa kweli sitarajii wanafunzi wote wapate *Division One*, kwa sababu *Division One* ni kiwango kilichokikubwa.

Lakini angalau tukiwa na *Division Two* waliowengi, basi tunaweza kuwa tumepiga hatua, hata *Division Two* katika *data* hizi Mhe. Spika ni ndogo sana. Kwa hivyo, nilisema niziseme hizo, kwa sababu ukiziangalia hizi data hazitoi matumaini ya kwamba kiwango cha elimu hapa kinapanda.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka nilizungumzie ni muhimu sana katika maendeleo ya elimu, kwa kweli ni maendeleo ya kila wizara katika uendeshaji wake ni kuhakikisha kwamba *good governance* ni jambo linalopewa kipaumbele.

Mhe. Spika, tunalo tatizo katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) na hili pengine Mhe. Waziri halifahamu, lakini sisi tumelipata basi inabidi kutumeleze Mhe. Waziri. Wakati tulipoanza Chuo Kikuu hiki hasa katika suala la uajiri, tulianza vizuri, yaani hakukuwa na suala la kuangalia mambo ambayo si ya msingi katika kuwapata walimu ambao wataweza kutusaidia.

Lakini taarifa ambazo tunazipata hivi sasa kidogo tunaanza kurudi nyuma. Kwa mfano, kuzingatia viwango vya elimu au ufaulu kama ndio njia ya kumpata mwalimu, sasa tunaanza kuangalia na *factors* nyengine.

Mhe. Spika, tumepata taarifa kwamba ni moja katika *Policies* za Vyuo Vikuu, yaani ni utamaduni wao, wanafunzi wanaofanya vizuri na kupata *First Class* mara nyingi wanakuwa *retain* katika Vyuo Vikuu, kwa ajili ya kuendelezwa mara moja, kwa sababu ile ni nyenzo ambayo ni muhimu.

Kwa mfano, ukiweza kumpatia *Masters*, halafu *PhD*, kwa kweli inapata mwalimu mzuri. Lakini hapa nasikia kuna mwalimu ambaye ametokea kabisa amepata *First Class* kwa sababu ya kuzingatia mambo mengine *Policy* hii imekiukwa na Wizara ya Elimu na wala hawakumuajiri kama *TA*. Mhe. Spika, inasemakana kwamba hatuna tena *Policy* ya kuariji *TA*, lakini *policy* hiyo haijazungumzwa kufutwa katika Chuo Kikuu.

Kwa hivyo, nilisema hilo lazima nilizungumze, ili Chuo Kikuu hasa katika Sekta ya Elimu kusiwe na mambo ya ajabu kwenye masuala ya uajiri, kwa sababu tunahitaji walimu ambao wenye uwezo. Kwa kweli walimu wenye uwezo wanawaandaa wenyewe kwa kuwafundisha na kuwafanyia mitihani na baadaye wanafaulu na kupewa.

Lakini ukimuachia mtu mwenye *Division* ya Kwanza na kuchukuliwa na sekta nyengine ukamtoa kwenye elimu, sasa elimu unataka kuchukua watu wenye division gani? Maana yake hawa ni watu wachache mno, sasa kama hakuna njia ya kuwa-*retain* na halafu na kuwaongezea elimu na baadaye wakabakia kwenye Vyuo Vikuu, basi tutakuwa na walimu wenye viwango vya chini.

Mhe. Spika, nilitolewa mifano miwili hapa ya wale walimu *Professor* Rai na *Professor* Mohammed Ali Shehe, ambaye ni ndugu yake Mhe. Omar Ali Shehe, ambao wameweza kupata uteuzi kama ni miongoni mwa wanasayansi 100 wa dunia katika mwaka huu.

Kwa kweli hili ni jambo la kufurahisha sana, wasingepatikana hawa tukiangalia wengi wao tunawafahamu kama vile Rai kijana tokea udogo wake namna alivyokuwa akifaulu na historia yake imeelezwa kwenye maelezo aliyokuwanayo Mhe. Hija Hassan Hija. Hata hivyo, walikuwa ni wanafunzi bora, hata *Form VI* alikuwa ni mwanafunzi bora na leo amekuwa *Professor* anatambulikana, kijana wa miaka 38.

Mhe. Spika, kwa Zanzibar hiyo ni heshima kubwa. Kwa maana hiyo, tunaweza kuwatengeneza akina Rai wengi sana, lakini tukifanya mas-hara tukasema mwalimu ni mwalimu tukazingatia *factors* nyengine zisizokuwa za kielimu basi tutakosa walimu wazuri. Hilo lilikuwa suala la *governance (Makofi)*.

Lakini suala la miradi kwa ujumla hii miradi ya skuli. Mhe. Spika, tunampongeza Mhe. Waziri kwamba majengo ya skuli yanaongezeka. Pamoja na hayo, majengo yanavyoongezeka sisi yanatutia hofu ya ule uendelevu wa majengo haya. Mhe. Spika, inawezekana ikawa leo tunayo idadi kubwa ya majengo ya skuli na baada ya miaka mitano yamekwisha.

Tunavyoona ushiriki wa wananchi katika *grass root* ni mkubwa kwenye miradi hii na kule kwa wananchi hakuna utawala mkubwa wa mambo ya majenzi, yaani kule kuna ufundi wa kawaida wa kupanga matofali na kujenga. Kwa hivyo, tumeziona baadhi ya skuli hizi ambazo zimejengwa kwa miaka michache tu tayari zimeanza kuporomoka. Aidha unaweza kuziona skuli hizi ambazo ni mpya kabisa, lakini haziko katika *design* nzuri au *structure* ambayo unaweza kuamini hii inaweza kuwa endelevu.

Mhe. Spika, tunasema pamoja na kuongeza majengo yetu, wizara lazima aingalie utaalamu wa ufundi katika majengo haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, labda nimshukuru tena Mhe. Waziri kwamba kilio changu cha muda mrefu sana kuhusu Gofu la Jambangome kilisikika, hivi sasa gofu hilo

linaangaliwa na serikali rasmi na kutambulika. Lakini tatizo liliopo pale ni kulifikia lile gofu.

Kwa hivyo, ni matumaini yangu kwamba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi nayo itatoa mchango wake, katika kuhakikisha kwamba zile kilomita mbili za barabara ambazo zinaende kwenye Gofu la Jambangome nazo zinatengenezwa, ili gofu lile lipate kutembelewa.

Mhe. Spika, nimekuwa nikifuatilia vile vile matatizo madogo ya skuli na hili sitaki kuwa muwazi sana ingawa uwazi ni mzuri. Lakini katika skuli zangu tano za Chambani iko skuli moja inakuwa inalalamikiwa sana kwa matatizo baina ya mwalimu mkuu na walimu wengine. Suala hili kwa kweli nilipolipata sikulidharau, nadhani hata Afisa Mdhamini kwa sababu na yeye ni skuli zake basi analifahamu suala hili.

Kutokana na hali hiyo, leo kwa mara ya mwanzo ingawa tumekuwa tukilizungumza kwa mara nyingi, kwa sababu hizi skuli ziliopo pale Chambani ni skuli tano. Kwa hivyo, mimi ninafahamu ilivyokuwa wizara imemteua huyu kama ni mwalimu mkuu basi anao uwezo, lakini pametokea msuguano katika ile skuli mmoja.

Mhe. Spika, mimi ninaushauri mwalimu huyu angeondoshwa na kupelekwa skuli nyengine ambayo mahusiano yake na walimu yatakuwa ni mazuri, yaani hayajavurugika. Wakati unapouliza swali kwa nini ufaulu wa wanafunzi unakuwa ni mdogo, basi moja katika sababu unaambiwa hili, suala hili haliko kwa walimu tu na hata ile Kamati ya Elimu pia inakupa sababu hizo hizo.

Kwa hivyo, naomba wizara ijivue walama katika hili, iende ikasikilize skuli hii na mimi ninamwambia Mhe. Waziri kwa siri ni skuli gani na vyema ni kulirekebisha tatizo hili.

Mhe. Spika, suala la tatizo la usafiri kwa wanafunzi limekuwa kubwa. Kwa kuwa hivi sasa tunaamini wenyewe kwamba *tuition* ni jambo la lazima ingawa hatulipendi. Wanaoathirika sana na *tuition* ni wanafunzi wa kike, kwa kweli tukiwaona wamejipanga mpaka wakati wa saa tatu au nne za usiku wakisubiri gani na wala hakuna gari za uhakika za kuwachukua wao, hili linaendelea kuwa ni tatizo sugu. *(Makofi)*

Tulisema hivi juzi tumesikia mfano mzuri wa Benki ya *CRDB* ikitoa mabasi kwa ajili ya kuanzisha usafiri wa wanafunzi. Mhe. Spika, tunaomba na hapa mzungumze na hizi *Institution* za Kifedha, ambazo wateja wao ni hawa wanafunzi pamoja na wazee wao, basi na wao waije mfano huu wa kuanzisha usafiri wa wanafunzi.

Mhe. Spika, pia kwa wale wafanyabiashara ambao watataka kuwekeza katika mabasi haya ya wanafunzi kwa sababu wanachukua nauli ndogo, basi serikali nayo izingatie kwenye masuala ya ushuru, ili tuone angalau suala hili linaanza kurekebishika *(Makofi)*.

Lakini tatizo la wanafunzi wa kike linaweza kupata ufumbuzi katika ujenzi wa dakhalia za wanawake. Pamoja na kwamba tumeondosha dakhalia hatuwezi kuzihudumia. Mhe. Spika, inaonekana kuwa dakhalia za wanawake zinazo umuhimu wake, hata kama zitakaliwa hizo siku za mitihani kwa hayo madarasa hayo yanayofanya mitihani.

Hivi sasa nyumba za watu binafsi unaambiwa wanafunzi leo wamehamia nyumba hii wanakwenda kusoma mpaka saa sita za usiku, wengine mpaka asubuhi, sasa vitu kama hivi havifurahishi, kwa sababu havina udhibiti. Lakini tukiwa na madakhalia ya wanafunzi wa kike na hilo haliwezi kuwa na gharama kubwa, kwa sababu dakhalia hizi sasa inaonekana sasa wazee wamebeba mzigo wa wanafunzi wale. Kwa hivyo, kazi ya serikali sasa ni kuwa na yale majengo ya kuwahifadhi wale wanafunzi kwa siku ambazo watafanya mitihani.

Mhe. Spika, nimalize kwa sababu tayari umeshanionesha dalili. Kwa kweli tunalo tatizo kama nilivyosema mzigo huu wa elimu. Kwa mfano, leo tunayo Elimu Mbadala, Elimu ya Chekechea, Elimu ya Msingi pamoja na Vyuo Vikuu katika kapu moja.

Mhe. Spika, ninaushauri wizara ingepunguziwa mzigo ikaachiwa Elimu ya Juu na *Primary* na Elimu hii ya Chekechea, ilivyokuwa *mainly* ni malezi ikabakia mikononi mwa wazee kupitia kwenye Serikali zao za Mitaa. Kwa maana hiyo, tukifanya hivi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itakuwa tumeipunguzia mzigo, kwa sababu kuiongezea mzigo leo ya kwenda kulea watoto.

Kwa mfano, tumeambiwa hapa bajeti ya kwenye *Nursery* kubwa zaidi kuliko bajeti inayotakiwa sehemu nyengine ambazo ni muhimu, yote hii kwa sababu tumeyachanganya mambo pamoja. Nadhani serikali iliangalie hili kuivua kidogo kwa ajili ya kuipunguzia mzigo wizara, ili ibakie na sehemu ndogo ambayo inaweza kuishughulikia kwa lengo la kuongeza ufanisi katika elimu.

Mhe. Spika, kwa sababu dakika zako sio nyingi. Kwa hivyo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, vile vile ninampongeza sana Mhe. Waziri na ninamtakia baraka na heri kwa yale anayoyaomba Mwenyezi Mungu ampe *Inshaallah. (Makofi)*

Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuzungumza machache sana ndani ya dakika kumi kuhusu bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, nataka nitoe pongezi zangu za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kuweza kuanzisha Vyuo Vikuu vyetu vya Zanzibar, tunashukuru kwamba hivi sasa vinaendelea vizuri na tunapata wataalamu wengi kutoka vyuo hivi. Kwa hivyo, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa jitihada ambayo serikali imeichukua.

Nikianza mchango wangu katika Jimbo langu la Kwamtipura. Mhe. Spika, namkumbusha Mhe. Waziri katika Skuli ya Shaurimoyo kwa muda mrefu hivi sasa zaidi ya miezi minane mpaka tisa hatuna mwalimu mkuu. Kwa hivyo, namkumbusha Mhe. Waziri, kwa sababu tayari nimeshamuandikia, lakini muda umekuwa mrefu na tunategemea pengine sijajua mwezi gani mitihani itaanza kufanywa. Kwa hivyo, tukipata mwalimu mkuu katika skuli yetu, basi naamini vijana wetu watapata maandalizi mazuri kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye mitihani yao.

Kwa kweli mwaka uliopita skuli yangu ya Shaurimoyo haikufanya vizuri kwenye mitihani. Kwa maana hiyo, nikiweza kupata mwalimu mkuu basi naamini kuwa tutaweza kupasisha wanafunzi wengi sana. Nadhani hili Mhe. Waziri atakuwa analikumbuka na ninaamini pengine ndani ya wiki hii aweze kutangaziwa mwalimu mkuu.

Mhe. Spika, nikiendelea nataka nimpongeze Mhe. Waziri zaidi baada ya kutoa takwimu ya ongezeko la madrasa katika maeneo yetu. Hivi sasa wananchi wetu hasa walimu wanajitahidi sana na kama walivyosema wenzangu walimu wetu hawa wako katika mazingira magumu. Hata hivyo, serikali imo kwenye mchakato wa kuangalia kutafuta namna ya kuweza kuwawezesha na wao, kwa sababu naamini hali ikiwa nzuri basi walimu wetu wa madrasa serikali itaweza kuwangalia.

Lakini katika maandalizi hayo kuna baadhi ya mambo nitamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, tujaribu kuyazingatia. Kwa mfano, tukiangalia hivi sasa kitakwimu sisi humu sote ni wanasiasa, kwa bahati nzuri humu tumo vyama viwili tu, yaani CCM na CUF.

Lakini tukiangalia kwenye majimbo yetu kitakwimu matawi ya CCM na CUF yaliomo ndani ya majimbo yetu, basi ni machache sana tukilinganisha na madrasa zilizomo ndani ya majimbo yetu. Kwa hiyo, hii inamaanisha kwamba wananchi wetu wanataka tuzishughulikia madrasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namfahamu Mhe. Waziri kwa jitihada zake kwa kweli yuko mahiri sana ukimwambia jambo basi anatekeleza. Hivyo, namuomba sana katika hii misaada ambayo tutakayoiomba pamoja na kuangalia kasma zetu kwa kuwa tunayo Idara ya Mufti hapa, basi si vibaya tukaweza kushirikiana naye ingawa yeye yuko kwenye Wizara ya Katiba na Utawala Bora, kwa ajili ya kuweza kuwasaidia kutafuta misaada kwa lengo la kuboresha madrasa zetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi karibuni nilifanya ziara katika madrasa zangu zote za Jimbo la Kwamtipura. Kwa kweli Jimbo zima la Kwamtipura kuna matawi saba ya CCM lakini kuna madrasa hamsini na sita, sasa tuangalie wananchi wanataka matawi wananchi wanataka madrasa, matawi ya CUF yamo mawili ndani ya jimbo langu. Kwa hivyo madrasa zimo hamsini na sita ukiunganisha matawi ya CCM na matawi ya CUF yaliyokuwemo ndani ya jimbo langu basi madrasa ni nyingi sana, kwa hivyo nilikuwa naomba sana madrasa hizi tuzisaidie nguvu na ukiangalia matatizo ya madrasa yanalingana, madrasa zetu nyingi utakuta wamejitahidi kujenga kwenye vipenu wameezeka lakini watoto wakati wa jua wanaumia sana.

Kwa hivyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tukishirikiana na Idara ya Mufti na kwa njia nyengine zozote wahisani pamoja na serikali basi walimu wetu wa madrasa tuweze kuwapatia yale *Plywood* kwa ajili ya dari kuzuia lile joto kwa kweli itakuwa tumewasaidia. Lakini vile vile Mhe. Waziri katika jitihada zako basi ukiweza kupata mabusati kwa sababu kuna mwenzangu mmoja alisema vijana wetu wanakwenda na nguo zao katika madrasa, lakini akirudi amechafuka kwa sababu wanakaa chini kwenye sakafu tukiweza kuwapatia mabusati sisi wenyewe kama viongozi wa majimbo tutajitahidi lakini Mhe. Waziri na wewe mikono yako iwe mirefu zaidi basi naamini unaweza kutusaidia.

Lakini vile vile hali kadhalika bati kuna madrasa nyengine wameshajenga lakini uwezo wa bati hawana hali kadhalika matofali na vitu vyengine, kwa hivyo Mhe. Waziri mimi nashukuru nilipoona jadweli ambayo inaelezea madrasa jinsi zinavyoongezeka, lakini vile vile tukiziimarisha madrasa zetu kwa kweli hii hali ambayo tunayo sasa hivi itapungua. Sasa hivi ukiangalia vijana wengi wanakaa katika vigenge wanakula unga na wanavuta bangi, sasa tukiziimarisha madrasa zetu basi naamini watoto baada ya kwenda kukaa katika vigenge wataingia katika madrasa zetu ili waweze kupata maadili ya kiislam. Kwa hivyo hili nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri tujaribu kushirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba madrasa zetu tunaziimarisha.

Mhe. Waziri tunakushukuru sana kwa kutupatia masahafu kila baada ya mwaka mmoja lakini tunakuomba kama tulivyosema madrasa ni nyingi kuliko hata

skuli, nilitaja matawi tu ya CUF na CCM lakini hata skuli, kwa hivyo bado tunahitaji misahafu mingi na vijana wetu waweze kupata elimu ya *Qur-an*.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nataka nimalizie kama alivyosema Mhe. Abass Juma Mhunzi, hizi skuli za chekechea ambazo katika sera yetu ya elimu tumesema tuanzishe na sasa hivi sera yetu ianze katika skuli za chekechea mpaka *Form IV,* mimi nashukuru kwamba katika jimbo langu tumejenga skuli ya Chekechea moja mwaka 2006 tuliifungua na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali nashukuru alinileta Mhe. Rais akaja kuifungua skuli ile lakini vile vile kuna skuli nyengine ya chekechea ambayo tayari sasa hivi tunaikamilisha tunategemea katika sherehe za elimu bila ya malipo mwezi wa tisa zikianza tutamualika tena, au tutamuomba Mhe. Waziri atuletee mgeni mzito kwa ajili ya kuja kufungua chekechea ile.

Kwa hivyo katika mwaka 2006 ulipokuja kufungua chekechea ya Kwamtipura tuliomba tupatiwe kompyuta sasa Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kwa kuwa chekechea zimeshakuwa mbili na sasa hivi vijana wanatakiwa kuingia katika mtandao mapema basi nitamuomba siku atakayokuja kuzindua ile skuli yetu ya chekechea atuchukulie kompyuta mbili, moja itakuwa ya Kwamtipura na moja hii ya Shehia ya Mkele ambayo tunategemea kuifungua hivi karibuni.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naamini kama nilivyosema Mhe. Waziri ni msikivu haya yote ambayo nimeyazungumza naamini ataweza kuyafanyia kazi, nawashukuru sana wananchi wangu wa jimbo la Kwamtipura lakini vile vile tunaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru sana dakika kumi leo sikuzisha ahsante.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Elimu: Mhe. Spika, kwanza na mimi natoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, kabla sijachangia kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza kwanza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtoni, naomba kuunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa asilimia mia kwa mia. Nina sababu ya kuunga mkono hotuba hii kwa msaada mkubwa ambao Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imelipatia jimbo la Mtoni kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2010, nina kumbu kumbu za kutosha kuhusu msaada ambao imetupatia jimbo langu la Mtoni hasa katika sekta hii ya elimu ambayo ni muhimu sana katika maisha ya vijana wetu.

Mhe. Spika, katika jimbo langu la Mtoni nilikuwa na skuli mbili wakati tunaingia madarakani lakini kwa bahati nzuri na kwa msaada wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali basi tumepata skuli nyengine mpya ambayo imeendelea kwa muda mfupi sana na kufikia hadi madaraka kumi na mbili kuanzia mwaka 2007, kwa kweli huu ni msaada mkubwa ambao Wizara ya Elimu inastahiki kupongezwa kwa kiasi kikubwa.

Miradi ya maendeleo ambayo imefanyika katika Jimbo la Mtoni basi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imechangia zaidi ya asilimia arubaini ya fedha ambazo zimepatikana katika jimbo la Mtoni, kumbu kumbu ziliopo zinaonyesha kwamba zaidi ya milioni mia moja na ishirini na nne zimetolewa kwa ujenzi wa madarasa katika jimbo la Mtoni. Kumbu kumbu zinaonyesha vile vile kwamba zaidi ya madarasa ishirini na tatu ambayo yamekamilika kabisa yamejengwa katika jimbo la Mtoni.

Lakini pia inaonyesha kwamba katika kijiji cha Mtoni Kidatu ambako kulikuwa hakuna skuli kabisa kuanzia mwaka 2005 kumekuweko na skuli ambayo hivi sasa ina wanafunzi zaidi ya elfu moja, inaonyesha dhahiri kwamba haya ni maendeleo makubwa ambayo yamechangiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika jimbo langu na mimi binafsi sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwa wizara kutokana na msaada huu.

Mhe. Spika, ukweli wa mambo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imelisaidia sana jimbo la Mtoni hasa katika kuchangia kutoa ajira vile vile, ujenzi wa skuli ambayo imejengwa inaonyesha dhahiri kwamba zaidi ya walimu thalathini wameajiriwa kutokana na miradi hii, kwa hivyo inaonyesha dhahiri kwamba mchango wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haukusaidia tu huduma za jamii, lakini pia imeinua kiuchumi kwa wananchi wa jimbo la Mtoni.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo machache na kuunga mkono sasa naomba nichangie kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza wakati wajumbe walipokuwa wakichangia hotuba hii, suala la kwanza ambalo limejitokeza ni kwamba wajumbe walionyesha kwamba kulikuwa na tetezi kwamba walimu zaidi ya ishirini wamehamishwa katika skuli ya Fuoni na wamepelekwa katika skuli nyengine na kusababisha upungufu katika skuli hiyo.

Mhe. Spika, tumefuatilia suala hili na kuona kwamba uhamisho huo haukusababisha upungufu katika skuli hii, takwimu zinaonyesha kwamba katika skuli ya Fuoni kulikuwa na walimu zaidi ya mia moja na wengine walikuwemo madarasani wakiwa wanne katika darasa moja, kwa hivyo uamuzi huu ni suala ambalo limechukuliwa kwa nia njema kuweza kuona kwamba

walimu wanatumika vizuri kadri inavyopaswa. Kwa hivyo suala la uhamisho huu kusababisha tatizo halipo na tunatarajia hizi skuli nyengine ambazo zina upungufu ziweze kupata walimu hao na waweze kutumika vizuri kama walivyoonyesha baadhi ya wajumbe kwamba kuna skuli nyengine zinaonyesha zina walimu wengi, ndio maana tukachukua maamuzi hayo kuona kwamba pale ambapo pana wingi wa walimu basi tunapeleka pale ambapo pana upungufu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limejitokeza ni kwamba katika kitabu cha bajeti imeonyesha kwamba shilingi milioni mia moja na hamsini zimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa Afisi kuu ya Wizara, mjumbe alihoji kwamba mwaka jana tuliweka kiwango kama hicho na tukasema tunakamilisha lakini mwa mwaka huu tunakamilisha.

Nadhani Mhe. Waziri Kivuli alikuwepo wakati kamati zinajadili bajeti hii na suala hili lilijitokeza na jibu likatolewa kwamba hapa ni suala la lugha tu ndio lilitatiza sio ukamilishaji lakini ni uendelezaji, kwa hivyo hapa ni suala la uendelezaji inawezekana kwamba halikurekebishwa katika maandishi haya.

Suala jengine ambalo limejitokeza ni walimu kupunjwa maslahi yao, Wizara haina taarifa kuhusu walimu wake kwa maana hiyo wengine wamekuwa wakipunjwa na wengine wamekuwa wakieleza, kama ilivyopendekezwa na wajumbe ni kwamba kama kuna mtu yoyote ambae anaonekana mshahara wake haujakaa sawa basi afike ofisini na kuweza kurekebishiwa mshahara wake mara moja. Nadhani hili hata wajumbe walichokuwa wakichangia walilipendekeza na nadhani hilo ndio suluhu yake, lakini wizara kupitia Tume ya Utumishi imejitahidi kadri inavyowezekana kuweza kurekebisha mishahara hiyo na kuona kasoro mbali mbali zinarekebishwa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limejitokeza ni kwamba Wizara ina mpango gani wa kuongeza walimu wa kiingereza wakati inasisitiza kwamba mafunzo ya wanafunzi yaanze mapema madarasa ya chini wakati walimu wa kiingereza hawapo, nasema tuna mradi ambao utaanza hivi karibuni mradi wa World Bank na walimu wa kiingereza basi itakuwa ni sehemu moja ya mradi huu ili kuona kwamba tatizo hilo la walimu linaondoka.

Mhe. Spika, suala jengine ni michango ya skuli itozwe kwa mujibu wa uwezo wa kila mzee, napenda kueleza kwamba hivi sasa kamati za skuli ndizo zinawajibika kusema kiwango gani mwanafunzi atozwe kwa mujibu wa mazingira na haja iliyopo katika skuli zao, kwa hivyo tunaamini kwamba kamati hizi za skuli zinafanyakazi kwa ushirikiano na wazee na wazee bila ya shaka wanashirikishwa katika kutoa maamuzi kiasi gani kitozwe kwa mujibu wa mahitaji yao. Hili si kwamba kila skuli inatozwa kiasi hicho hicho inategemea na skuli pamoja na mazingira na maamuzi ambayo wanayatoa

kamati zilizopo, kwa hivyo tunaamini kwamba kiwango hicho sio sawa lakini kinatofautiana baina ya skuli na skuli kutegemea na maamuzi ya kamati ya skuli.

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo limejitokeza ni nauli za walimu ama hazitoshi ama hazipatikani kabisa, suala hili Mhe. Mjumbe aliagiza au alipendekeza liangaliwe vizuri, suala la nauli za walimu mara nyingi nimekuwa nikilielezea hapa barazani ya kwamba nauli hizo hutozwa kwa mujibu wa nauli ambazo zinahusika katika eneo ambalo mwalimu anahudhuria. Mhe. Spika, inapotokea tofauti ya nauli mara nyingi wizara nayo hukaa chini na kuona kwa kiasi gani iweze kurekebisha nauli hizo ambazo walimu huwa wanapatiwa kwa wakati na kila mshahara unapotoka nauli hizi huwa zinapatikana.

Nadhani kuna tatizo la walimu ambao wameajiriwa kwa wakati ambao Wizara tayari imeshatoa miongozo kwamba anayeajiriwa katika maeneo yake basi hakuna nauli ambayo atapewa, baadhi ya walimu wamekubali kuajiriwa katika maeneo hayo kwa masharti ya kwamba hawatapokea nauli kutoka Wizarani, wale wote ambao wanastahiki kupewa nauli basi wanapata nauli zao kwa wakati na nauli inayostahiki kwa wakati ule.

Mhe. Spika, suala jengine ni posho za wanafunzi hazitoshi ama zinachukua muda mrefu, napenda kueleza kwamba wizara ya elimu kupitia bodi ya elimu ya juu inawapa posho wanafunzi ambao wanahudhuria masomo Tanzania Bara kwa hivi sasa, wale ambao wanasoma hapa Zanzibar basi hivi sasa hawapati posho hili la wanafunzi hii imetokana na sababu kwamba mwaka jana tulibajeti wanafunzi mia tatu, lakini waliokwenda kusoma ni zaidi ya mia sita. Kwa maana hiyo idadi ya bajeti hiyo haikuweza kutosha kuweza kuwapa posho wa hapa Zanzibar na wale ambao wanahudhuria bara mara nyingi Wizara inajitahidi kwamba mwanafunzi apate posho hiyo kwa wakati na kwa kiasi ambacho amepangiwa, kama kutatokezea tofauti pengine itakuwa ni ucheleweshaji wa kupata pesa hizo ama matatizo mengine ambayo Wizara itayaangalie kwa upande au inavyofaa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limevuta hisia za wajumbe wengi ni suala la magofu ya kwa Bihole kuna tuhuma kwamba magofu ya Bihole kuna sehemu imeuzwa na kwa maana hiyo kuna malalamiko katika maeneo hayo, mimi binafsi nimelifuatilia suala hili kwa kuwahoji baadhi ya watu ambao wanaishi katika maeneo ya huko kwa Bihole, lakini pia wengine wamo katika kamati hiyo ya hao wanaoshiriki katika magofu hayo. Kilichojitokeza ni kwamba kwa muda mrefu magofu haya au eneo hili la magofu lilikuwa halijapimwa na nadhani mwaka jana tu ndio uamuzi wa kuyapima magofu haya au maeneo ya magofu ndipo ulipofanikiwa, kilichojitokeza kuna baadhi ya wananchi walishaimarisha baadhi ya vipando katika maeneo ambayo yako karibu na eneo

hili la magofu na wakati upimaji ulipofanyika ulizingatia suala hilo la wazee pamoja na wananchi ambao wamejiimarisha katika maeneo hayo ili kuepusha migogoro wakati wa upimaji.

Kwa maana hiyo eneo ambalo limepimwa hakuna sehemu hata ndogo ambayo imeuzwa na kupewa mtu mwengine kilichojitokeza ni kwamba upimaji ulipofanyika ulizingatia maeneo ambayo watu tayari wameshapanda vipando vyao ili kuepusha migogoro na migongano katika eneo hilo. Napenda kutuoa taarifa tu kwamba eneo lote ambalo limepimwa hivi sasa liko salama na hakuna mtu ambae anaweza kuliingilia na kuweza kufanya kazi zake binafsi.

Mhe. Spika, eneo hili nafikiri tutakumbuka kwamba limefika hadi kwenye miembe ile na nadhani katika ile miembe kuna sehemu ambazo watu wameshajiimarisha kwa hivyo sehemu zile wakati wa kupimwa ziliachwa, tukasema tuweke mipaka ambayo hivi sasa itakuwa ndio mipaka inayohishimiwa kwa maeneo hayo.

Mhe. Spika, kuhusu ajira ambayo imefanywa kwamba zimefanywa katika familia moja hili sio kweli, kwa sababu aliyeajiriwa pale ni mtu mmoja tu hadi hivi sasa na ambae ameajiriwa kwa ajili ya kusafisha sehemu hiyo ya magofu, kwa hivyo hakuna ajira zilizopatikana kwa familia moja tu. Kilichokuwepo ni kwamba kuna kamati ambayo wenyewe wamejichagua kwa mradi huu ambao ni wao wenyewe wa maendeleo, kwa hivyo mradi huu unawahusisha wananchi wote lakini kupitia kamati yao ya maendeleo ambayo wenyewe wameichagua, kwa hivyo hakuna suala la kwamba walioajiriwa au wanaoshiriki wote wa familia moja.

Suala jengine kuhusu magofu ni lile la mji wa kele Unguja Ukuu. Mhe. Spika, eneo hili kama ilivyodaiwa kwamba lilivamiwa lakini serikali imepeleka malalamiko yake Mahakamani na Mahakama imezuia uendelezaji wa eneo hili hadi itakapotoa amri nyengine, wizara yangu imefuatilia kwa karibu na kukumbusha ili kuona kwamba tatizo la eneo hili linatolewa uamuzi na serikali azma yake ni kulipima eneo hili bado iko pale pale na mchakato wa kupima tayari umeshaanza, tunasubiri maamuzi ya Mahakama vipi itaamua kuhusu eneo hili.

Kwa hivyo napenda niseme tu kwamba eneo hili au malalamiko haya yako Mahakamani na mahakama imesitisha ujenzi na serikali kupitia Wizara ya elimu inasubiri maamuzi ya Mahakama.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limejitokeza ni suala la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itilie mkazo elimu ya msingi, suala hili la elimu ya msingi nadhani tuna mradi mzima wa kuendeleza elimu ya msingi na kila baada ya

muda serikali inatoa fedha kwa ajili ya kuelimisha au kutilia mkazo elimu hii ya msingi, kwa hivyo kuna fedha kila. *cotter* au kila miezi mitatu huwa zinatiwa kwa ajili ya uimarishaji wa elimu ya msingi. Kwa hivyo Wizara imeliona hili na kuona kwamba kila baada ya muda ikiwezekana au ikipatikana fursa ya kuzitoe fedha hizo kwa uimarishaji wa elimu ya msingi basi linafanyika, moja ambalo linafanyika ni uimarishaji wa madarasa, ujenzi wa madarasa ni moja ya uimarishaji wa elimu ya msingi lakini pia uendelezaji walimu nayo pia imekuwa ni sehemu ya kuweza kuelimisha elimu ya msingi. Kwa hivyo wizara haijalitupa nyuma lakini inaliona na ndio maana ikaweka kipengele au kifungu maalum kwa ajili ya uimarishaji wa elimu ya msingi.

Suala jengine Mhe. Spika, ni kuhusu changamoto ambazo inazikabili Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali mjumbe alitaja changamoto mbali mbali ambazo zinawakabili walimu, vikalio upungufu wa walimu, walimu kupandishwa daraja na mambo mengine. Mhe. Spika, tunakubali kwamba changamoto nyingi bado zinazikabili Wizara ya Elimu na ni jukumu la Wizara kuona inakabiliana na changamoto hizi na kuweza kuzipatia ufumbuzi na haitochoka kuweona inazipatia ufumbuzi changamoto hizi, tunakubali kwamba bado tunazo changamoto nyingi. Kama Wizara basi inayo haki ya kuona changamoto hizi zinapatiwa ufumbuzi, tunakubaliana na mjumbe kwamba kweli bado ziko changamoto nyingi.

Mhe. Spika, suala jengine ni mishahara imeonyesha Mhe. Mjumbe mmoja kifungu cha mishahara kasima kinaonyesha ziro ziro tupu na alitaka ufafanuzi kwa nini kifungu hiki kinaonyesha ziro ziro tupu, suala hili pia lilijitokeza wakati wa Kamati ilipokuwa inajadili hotuba hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Nakumbuka kwamba lilitolewa jibu wakati ule na jibu lililotoka kwamba kifungu hiki kimewekwa katika Idara moja ya utumishi, kwa hivyo kuna sehemu ya Idara ya Utumishi Unguja na sehemu ya Idara ya Utumishi Pemba ndipo ambapo vinaonekana vifungu hivi vya mishahara.

Mhe. Spika, kuna suala la uezekaji wa skuli na Mheshimi Mjumbe alizungumza zaidi skuli ya Kizimbani kwamba ni skuli ambayo ina mabati ya *ASBESTO* mimi nadhani Mhe. Mjumbe atakubaliana na mimi kwamba tusubiri tumalize bajeti na nadhani Wizara itachukua hatua ya kuiingiza skuli hiyo katika mpango wa kuzifanyia marekebisho.

Mhe. Spika, kwa vile muda unakwenda nataka kumaliza masuala mawili yaliyobakia suala lililojitokeza jengine ni Chuo cha Ualimu Mchanga Mdogo je kuna hatua gani zilizofikiwa hadi hivi sasa, napenda nimuelimishe au nimjulishe Mhe. Mjumbe kwamba Chuo cha Ualimu Mchangamdogo imo katika Miradi ya World Bank, miradi ambayo inadhaminiwa na Banki ya Dunia

na miradi hii iko mingi na inakwenda hatua kwa hatua. Hatua iliyofikiwa katika mradi huu ni kama ifuatavyo.

Kwanza tunatarajia mwezi unaokuwa wa saba tutatangaza dhabuni za ujenzi na kutafuta mkandarasi wa Chuo hicho, lakini kuna hatua tayari zimeshachukuliwa ambazo ni kutafuta mshauri na michoro yake tayari imeshaletwa, lakini pia tukimaliza kupata mkandarasi tunategemea kwamba Septemba 2010 ujenzi unaweza kuanza rasmi ili kuweza kujenga chuo hicho cha Mchangamdogo.

Jengine skuli ya Sekondari ya Kwamtipura nalo pia Mhe. Muwakilishi alilieleza hili na akataka basi Mhe. Waziri wa elimu aonyeshe angalau kwenda kupiga *grader* katika eneo hili la Kwamtipura, napenda nimueleze Mhe. Mjumbe kwamba tayari ripoti ya mshauri imeshapatikana na michoro pia imeshawasilishwa lakini pia tunatarajia kutafuta mkandarasi na itakapokamilika hatua hizi basi ujenzi utaanza 2011.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa Mhe. Spika, ni suala la hati miliki ambalo limejitokeza wajumbe wameonyesha mazingatio yao kuhusu kwamba skuli nyingi hazina hati miliki, wameiomba Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyengine skuli hizi kupatiwa hatimiliki. Mhe. Spika, hili nawaomba wajumbe pamoja na taasisi zinazohusika tushirikiane kwa sababu lina matatizo yake na mara nyingi tumekuwa tukieleza matatizo ya upatikanaji wa hati za maskuli.

Moja tatizo ambalo linazikabili ni wakati wa upimaji wa maeneo ya skuli nimezungumza si mara moja wala mbili na Mkurugenzi wa upimaji kuona vipi tunaweza kupata ufumbuzi wa tatizo hili, lakini bado kuna tatizo huko mitaani migogoro mingi imekuwa ikijitokeza wakati wapimaji wanapokwenda kupima maeneo ya skuli. Kuna baadhi ya watu wanahoji kuwa ni maeneo yao kwa hivyo wapimaji mara nyingi wamekuwa wakishindwa kupima maeneo haya kutokana na migogoro ambayo inajitokeza, kwa hivyo ningewaomba Weheshimiwa wenzangu pamoja na viongozi huko mitaani tushirikiane kuweza kulitatua tatizo hili ili lipate ufumbuzi, ni suala ambalo linashirikisha taasisi mbali mbali tukiwemo sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Lakini pia Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, lakini pia sisi viongozi ambao tunahusika kupata ufumbuzi wa matatizo haya ya migogoro ya maeneo ya skuli.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya machache napenda tena niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali mia kwa mia, wajumbe mbe wote nawaomba tuipitishe sote bila ya kipingamizi bila ya buti. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nilikuwa naomba maji kidogo nashukuru sana kwa nafasi ambayo nimeipata kufanya majumuisho kwa michango mbali mbali ya waheshimiwa wajumbe. Nitangulize kwanza kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa jinsi ulivyotumia busara zako za kawaida za kuwapa nafasi wajumbe na hatimae tukapata jumla ya wajumbe waliochangia pamoja na wale wa maandishi kufika thalathini na mbili.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niwataje wote ambao wamechangia kama ifuatavyo:

1) Mhe. Ali Suleiman Ali
2) " Mohammed Ali Salim
3) " Mtumwa Kheir Mbarouk
4) " Makame Mshimba Mbarouk
5) " Rashid Seif Suleiman
6) " Haji Mkema Haji
7) " Said Ali Mbarouk
8) " Ali Denge Makame
9) " Omar Ali Jadi
10) " Asha Moh'd Hilali
11) " Salim Ali Hamad
12) " Ali Abdalla Ali
13) " Haji Faki Shaali
14) " Ali Mohammed Bakari
15) " Mzee Ali Ussi
16) " Ashura Abeid Fareji
17) " Hijja Hassan Hijja
18) " Nassor Ahmed Mazrui
19) " Mwanajuma Faki Mdachi
20) " Zakiya Omar Juma
21) " Thuwaybah Edington Kissasi
22) " Mahamoud Thabit Kombo
23) " Subeit Khamis Faki
24) " Abass Juma Mhunzi
25) " Hamza Hassan Juma
26) " Khamis Jabir Makame
27) " Ame Ussi Juma
28) " Najma Khalfan Juma
29) " Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini
30) " Muhiydin Moh'd Muhiydin
31) " Mansour Yussuf Himid
32) " Abdalla Juma Abdalla

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwashukuru wachangiaji wote waliochangia, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, lakini pia namshukuru sana Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa utulivu wake anaonyesha ametulia sana kipindi hiki kiasi ambacho aliwakilisha hoja zake kwa umakini sana kama kawaida yake.

Lakini kwa ujumla naomba niwashukuru waheshimiwa wote ambao walichangia hoja mbali mbali, vile vile namshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuweza kunisaidia hoja nyingi sana na mimi nitakwenda kwenye mambo ya ujumla tu ili tunusuru wakti na tuwahi mambo yenyewe.

Mhe. Spika, la ujumla ambalo limezungumzwa na hili nalipa nafasi ya kwanza ni suala la ubora wa elimu. Tunakubali kabisa kwamba bado hatujafika kile kiwango ambacho kila mmoja angetarajia kifike. Suala la ubora wa elimu linaendana na mambo matatu ya kimsingi.

1) Huwezi kupata elimu iliyobora kama huwa walimu wenye sifa za kutosha.

2) Pia upate na mahali pa kufanyia kazi kwenye maeneo kama majengo mazuri.

3) Pia upate na nyenzo kama vitabu na mambo yanayohusiana na hayo kwenye taaluma.

Mhe. Spika, kwa kadiri hali inavyokwenda nasema pamoja na matatizo tuliyokuwa nayo lakini tusijivunje moyo. Kiwango chetu cha elimu kuna waheshimiwa wamesema nimemsikia Mhe. Muhunzi na waheshimiwa wengine wamesema kwamba kuna Vijana wa Kizanzibari ambao katika wale wataalamu mia moja mabingwa basi Wazanzibari wamo wawili.

Mimi naamini kuna wengi sana ambao ni wataalamu, kuna ndugu zetu wa Zanzibar ambao wapo hapa hapa lakini wapo ambao wapo nje ya Zanzibar na nina hakika kwamba ni mahiri na mahodari sana. Wanafunzi wetu wengi ambao wametoka Zanzibar kina wanapokwenda duniani basi wanafanya vizuri sana.

Jana kuna kijana mmoja katoka Malaysia anasoma mambo ya uhandisi wa ndege, kasoma mwaka mmoja tu pale Malaysia mwaka uliofuata sasa hivi wamemuajiri ili na yeye asomeshe pale pale hata hajamaliza ile digirii yenyewe, kaonyesha upeo mkubwa sana. Kwa hivyo vijana wa Zanzibar akili

wanazo na akili hizi zinapatikana kwa kusomeshwa na walimu hawa hawa waliokuwepo hapa Zanzibar, au waliokuwepo wakati huo.

Kwa hivyo suala la ubora wa elimu lina umuhimu mkubwa sana, tuna matatizo kweli baadhi ya wanafunzi mpaka leo wanakaa chini. Walimu wa sayansi tuna upungufu nao mkubwa sana. Hili ndilo ambalo hivi karibuni lilinifanya nisafiri, nimekwenda Iran, nimekwenda na Oman katika njia mbali mbali pamoja na India katika kuhakikisha kwamba tunapata walimu wenye sifa.

Kuna Mheshimiwa mmoja nadhani Mhe. Rashid Seif alizungumza kwamba kulikuwa kuna wakati fulani walimu walikuwa wanatoka India. Lakini wakati ule degree za Zanzibar zilikuwa zinahesabika ndio maana wakatoka walimu kutoka India. Kweli tunahitajia lakini bado ukitizama hesabu zetu, takwimu zetu walimu wenye degree ni wengi sana. Lakini kwa bahati mbaya kidogo wengi wenye digirii hizi ni wale ambao wamesomea masomo ya art, sayansi ni kidogo sana. Ndio maana tukaanzisha utaratibu wa kuimarisha sayansi.

Hivi sasa tunaanzisha kozi maalum za digrii ya kwanza hapo Chuo Kikuu cha SUZA, *College of Education* Chukwani na kwenye Vyuo vyetu vyengine vilivyokuwa nje ya Zanzibar. Lakini pia diploma yetu ya sayansi bado inaendelea kutolewa kwenye vyuo vyetu. Tumeondosha masomo ya cheti kwa sababu kwa hivi sasa hatuhitaji tena kuendelea kusomesha walimu wa cheti. Walimu wa diploma tuliwapeleka kipindi hichi karibu walimu 1200, wapo pale na kwa kweli baada ya miaka miwli mitatu, tutakuwa na walimu wengi sana wa diploma, hata hao wa sayansi nao tutakuwa nao vile vile lakini itachukua muda kidogo.

Kwa hivyo bado naomba tuwe wastahamilivu, Rom ile haikujengwa kwa siku moja imejengwa kwa siku nyingi, tunakwenda. Lakini bado tunakubali kama kweli zipo changamoto ambazo zinahitajika. Na sisi kwa upande wetu tutajitahidi ili tupate *quality of education, quality teachers*, nao wanahitajia wapate *insentive*, ndiyo hizi ambavyo hivi karibuni tumezifanya na Ishallah tukijaaliwa tunatarajia kuzifanya nyengine huko mbele hali ya uchumi itakapokuwa inaruhusu.

Tatizo jengine ambalo limezungumzwa kwa umakini na kwa wingi sana ni suala zima la vyuo vya Qur-an. Hili kwa kweli tumejibebesha sisi Wizara ya Elimu lakini wenyewe hasa ni watu wa Katiba na Utawala Bora, wapo watu wa Mufti na wengineo, hata Tawala za Mikoa wanaweza wakatusaidia. Lakini sisi kwa vile ni taaluma tumesema tujiingize. Kwa sababu na mimi mwenyewe nina *interest* nalo hili ndio maana katika ziara zangu ambazo nazifanya katika maskuli mbali mbali huwa naomba nipangiwe kwenye vyuo vya Qur-an. Kile

ambacho tumekiweza tumeweza kuwasaidia. Maombi yaliyokuja mengi sana hapa ni masuala ya kusaidia ujenzi kama tunavyosaidia katika skuli nyengine.

Mhe. Spika, kwa sasa hivi siwezi kuahidi kama tutasaidia ujenzi lakini kila tutapopata wafadhili au na sisi wenyewe tutakapopata wasaa ni sadaka hii waheshimiwa na nyie pia msiwe wazito sana jitahidi mtakwenda kuyakuta huko mbele tukijaaliwa. Tulichoweza misahafu na vijuzuu tumetoa na pale ambapo tunafanya ziara katika vyuo vya qur-an hivyo basi huwa tunasaidia kutoa misaada kama mabati, saruji na vifaa vyengine. Na wale wote ambao wameomba niwatembelee kwenye vile vyuo vya *Qur-an* basi ishallah wanastahamilie kidogo chungu kipo jikoni tukimaliza tu basi tutakwenda kwenye hizo ziara zetu tukijaaliwa Ishallah.

Vile vile wamezungumza suala la maslahi ya walimu wa vyuo vya qur-an. Mimi nakubali ni jambo muhimu na tutaliona ni njia gani tunaweza kufanya ili tuweze kuona kwamba angalau tunawapatia sabuni kwa utaratibu . Lakini kwa sasa hivi kwa bajeti hii haitowezekana, lakini tutaweza kufanya utaratibu katika miaka ijayo tuweze kulifikiria. Pale ambapo Mungu atatupatia uwezo na kutafuta mtu ambaye ataweza kutusaidia au Shirika basi tutakuwa nao kama ISESCOW Shirika moja la Kiislamu ya Sayansi na Utamaduni, liliwahi wakati fulani likawa linatupatia mishahara kwa walimu wetu wanaofundisha lugha ya kiarabu pamoja na dini ya Kiislamu. Kwa hivyo bado tuna ihsafu nzuri na wale na tutaendelea kuzungumza nao ili kutizama uwezekano na hivi vyuo vya qur-an kuviimarisha.

Mhe. Spika, vile vile kumezungumzwa uhaba wa vifaa vya maabara (*Laboratory*). Ni kweli tunakubali vyumba tunavyo lakini vifaa havipo na lazima tukubali kwamba kweli tunaukosefu mkubwa sana. watoto wetu wanafanya mitihani katika mazingira kama hayo magumi ni kweli. Lakini pamoja na hayo yote watu wanaondoka na (A) wanaondoka na (B) ni juhudi ambazo wanazifanya walimu wetu kwa njia mbali mbali kutafuta ili kuhakikisha wanawasaidia vijana wetu. Tayari katika mpango huu wa Benki ya Dunia tumefanya jitihada na tunatarajia vifaa hivi vya maabara vingi vitapatikana hivi karibuni na tutaanza kuvisambaza tukijaaliwa.

Tatizo la wenzetu wa Benki ya Dunia hawa urasimu wao ni mkubwa sana. Naamini na nakubaliana na waheshimiwa hata mimi linakereketa sana, nagombana na wakurugenzi, nagombana na maafisa wangu naona kama hawafanyi kazi. Hivi sasa tumeshatoa ruhusa ya ujenzi wa skuli tatu zile za Sekondari kwa Mkoa wa Kaskazini. Nilipouliza juzi nikaambiwa sasa ataitwa yule *contractor* waje wafanye *negotiation* kwanza wakimaliza halafu wapewe mkataba sijui atie saini yake, kwa hivyo kuna wiki mbili au tatu nyengine.

Mimi nilitarajia wiki hii tungetia saini mapema iwezekanavyo ili na nyengine tuweze kuzisaini vile vile. Lakini tusiwe na mashaka katika kipindi ha wiki mbili au tatu zijazo Skuli hizi 15 zote tutazisaini na ma – *contractor* watapewa kazi kwa kuanza ujenzi. Zile nne za Sekondari kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwa Mtipura, Kiembesamaki, na sehemu za Utaani basi tusiwe na mashaka mambo hayo yatakuwa mazuri. Ukarabati nao vile vile kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri skuli tatu zile za Skuli ya Fidel –Castro, Skuli ya Uweleni, Utaani na kwa hapa Unguja, Skuli ya Forodhani, Hamamni na Tumekuja nazo Ishallah hazitochukua muda mrefu, tatizo ni rasimu wa Benki ya Dunia.

Mhe. Spika, mimi ningetamani tokea miaka miwili hata kuiweka *statement* ya ujenzi wa skuli naona tabu kwenye kitabu changu kwa sababu naona wenzangu hawatoniamini. Na wakati huu nataka waniamini sana sitaki niseme uwongo. (Makofi)

Mhe. Spika, ma – *dictionary* yamezungumzwa, nakubali na hili napenda nihakikishe kwamba nitalichukuliwa hatua ili tuweze kupata madictionary ya kutosha kuyapeleka katika maskuli.

Hati za kuli ni kweli lakini hili tuliwaachia Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya watusaidie kwa kushirikiana na masheha, tuliwambia watakapokwama watuletee na *Ishallah* sisi tutajitahidi.

Scheme of Service ya uwalimu imezungumzwa. Mheshimiwa ni kweli tumejitahidi, kuna matatizo yamejitokeza baadhi ya walimu na imechukua muda. Lakini naahidi kwamba katika kipindi kifupi kijacho matatizo ya walimu hawa ambao walipata msukosuko wa hapa na pale na matatizo basi nitachukua hatua za kufaa. Hatukutoa maelekezo au pengine ufafanuzi kwamba nyongeza hizi zimetolewa vipi.

Mwaka 2007 walipofanyiwa marekebisho ya mishahara wafanyakazi wote, walimu wangu hawakufanyiwa marekebisho. Kwa sababuu wafanyakazi wote wa mawizara walifanyiwa *consolidation* ya mishahara yao walimu hawakufanyiwa. Walimu walitamani ile 25% yao waiyone kama ilivyo isichanganyishwe na pale kwa sababu ile ni tunzo maalum au ahsante kwa kazi ya kufundisha na wanapewa wale ambao wapo madarasani, hata kama ni mwalimu lakini huko darasani hupati ile 25%, tumehangaika nayo kwa muda mrefu sana.

Mhe. Spika, pia kulikua na tatizo la nyongeza za mishahara zilikuwa hazitolewi tokea mwaka ule. Tukafanya juhudi maana wale walimu wa zamani wanalalamika kwamba mishahara yetu sisi sawa na walimu walioajiriwa juzi na

jana. Tukafanya hesabu tukaanza kupandisha nyongeza za mishahara kila baada ya miaka miwili tumepandisha nyongeza kama miaka 20 au 30 tumeongeza nyongeza zile. Na wale wapya tumewaongezea nyongeza lakini wao hatukuwapa miaka miwili tumewapa baada ya miaka mitatu ili kuwe na tofauti kidogo. Nina hakika kwamba sasa hivi mambo mengi yamekaa sawa na yaliyobakia tutajitahidi kuwayaweka sawa ili kila mmoja apate haki yake. Wasiwe na wasi wasi walimu bado serikali itajitahidi kuhakikisha tunatengeneza maslahi mazuri.

Mhe. Spika, suala la michezo maskulini. Nadhani sote tunaelewa kwamba michezo yetu na tunajitahidi kuiyendeleza.

Mhe. Spika, jengine napenda nilizungumze mikopo ya elimu ya juu. Ni kweli bajeti ni ndogo wanao *qualify* ni wengi. Tusijivunje moyo tukasema kiwango chetu cha elimu kiko chini. Nasema tena vijana wanaopasi *University* sasa hivi ni wengi mno tena wenye sifa. Wale ambao tumeona kwenye daraja la kwanza hata kama 38 au 40 wa daraja la pili wapo kama 180 na zaidi, wote wale wana *qualify form six* kuingia kwenye *University* kwa kutegemea na *areas of interest* . wapo ambao wengi wao safari hii waliopata daraja la kwanza bahati nzuri Mungu amejaalia wamekwenda kwenye sayansi.

Mhe. Spika, tumejaribu kuwapangia kwenye maeneo ambayo watapata sayansi kuhusu kusoma. Bahati nzuri tumepata *scholarship* nyingi sana na zimaendelea kutangazwa zipo za Iran zipo za Oman, tumapata nafasi vile vile za uhakika mwaka huu September hii, wapo wale vijana waliokwenda kusomea mambo ya mafuta, wengine wamekwenda kwenye mambo ya *medicine*. Mimi nadhani ikifika Disembar vijana wetu wambao wapo nje kwa masomo katika masuala mbali mbali haya watakuwa ni vijana wengi sana. Ishallah baada ya miaka mitatu Zanzibar itakuwa tumepiga hatua kubwa sana katika maendeleo ya elimu. Safari ni hatua kwa hivyo tuwe wastahamilivu.

Nakubali vile vile tatizo la nyumba za walimu ni tatizo moja ambalo linahitajiwa kufanyiwa ufafanuzi na nalifafanua hili kwa sababu katika katika skuli hizi ambazo tunazijenga za vijijini basi tutajenga na nyumba za walimu. Katika kila skuli tutakapojenga tutajenga na nyumba za walimu zisizopungua tatu ili kupunguza tatizo la uhaba wa walimu.

Pia tutajitahidi katika bajeti inayokuja uwe ni mradi maalum wa ujenzi wa nyumba za walimu. Kwa sababu tunapata matatizo sana, ili kuhakikisha kwamba walimu hawa wanafanya kazi katika mazingira mazuri. Lakini walimu wanaotoka mjini ukiwapangia shamba, shamba mjini siku hizi, miye mmoja mshamba lakini nina *I feel* niko mjini kule Makunduchi.

Zamani nilikuwa nawatoa walimu mjini hapa wanafika pale Jumatatu na Jumaane Ahamis wanaondoka wanasomesha siku nne kwa sababu ya matatizo yaliyokuwepo wakati ule vijijini. Lakini sasa hivi kila kitu kinapatikana huko, barabra nzuri, umeme, maji safi Alhamdulillah, kwa hivyo ishallah tutazijenga nyumba hizi wale walimu wenye matatizo ya uhaba wa walimu katika maeneo yao tutajitahidi kuwapaleka huko.

Mhe. Spika, pia tunafanya mpango wa kupata walimu wataalamu. Tumeshazungumza na Serikali ya India mazungumzo ambayo nimefanya hivi karibuni kupata walimu angalau 20 kwa kuanzia. Na hizi Skuli za Sekondari ambazo zinakuja zitakuwa zina wataalamu wa hesabu na sayansi vile vile tutawapata.

Jengine ambalo limezungumzwa hapa ni suala la Skuli ya Kijichi kuitolea ufafanuzi, Mhe. Ali Abdalla. Skuli ile hasa imekusudiwa kwamba ni *model primary school*. Na kwa kweli ridhaa ya wazee nimeisikia kwamba wangefurahi kuona wale watoto wadogo ambao walikuwa wanakwenda masafa marefu tunawapatia elimu. Mimi kwa kushirikiana na wenzangu nilikuwa nina mawazo ile skuli tukaifanya kama ni *model primary school* sawa lakini ikawa ni *special school* kwa wale watoto ambao wana vipaji maalum tuwe tunawapeleka katika eneo la pale. Hili tutaliangalia na kuona uwezekano wa wale watoto wadogo kuwapunguzia masafa tukawapatia nafasi pale.

Suala la usafiri na nauli za walimu, mimi sidhani kama kuna uchelewashaji wa nauli za walimu. Kuna Mheshimiwa mmoja alipendekeza kwamba tuwapatie utaratibu wa usafiri, hawaingii. Tuliwahi kujaribu ikawa wanajichelewesha ikawa hawendi kule. Kwa sababu haja yao wapate zile pesa za nauli wafanyie mambo yao mengine. Sasa leo ukimwambia panda gari hapo pesa ya nauli tunakunyang'anya atasema hapana nipeni pesa zangu.

Kwa hivyo tumefanya jitihada hiyo huko nyuma lakini haikutusaidia. Jamani mtu nauli tunamlipa na sio kama zimepanda kiasi hicho. Kama kuna marekebisho ya nauli sisi tunarekebisha kutokana na hali ya wakati ule ilivyo na kama hazijarekebishwa basi hili naliahidi kwamba tutaondoka nalo tutakwenda kulirekebisha. Tunajitahidi sana kuona kwamba walimu waweze kufika kazini mapema. Isipokuwa hapa Chuo cha Kiislamu kuna matatizo, kuona kwamba wanafunzi wanawake wanakaa mabarabarani muda mrefu sana. Alhamdulillah nilipokuwa nataja tena safari yangu ya Oman kwani kule nilipata mengi fari hii. Nimeomba mabasi kule kama manne, matano, ishallah nimeahidiwa nitapata, lakini nikaambiwa omba zaidi kwa hivyo tutapata mabasi kwa ajili ya Chuo cha Kiislamu Mungu atujaalie pamoja na kupeleka Kiuyu kule kusaidia wanafunzi wetu wa Chuo cha Kiislamu na yatakayobakia tutawasaidia wenzetu.

Mhe. Spika, mambo ya kale yamezungumzwa namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri ametoa ufafanuzi.

Mhe. Haji Mkema alikuwa na wasi wasi eneo la kwa Bi Hole kuna mtu kapimiwa. Eneo lile zamani lipo pale na wakulima wa pale walikuwa wanalima sana eneo lile lakini lile eneo letu hasa tumelilima na tumelihifadhi vizuri. Eneo lile la pele Bungi hata ile miembe ile ni mali yetu vile vile lakini mimi sijawahi hata siku moja kuletewa hata embe moja, wanavuna wenyewe wananch tena kila mtu anakula riski yake, tumewaachia lakini ile ni mali ya serikali ambayo tunahitajia kuihifadhi katika eneo lile. Maeneo yamehifadhiwa vizuri na tutaendelea kuyahifadhi.

Mhe. Haji Faki uliuliza suala zima la Skuli yako ya Mkanyageni. Kweli tunajenga skuli 19 mbili katika kila Wilaya, Wilaya ya Mkoani tunajenga 2. Kweli kuna bado skuli moja ambayo inahitajiwa kujengwa hii ni BADEA. Hii *Model Secondary School*, hii umebahatika wewe Mwakilishi wa Mkanyageni na Mwakilishi wa Makunduchi. Mimi sikufanya haraka pale mwanzo katika zile mbili za mwanzo nikasema tupatiwe moja tu. Sasa imekuja hii tumeongezea kidogo hesabu pale.

Hizi tayari zimeshafika hatua nzuri sana na Mwenyezi Mungu akipenda siku si nyingi lile eneo litakaguliwa na mambo ya ujenzi yatakuwa yanakaribia kuanza. Kwa hivyo ipo na wananchi wako u watoe wasi wasi. Kwa hivyo Wilaya ya Mkoani kutakuwa na skuli za Sekondari tatu za kisasa si jambo dogo, Mhe. Mula hii kazi nzuri unayoifanya.

Nimekubali vile vile tumeanzisha utaratibu wa sera mpya ya Elimu wa Maandalizi. Kwa hivyo tuandae *train program* nzuri kwa walimu wa *Nursery school* ni jambo la kimsingi na hilo tumejiandaa na tayari hiyo *package* ya *train* ipo tayari na *Ishallah* tukijaaliwa lengo hasa kujenga Chuo cha Uwalimu kwa ajili ya Skuli za maandalizi. Kwa sababu pale Saateni hapana Chuo cha Uwalimu kile ni kituo cha walimu kama zilivyokuwa TC nyengine. Wengine wanakuja wanasema kwamba tumeshapata *certificate* ya Saateni. *Certificate* ile sio kama ni ya chuo isipokuwa ni ya kituo. kama ni *certificate of attendance* kwa hivyo haitoku – *qualify* wewe kwamba tuweze kukuajiri.

Mhe. Spika, masuala ya *vocational training* nayo yamezungumzwa na mimi napenda niyazungumze kwa ufupi kwamba ni kweli tumeanza. Lakini nimesikitika kusikia taarifa hii kama ni sahihi nitazifatilia. Kwamba pale vitongoji wanafunzi wanakaa tu hawasomeshwi kwa sababu pale kuna *department* kama sikosei kama tatu zimeanzishwa. Sasa kama hawasomeshwi kwa sababu gani? Kwa sababu walimu tuliwachukua Chuo cha Karume, tumewapeleka kule makusudi wengi tu. na tume - *invite* na walimu wengine

vile vile wamekuja. Kwa hivyo hili napenda nilichukue Ishallah nikalifanyie kazi.

Mhe. Spika, nakubaliana na wazo la kuimarisha hivyo vituo vyenyewe vya kazi za Amali. Tumeanzisha kwa gharama kubwa na mamlaka tayari imeshaundwa. Bahati nzuri ina bodi nzuri, tunahakikisha kwamba tunashirikiana nao vizuri kuhakikisha kwamba vituo vile vinaimarika vizuri zaidi. Ni hazina kubwa sana na Ishallah tukijaaliwa tuna nia ya kujenga vituo vyengine kama vile katika Mikoa mengine iliyobakia.

Ujenzi wa SUZA unaendelea vizuri. Mhe. Haji aliuliza kwamba awali kulikuwa na mazungumzo au makubaliano kwamba tunajenga Idara ya Uhandisi. Ni kweli *block* zilizokuwepo pale ni nne, pana *block m*oja ya *administration*, moja. ya *library*, halafu kuna moja *department education* ambayo itakuwa *education* kwa ujumla na nyengine ya *engineering* kwa hivyo tukijaaliwa tunatarajia ikiwa kazi zinakwenda kwa *speed* inayokwenda sasa hivi inawezekana pengine *between September* au *October* basi angalau ma *block* mawili pale tukayafungua na yaliyobakia tukijaaliwa yatakuja kufunguliwa pengine baadaye. Lakini *department* ya *engineering* pale ipo na hilo ni jambo la kimsingi na tutalihimiza kwamba litendeke.

Mhe. Spika, sambamba na hilo Chuo cha Karume nacho tunakiimarisha sana. Sasa hivi wapo katika hatua nzuri sana za kuimarisha. Wameshazungumza na Serikali ya Marekani kwa sababu wao ndio waliokijenga Chuo kile na kuna muelekeo wa kutusaidia. Tutajitahidi kuimarisha *technical education* ili iweze kufanya kazi zake vizuri zaidi katika taasisi ile.

Pia Skuli ya Kengeja *technical* pamoja na Mikunguni hasa ya Pemba sasa hivi tumeanza kutenga fedha, tumeendelea mwaka jana na mwaka huu tunajenga majengo mapya ya kuongeza lakini na vifaa vingi tumepeleka kipindi hiki kwa ajili ya kusaidia usomeshaji wa pale. Pia pendekezo hapa kwamba sasa *high time* kwamba SUZA waweze kutoa digiriii ya pili. Na mimi nakubaliana na wewe Mheshimiwa kwamba kweli *they is need* kwamba tuwe na *degree* ya pili na ikiwezekana. hata *doctor degree* kwa sababu ikiwa digrii ya *research* haina haja kwamba mpaka lazima upate majengo, hata na hilo linawezekana.

Mhe. Spika, jengine lilozungumzwa Waheshimiwa wengi wanasema kwamba wanafunzi tuwapige bakora. Walipendekeza kwamba fimbo ziweko. Wizara haijasema kwamba watoto wasipigwe isipokuwa tumesema ni vizuri tukatafuta adabu mbadala ikiwa kuna elimu mbadala basi na ababu mbadala hakuna. Kwa mfano mwanafunzi kachelewa badala ya kuwa umekaa mwalimu mlangoni na bakora pale mwanafunzi hapiti atahangaika huku nje, atembea tembea tu. Lakini hebu mruhusu aingie ndani, andika jina lake baadae mpe kazi ya bustani

za kilimo, mfundishe ni sehemu ya *training* vile vile. Kama kachelewa andike mara mia moja mara mia mbili pale wenzake wanaondoka si chelewi tena, si chelewi tena hizo ndio adabu mbadala na zinaudhi zaidi kuliko hiyo bakora.

Mtoto ukimuweka wakati wenzake wanaondoka ukamwambia wewe ubakie pale anaona ni adabu kumbwa mno, hakubali yuko radhi atakwambia mwalimu bora nipige bakora lakini niondoke na wenzangu. Lakini na mwalimu pia itakuwa tunamtia adabu pale, kwa sababu itabidi wanafunzi hawakai peke yao na mwalimu nayeye pia itabidi abakiye.

Sasa hii kazi si ndogo lakini waheshimiwa nasema kwa mujibu wa taratibu za kisheria za c*opra punishment* unaruhusiwa kumpiga mtoto au kumtia adabu mtoto na mwalimu mkuu ndio aliyepewa amri hiyo au dhamana hiyo. Kama mwalimu mkuu hawezi kuchapa kwa sababu kuna mwalimu anam – *delegate* kwamba mtie bakora, tena bakora zenyewe umeambiwa maeneo ya kupiga. Leo tumeshuhudia hapa kesi za wanafunzi.

Mimi sikumoja wakati nafundisha Skukli ya Makunduchi nilikuwa na mwenzangu usimtaji kwa sababu mnamjua nikimtaja. Kaja Mzee akasema namtafuta mwalimu fulani na yule mwalimu fulani ndiye nilikuwa nazungumza naye mimi, kachukua panga mkononi, zamani sana mwaka 77 wakati huo. Nikamwambia mwalimu huyu leo hakuja, nikamtizima yule mwenzangu kijasho kinamtoka. Nikasema nitajitahidi leo sikutaji leo. Bahati mbaya kampiga bakora yule mtoto mkono umevunjika. Kuna baadhi ya watoto wengine wamepiga mpaka wamepoteza macho.

Sasa tusiruhusu tu kupiga, tupige kwa utaratibu uliowekwa. Mimi nasema tena kumchapa mtoto kwa kumfundisha haijakatazwa isipokuwa kupiga kwa kile kiwango ambacho sio cha kibinaadamu. Tuchape kumfundisha, tukimchape kumuumiza. Kweli wala sisi hizi hatukufuata mataifa ya nje kama wengi mnavyofikiria. Kweli Swiden wapo mstari wa mbele na mimi nimekuwa nikihubiri hivyo, nasema jamani kupiga hakusaidii na wala hakulei. Nyumbani unaweza ukawapiga weee watoto na wala wasikusikie.

Kuna Mheshimiwa mmoja kasema hapa kapigwa alikuwa sugu kweli kweli na akabakia vile vile kasema kajirekebisha siku hizi tu, lakini alisema alikuwa suguu kweli kweli, kajirekebisha siku hizi tu. Sasa mimi nakubali kweli bakora hazilei lakini nasema zinafundisha, lakini tuwe makini kafika hilo.

Mhe. Spika, kuhusu matumizi ya simu. Hili nimelisema na naendelea kulisema nimepiga marufuku wanafunzi kupewa simu na nasema tena jamani tangazo hili bado nalitoa agizo hili nalitoa ni marufuku kwa wanafunzi kuchukua simu maskuli. Kazungumza vizuri Mhe. Ali Moh'd Bakari anasema tatizo hili ni

wazee wenyewe. Siku moja nilisema hapa Mhe. Spika, kuna skuli fulani walifanya zoezi la kukusanya simu. Baada ya kufanya zoezi lile simu zile nilikuja nikaletewa Afisini kwangu zinafika 12. zile simu moja tu nikaambiwa nifungue nitizame humo ndani. Nilishtuka hao ni watoto wa *form one*, miye maisha yangu sijaona mambo hayo na Mungu aninusuru nisiyaone, hatari. Hata ile picha yenyewe imeandikwa "**Hatari**" na hatari kweli.

Mhe. Spika, nakuombeni wazee, wananchi, Waheshimiwa hili tulikemee kwa nguvu zetu zote watoto kuchukua simu, zinamuathiri mtoto. kimawazo na kisaykolojia, *concentration* yake inakuwa haipo pale, kweli tunawahitajia inapotokea dharura lakini kama dharura skuli kuna simu za dharura zipo. Kwa hivyo bado nasema Waheshimiwa kwamba hili Serikali imeshapiga marufuku utumiaji wa simu katika taasisi zote kuanzia maandalizi mpaka juu, kwenye vyuo vikuu mpaka watu wazima.

Waheshimiwa walitaja juu ya uwezekano au pengine kutafuta utaratibu wa kuimarisha usomeshaji wa mambo ya mitandao au ICT. Hivi karibuni Wizara yangu imetiliana saini na Marekani kwamba skuli zote za Unguja na Pemba zitaunganishwa na mitandao ya *Intenent* na *Ishallah* tunatarajia pengine katika miaka miwili au mwaka mmoja ujao kila mwanafunzi wa Zanzibar anaweza akapatiwa *Compyuta* yake ya kufanya mazoezi na kusomea.

Mhe. Spika, kuna suala jengine limejitokeza.

Mhe. Spika: Wajumbe tunaokwenda kusali tusisahau kurudi haraka ili kumaliza shuhuli hii.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Kuna suala limejitokeza Mheshimiwa mmoja amezungumza la skuli mwalimu wake anampa tabu kidogo na sisi tutajitahidi kuchukua hatua Mhe. Hamza kulirekebisha hilo.

Halafu kulikuwa kuna suala zima la *peoples teacher ratio* tunaonekana kwamba mwalimu mmoja anachukua wanafunzi 28, kilichofanyika hesabu zake kwamba wanafunzi wote tuliokuwa nao na walimu wote tuliokuwa nao ukigawa ndio unapata ratio hii. Lakini kweli kuna baadhi ya maeneo kuna wanafunzi 100, maeneo mengine 200 inawezekana katika darasa. Wengi sana ni *large classes* au *big classes*, imetokezea *ratio* hii ukichukulia kwa ujumla tu lakini tunajitahidi kupunguza wingi huo na kwa kuweka walimu wawili mpaka watatu ili kuweza kusaidia tatizo hilo.

Nawashukuru sana waheshimiwa wengi waliozungumzia suala la bajeti ya elimu kamba iongezwe. Ni kweli inastahiki na Waziri wa Fedha nadhani anasikia na *Inshallah* hilo atalifanyia kazi.

Usomeshaji wa sayansi na teknolojia tutaimarisha katika nguvu zetu zote na kuhakikisha kwamba Ishallah mambo haya yanakwenda vizuri.

Maktaba Pemba tayari mipango yake imeshakamilika michoro yake na hilo tutajitahidi.

Mhe. Mwanajuma aliniomba kuna gofu la Sharifu Jini na nilishauriwa na mimi niende mara moja. Sasa naomba unipeleke mimi tu usije ukawapeleka na wengine. Kwa hivyo Ishallah tutafanya utaratibu ili nende huko kwenye pango hilo la Sharifu Jini tukaombewe duwa.

Lakini pia kuna vyuo vya qur-an ambavyo umesema vimefukilika basi mimi nadhani juhudi imefanywa kwani kuna Misikiti mingi ilikuwa imefukilika. Kuna ule wanaita Ikulu pale Tumbe nimeiyona vile vile ilikuwa imefukiwa kabisa na wameanza kuichimbua sasa hivi iko juu. Tumekuta vitu vingi ndani ambavyo vimekusanywa kwa kuhifadhiwa.

Kuna tatizo la kufutiwa matokeo, waheshimiwa wengi wamelizungumza, anafutiwa matokeo yote kwa kosa la somo moja. Haya tunayafanya hata sisi mitihani yetu ya Zanzibar kwa sababu haturuhudu watoto kufanya udanganyifu wa mitihani.

Kwa mfano mitihani safari hii imefutwa kuna skuli fulani yaani karatasi 30 zote zimekuwa na majibu ya aina moja. Sasa tatizo linatokezea wakati mwengine unakopia sasa katika kurejesha karatasi unasahau na lile bomu unaliingiza ndani ya karatasi, likifika huko linaripuka. Sasa hivi kule Baraza la Mitihani wameweka wataalamu maalum wa kusomea hati, nilitoa mfano hapa siku moja kwa wanafunzi wa skuli ya Makunduchi alifutiwa matokeo katika somo la *Civics*, akaja akaniambia kwamba mimi siamini kwamba nimefeli mimi nimepasi. Ripoti inasema kwamba hati zilionekana ni tofauti *page* ya juu na ndani hati ni tofauti.

Nikamuuliza wewe hukuandikiwa akasema mimi sikuandikiwa, lakini na yeye akaniuliza suala akaniambia nisamehe lakini mwalimu nikuulize. Nikamwambia haya niulize mimi mwalimu, unapopata buku jipya ukurasa wa mwanzo huwa unaandika hati nzuri sana halafu huku mbele unakuwa unachanganya tu, na mimi nilipoanza mtihani nimeanza kwa hati nzuri lakini muda ulikuwa unapotea na mimi ndio nikachanganya tu huko mbele. Mhe. Spika, mimi kweli nitachanganya maana yake ndio hati zangu mbaya ndio Mwenyezi Mungu alivyonijaalia, lakini wewe sifikirii.

Mhe. Spika, humu ndani waheshimiwa wana hati nzuri kweli kweli na kila akiandika mwanzo mpaka mwisho hazibadiliki. Kwa hivyo, hilo ni tatizo na tunajiharibu sisi wenyewe na jamii wakati mwengine inachangia, tunakwenda kwenye maeneo ya mitihani wanasimamia pale, wanaomba ruhusa wanakwenda kujisaidia, wakifika huko kwenye kujisaidia kuna watu wanawasubiri wanawapa karatasi zimeshajibiwa. Mhe. Spika, simu zimekamatwa zinapeleka masuala nje wanatuma ujumbe inakuja pale wakati mwengine zile simu zikija huwa zinalia.

Mhe. Spika, mwaka juzi nilikwambieni hapa kuna skuli fulani ilikamatwa na raba darasa zima ile raba ina majibu ya *multiple choice* zimeandikwa pale, mwanafunzi mmoja akimaliza kutumia raba anamwambia mwalimu naomba raba, inazunguka raba nyengine, mchezo ukawa ndio huo tu. Mhe. Spika, raba hiyo iko ofisini mpaka leo haya ni makosa ambayo yanatendeka na sheria zetu za mitihani tumejiwekea ukikutikana na kitu chochote ambacho hakihusiani na mitihani adabu yako unafutiwa matokeo yote. Kwa hivyo, tunaomba sana tusi-*encourage* watoto hata mara moja tukasema ah kakosea somo moja tu na pengine si somo moja, pengine sentensi moja tu au hesabu moja kwa hiyo masomo yote tisa anafutiwa. Kwa hivyo, naomba tulinde maadili haya ya kuweza kufanya mitihani kwa lilahi taala.

Mhe. Spika, kuhusu ajira za walimu wa 2007. Mhe. Spika, ni kwamba tunalijua hili tumepunguza kama walimu 500 lakini tutajitahidi huko mbele kuendelea kupunguza kadri hali itakavyokuwa inaruhusu. Vile vile kuna suala zima limeulizwa kwamba Mhe. Zakiya Omar Juma alisema anasikia kuna baadhi ya walimu wametumia vyeti feki, nakubali kwamba hilo ni kweli na tumeshalifanyia kazi na wako vijana fulani hivi sasa wanahojiwa na polisi na ikithibiti hatua za kisheria zitachukuliwa.

Mhe. Spika, udanganyifu wa vyeti huo haufanywi hapa Zanzibar tu sasa hivi, hivi karibuni tulisikia TCU wameanzisha utaratibu wa kuwapitia hawa Maprofesa wetu kutizama vyeti vyao na wamegundua kwamba kuna matatizo, baadhi ya vyeti sio sahihi. Kwa hivyo, hali imefikia hatua hiyo kwa hiyo na sisi hatuwezi kukaa tukangoja tusubiri tunafanya upekuzi wa kutosha ndio maana yake sasa hivi kabla ya kuajiriwa kwa mwalimu lazima tuhakikishe kwamba vyeti vyako ni sahihi.

Mhe. Spika, suala la maktaba nimeshalizungumza. Vile vile kulikuwa na ombi hapa la kuweka matuta Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi alilisema na naomba nimuhakikishie kwamba tutalifanyia kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ili kuhakikisha kwamba matuta hayo yanawekwa katika maeneo ambayo yanahusika.

Mhe. Spika, lilikuja suala kwamba kwa nini mwalimu hawi na leseni, leseni anapewa mwendeshaji pikipiki, gari lakini mwalimu hapewi leseni. Mhe. Spika, tulipokuwa kwenye sheria fulani Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi alivutiwa sana na skuli moja akamwambia Rais pale kwenye sherehe ile hii skuli imenitia hamu kwamba hata na mimi nije nisomeshe akapiga makofi sana. Lakini aliposimama Waziri wa Elimu katika kumkaribisha Rais akasema Mhe. Abdalla Mwinyi hajaamua kuja skuli hii kwanza apite pale wizarani tumpe leseni yake kwanza vyenginevyo kwa sababu leseni maana yake ni uthibitisho kwamba wewe umekuwa ni *train teacher* na tumekuruhusu ukasomeshe baada ya kuridhika na viwango ulivyokuwa navyo. Kwa hivyo, amekubali ameshakuja na tumeshampa leseni yake na ruhusa anaweza kuendelea kusomesha.

Mhe. Subeit Khamis Faki hayupo lakini amekuwa akilizungumzia sana suala la msikiti. Napenda nimuhakikishie kwamba tayari tumeshapeleka maombi yetu Falme za Kiarabu kwa ajili ya kujengewa msikiti pale Micheweni na *inshaallah* tutajitahidi. Vile vile kuhusu transformer Afisa Mdhamini amenipa taarifa kwamba ameshawasiliana na Afisa Mdhamini mwenzake na hilo tutajitahidi kulifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba tatizo hilo tunaliondoa.

Mhe. Spika, Mhe. Abass Juma Muhunzi alizungumza suala zima la uongozi wa skuli fulani. Mhe. Muhunzi nakuomba baadae kama ulivyosema mwenyewe nipatie jina la huyo mwalimu ili ashughulikiwe ipasavyo. Lakini pia umesema suala la ajira ya hawa wakufunzi wa pale SUZA. Taarifa nilizokuwa nazo ni kwamba taratibu zote zinafuatwa wala hakuna njia yoyote ambayo inatumika labda ya kufanya kitu ambacho sio cha utaratibu na walivyojiwekea pale kwamba anayefanya vizuri lakini kuna na vigezo vyengine wanavitumia.

Mhe. Spika, unaweza kuwa hodari sana darasani lakini ukawa mkorofi, na mara nyingi watoto mahodari wanakuwa machepe kidogo. Huyu pengine ni mwanafunzi hodari sana yeye hana matatizo, lakini kuna vigezo vyengine vinatumika na wanachofanya wanawachukua pale kwenda kuwapeleka kwanza wakapate masomo kama ni *first degree* wanakwenda kupata *master degree*, wakishapata *master degree* yao wanarudi na baadae wanafanyiwa mpango ili waendelee na *doctor degree*. Mhe. Spika, sasa hivi kuna vijana wengi sana nadhani hawapungui nane mpaka kumi wamepata kozi kama hizi ambao walikuwa wameajiriwa pale kama ni wakufunzi. Kwa hivyo, tunajitahidi kama pana kasoro za hapa na pale tutajitahidi kuzirekebisha.

Mhe. Spika, lilikuja suala zima la dahalia ya wanawake na mimi naliona umuhimu wake ni kweli tulifikiria tuwe na dahalia za wanawake. Tutaliangalia tutizame utaratibu ambao utaruhusu lakini tatizo tulilokuwa nalo sijui tujenge

dahalia ya *size* gani maana yake wanafunzi ni wengi kweli kweli wanaoendelea na masomo ya vyuoni.

Mhe. Spika, kuna mheshimiwa aliuliza suala zima la kuweza kuzibagua skuli kidogo hizi tukazipeleka pengine kwenye *community*, lakini ni kinyume chake sasa hivi hao wananchi waliokuwa na skuli za *community* basi wanataka skuli hizi zirejeshwe serikalini. Mhe. Spika, tutaangalia uwezekano gani ili tuweze kuzipatia *concentration* maalum ambayo itaweza kusaidia.

Mhe. Hamza Hassan Juma nae aliendelea kuuliza suala la vyuo vya kur-ani tutajitahidi na skuli yake tumeshamuahidi tutajitahidi kuijenga.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla amezungumzia suala zima la kufikiria zaidi masuala ya mishahara ya elimu. Hilo nimeshalieleza lakini pia ulipendekeza suala zima la uvuvi na kilimo.

Mhe. Moh'd Ali Salim alitaka ufafanuzi wa baadhi ya masuala yako naomba nimalizie kwa hoja zake Mhe. Mulla haraka haraka. Yeye aliuliza kwamba anaona bajeti hii inazungumzia pesa za serikali tu, pesa za wafadhili hatuzungumzii. Ni kweli bajeti hii ya serikali yetu sisi huwa inazungumzia kua-*proove* zile pesa za serikali za wafadhili mara nyingi zinakuwa tayari zimeshakuwa saini katika Wizara ya Fedha na wao katika bajeti yao wanaonesha pesa za wahisani na mambo mengine. Kwa hivyo, sisi kazi yetu sikuzia-*proove* pesa zile kwa sababu zile zinatoka katika mfuko mwengine, isipokuwa sisi jukumu letu ni zile pesa za serikali.

Mhe. Spika, vile vile aliuliza suala la uimarishaji wa ujenzi wa Makao Makuu ni kweli pesa tulizipata lakini hazikutosha tumeomba nyengine tunajenga *parking* ya magari pale utaiona sasa hivi ukija pale ili ikae kama kweli ni wizara, pia upatikanaji wa vifaa kama komputa na tumenunua *furniture* nyingi sana kwa ajili ya afisi yetu ya Pemba katika utaratibu huo huo. Kwa hivyo, bado fedha tunazihitajia ni kidogo lakini alhadulilahi zinasaidia.

Vile vile suala la tatu aliuliza Baraza kushindwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi na kukosa ufafanuzi

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe *quorum* yangu sio nzuri nawaomba wale ambao wote wako nje hapo waharakie kuja ndani ili tuweze kumaliza shughuli hii. Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nadhani suala hili la uimarishaji na kufanya tathmini au utekelezaji wa miradi kuhusu pesa za

wafadhili za *BADEA* na Benki ya Dunia nimeshalitolea ufafanuzi kwamba hizi huwa zinaingizwa katika mfuko wa moja kwa moja wa Hazina.

Mhe. Spika, Mhe. Mulla vile vile alisema katika miradi ya mwaka uliomalizika zimetajwa asilimia za fedha zilizotolewa na SMZ lakini za wahisani nadhani jibu ndio hilo hilo, kwamba pesa ya wahisani mara nyingi zinakuwa katika Wizara ya Fedha. Nakubali kwamba mipango hii ya elimu huandaliwa kabla ya kutoa elimu stahili, bahati nzuri tumesema mipango yetu tumeiandaa kuna mpango wa miaka minane tumeiandaa na kuna mipango ya muda mfupi pia tumeianda. Kwa hivyo, tumejitahidi kujipanga vizuri na tumeandaa mipango ili tutakapoitekeleza tusipate shida na kwenye sera yetu ni ndivyo ilivyotuelekeza hivyo.

Mhe. Spika, kuna suala zima la wanafunzi wote walioandikishwa darasa la kwanza hupatiwa nafasi, je, madarasa hayo yana vikalio. Jibu ni kwamba hayana. Lakini sio skuli zote nyengine wanapata na Mhe. Mulla bahati nzuri wizara yangu kama nilivyosema huko nyuma na sasa nasema tena kwamba tumejiandaa vizuri sana. Kwanza skuli zote ambazo tunazijenga sasa hivi kupitia *SIDA*, *ADB* basi vikalio vinapatikana, lakini tumetenga bajeti yetu safari hii milioni mia moja katika pesa tunazopata kutoka Wizara ya Fedha kuhakikisha tunatafuta vikalio.

Mhe. Spika, tuna upungufu wa vikalio vingi sana kwa sababu nasema kiasi ya robo ya watoto wetu bado wanakaa chini, kwa hiyo tutajitahidi kwa kutumia nguvu ambazo Mwenyezi Mungu atatujaalia kuendelea kutafuta misaada. Mhe. Spika, tumepata misaada mbali mbali kutoka mashirika mbali mbali na tutajitahidi kuendelea. Hivi karibuni katika kipindi hiki kifupi tumejaribu kusambaza karibu meza na viti elfu moja.

Mhe. Ali Denge Makame alikuwa anasema kwamba meza zinaibiwa mbao, nadhani alikusudia yale madeski ndio yanayoibiwa. Mhe. Spika, jambo hili tena sio la wizara kwa sababu skuli ziko katika jamii hivyo watusaidie kuzilinda.

Mhe. Waziri Kivuli alisema kwamba skuli nyingi za serikali hazina vikalio, jibu ndio hilo Mhe. Mulla nadhani tutajitahidi tukijaaliwa. Mhe. Spika, kuhusu vitabu pamoja na muhtasari tumejitahidi vimepatikana na katika mradi mzima huu wa Shirika la Misaada la Marekani *USAID* tumetia saini juzi *twenty million dollars* alhamdulillahi ndio wataziunganisha skuli na mitandao. Pia vitabu vya darasa la kwanza hadi la nne tutavipata vya walimu na vya wanafunzi pia vitapatikana, na darasa la tano na la sita maandalizi yake yamekamilika. Pia sekondari masomo yote ya *science* na yale ya *art form one* mpaka *form six*

navyo vitabu hivyo *inshaallah* vitakuwa tayari maskulini kabla ya mwisho wa mwaka huu. Kwa hivyo, tutajitahidi kufanya hivyo.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka nimalizie suala la maktaba ambalo nimeshalizungumza ndio linahusiana na utaratibu huo huo kuna haja ya serikali kuandaa mpango wa kuwa na maktaba kila skuli. Mhe. Spika, hilo inshaallah tutajitahidi kwanzi tumeanzia kuziimarisha TC zetu katika kila TC kuna *library* ambayo inaweza kuwasaidia walimu wetu kwenda kufanya reference, lakini *library* isiwe kumsaidia mwalimu tu lakini iweze kumsaidia pia mpaka mwanafunzi. Mhe. Spika, baadhi ya skuli tunashukuru zimeanza kufanya hivyo na tunazipongeza na tunaomba waendeleee.

Mhe. Spika, nakubaliana na wewe moja kwa moja kwamba watoto wetu wanakosa kufanya *pratical* kutokana na uhaba wa vifaa. Nimejibu suala hilo mheshimiwa na tutajitahidi kadri itakavyowezekana kuhakikisha kwamba skuli zetu tunazipatia vifaa kutokana na huu msaada mkubwa ambao tutaupata kutoka Benki ya Dunia.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo Mhe. Mulla alitaka ni mahitaji ya walimu kutokana na sera ya elimu masomo ya madrasa ya msingi yanayofundishwa kutumia lugha ya Kiingereza, je, kuna walimu wa skuli za msingi wenye uwezo wa kusema Kiingereza sahihi. Mhe. Spika, suala hili ni zuri sana.

Mhe. Spika, ni kweli ndio maana yake *medium restriction* sasa hivi tumesema itakuwa darasa la tano na la sita ni Kiingereza, ili kuanza tokea chini kuweza kuwaimarisha vijana wetu. Lakini tumeandaa mpango maalum wa mafunzo karibu walimu mia tano tutawachukua kuwapa *training* kwa ajili ya kuwaandaa walimu hawa waweze kufundisha kwa Kiingereza vizuri sana na *inshaallah* tusiwe na wasi wasi Mzanzibari akisema Kiingereza basi utafikiri anatoka Uingereza, ni kweli kabisa hilo Mwenyezi Mungu ametujaalia Wazanzibari ukizungumza Kiarabu, Kiingereza, Kiswahili ndio mambo wenyewe hasa Mungu ametujaalia kwa hilo.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mulla yaliyobakia tena nimeshayajibu anisamehe nimalizie kwa suala zima ambalo nimelizungumzia kwenye bajeti yangu kuhusu suala kuudumisha umoja wetu. Mhe. Spika, suala hili kama nilivyolizungumza kwenye bajeti kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa ina umuhimu mkubwa kwa mazingira yetu ya Zanzibar na mimi kama ni Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi nimesema ingawa wengine nawakera nikisema hili wanisamehe lakini itabidi niseme kwa sababu tumeshajua tatizo hili lilivyo na tumeshayaona huko nyuma hatuwezi kurudi kule tulikotoka. Kwa hivyo, sisi nasema kwamba kwa niaba na wizara tumetia kwenye kitabu cha

bajeti kwamba tunaliunga mkono jambo hili na nawaomba waheshimiwa sote tuliunge mkono jambo hili kwani lina faida kubwa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru waheshimiwa wote waliochangia, kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunivumilia na kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa kunipa nafasi hii na leo kusimama hapa mbele yenu ili kuweza kutoa majumuisho ya bajeti hii. Pia nawashukuru sana wale wote ambao wamenitakia kheri katika maamuzi yangu hayo na *inshaallah* ninachowaahidi kwenu kwamba tutafurahi sote. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 23 – WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Kifungu 04	Idara ya Mipango na Sera	10,000.000
Kifungu 05	Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale	125,720.000
	Jumla ya Kifungu	**135,720.000**

FUNGU 23 – WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Kifungu 04 Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, leo hatupendi tupige buti hata kidogo lakini Mhe. Waziri asione vibaya tuko katika kutengeneza hatuna nia mbaya. Mhe. Mwenyekiti, mimi wakati wa kuchangia pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri aliyonipa lakini nilimuomba mambo mawili. Kwanza kunimalizia kuezeka banda langu la Mkanyageni na Michenzani na pili kilio

changu cha muda mrefu juu ya mabanda mabovu Kisiwa Panza yaliyojengwa tokea 1969 kwa udongo na mawe. Kwa bahati mbaya kutokana na michango mengi hakunipa ufafanuzi ni hilo tu, sitaki kumsumbua Mhe. Waziri wangu lakini atanisamehe kwa hilo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nadhani nilipozungumza nimezungumzia kwa lugha ya *jam* maana yake ni *plural* nimesema mabanda yote ambayo hayajakamilishwa tutajitahidi kuyakamilisha na lile lake limo. Kwa hivyo, mheshimiwa tutafanya hivyo *inshaallah.*

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, basi kama *jam inshaallah* tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, na mimi namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi kuhusu habari ya Skuli ya Sekondari tulisema Wilaya na eneo tukalitayarisha na tukapata hati lakini katika majumuisho yake sikulisikia hilo, naomba nipate ufafanuzi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina habari nayo kama kulikuwa na skuli ilipwa na hati zimepatikana kama anayo hati aiweke tayari tukapata fedha tutakwenda kumjengea.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Katika hizi sekondari kubwa za Wilaya tulipewa taarifa rasmi kuna mradi fulani ambao tutafadhiliwa ndio mpaka leo hatukupata jibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina taarifa kwamba kuna mtu alikwenda kumpa agizo akapiwe kule, lakini nasema kama imeshapimwa ndio ameshaturahisishia kazi basi astahamili kwa sababu hizo walizoambiwa watajengewa hawajajengewa, kwa hivyo astahamili kidogo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, na mimi wakati nilipochangia nimemwambia Mhe. Waziri kama bajeti wanayopewa Chuo cha Kiislamu Kiuyu ni ndogo sana kwa hiyo wafikirie na waliangalie kama shilingi hamsini milioni haziwezi kukidhi haja kabisa. Kwa hivyo, nilimuomba Mhe. Waziri afanye hivyo naona hajanipa jiibu suala hili.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, wakati najibu Mhe. Subeit yuko msikitini hasa itakuwa kazi kubwa hapa leo kila anayetoka msikitini kwamba aje aulize yale niliyokwishayasema. Mhe.

Mwenyekiti, mimi nimeshajibu kwamba suala hilo tutalishughulikia na kuona kiasi gani tunaweza kusaidia na nikasema mpaka mabasi tutawapelekea na msikiti tutajenga.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa nilikuwa msikitini lakini tuna utaratibu kama niliondoka mimi kuna watu wananisikilizia nikija nawasikiliza kama suala langu limejibiwa au vipi. Mhe. Mwenyekiti, kweli amejibu kama msikiti tumeshaomba msaada kwa wafadhili wa Wakiislamu na inshaallah tutajenga na mabasi tutajenga. Lakini suala la bajeti ya elimu wanaopelekewa Chuo cha Kiislamu ndio ninayomuuliza.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kinachotosha ngapi maana yake hizo ndizo tulizozipangia kwenye bajeti na bajeti unapewa *ceiling* panga hivi panga hivi. Kama tumepangiwa hamsini milioni, mimi nasema nataka nipeleke hata milioni mia moja hili tatizo lake limalizike. Kwa hivyo, basi tutafanya utaratibu tutasubiri msikiti na mabasi tusipeleke tutafute pesa kwa njia nyengine ili tuimarishe hayo mengine ya Chuo cha Kiislamu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Subeit labda nikueleze zaidi kiutaratibu bajeti ikishapangwa hatuna uwezo wa kuongeza fungu hiyo ni kwa mujibu wa kanuni, hayo ni masuala ambayo labda waziri azingatie kwa miaka ijayo lakini huu itakuwa kwa kweli ni ngumu sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa maelekezo yako na mimi najua kwamba bajeti ikishapangwa ndio imepangwa lakini nilifikiri kama waziri ataniambia kwamba kwa suala hili kwa mara hii limeshapangwa kwa hiyo tuvumilie Mwenyezi Mungu akipenda kipindi kinachokuja nitajitahidi ili bajeti ikuzwe. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 04	Idara ya Mipango na Sera	179,713,000
Kifungu 05	Idara ya Nyaraka na Makumbusho na Mambo ya Kale	106,820.000
Kifungu 07	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	23,184,536.000
Kifungu 08	Idara ya Elimu	101,000.000
Kifungu 09	Idara ya Mitaala na Mitihani	

Mhe. Moh'd Ali Salim: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sikuwa na haja ya kumpigia buti rafiki yangu lakini kwa sababu kuna suala la msingi ambalo nimeagizwa na Kambi ya Upinzani nimuulize na bahati mbaya amesahau, niliomba kuwa hivi sasa umeshafika wakati wa kuwa na Baraza letu wenyewe

la mitihani na elimu ya juu iwe ni yetu wenyewe tusiendelee kung'ang'ania huko. Hili nafikiri sikupata jawabu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, pale niliposema na mengine tunakwenda kuyafanyia kazi pamoja na hili lakini hii miguu inaniaga hamna tatizo. Mhe. Mwenyekiti, katika sheria yetu mpya hii ya elimu ambayo inshaallah tutaiwasilisha hapa itakapomaliza taratibu zake, tumesema tutakuwa na bodi yetu ya mitihani. Kwa hivyo, tutaangalia hili tuendelee na mitihani yetu, au tunaweza kuchukua na mitihani kwa kutafutiwa kwa sababu ni muhimu ku- *maintain* na *quality* ya mitihani yenyewe. Nina hakika tunaweza katika sheria yetu mpya ambayo tutaileta tutakuja kuiona tutavyoichangia lakini suala la bodi la mitihani limo vile vile.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 09	Idara ya Mitaala na Mitihani	1,075,625.000
Kifungu 12	Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala	183,338,000
Kifungu 13	Idara ya Ukaguzi	43,600,000
Kifungu 14	Idara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia	7,800,292,000
Kifungu 16	Idara ya Mafunzo ya Ualimu	140,000,000
Kifungu 17	Idara ya Elimu Sekondari	120,408,000
Kifungu 20	Idara ya Mipango na Sera Pemba	64,723,000
Kifungu 21	Idara ya Nyaraka Makumbusho na Mambo ya Kale	64,723,000
Kifungu 21	Idara ya Nyaraka Makumbusho na Mambo ya Kale Pemba	8,569,000
Kifungu 22	Idara ya Utumishi na Uendeshaji Pemba	9,283,798,000
Kifungu 23	Idara ya Elimu Pemba	115,885,000
Kifungu 25	Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala Pemba	67,686,000
Kifung 24	Idara ya Ukaguzi Pemba	12,857,000
Kifungu 27	Idara ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia Pemba	4,236,000
Kifungu 28	Idara ya Mafunzo ya Ualimu Pemba	58,105,000
Kifungu 29	Idara ya Elimu na Sekondari Pemba	15,761,000
	Jumla ya Fungu:	**42,618,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 23 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Kifungu 04	- Idara ya Mipango na Sera	50,850,089,000
Jumla ya Fungu:		**50,850,089,000**

(Kijifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa naKamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makisio hayo.

Mhe. Waziri wa Utalii Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na makisio hayo wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi kubwa mlioifanya kwa mashirikiano makubwa. Sasa tusitishe shughuli zetu hapa na nahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 29/06/2010 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:04 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 29/062010 saa 3:00 asubuhi)